# MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA TISA

**Kikao cha Kumi na Moja – Tarehe 13 Novemba, 2007**

(*Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi*)

**D U A**

*Spika (Mhe. Samuel J. Sitta) Alisoma Dua*

**HATI ZILIZOWASILISHA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. MUSTAFA H. MKULO):** Taarifa ya Mwaka ya Benki Kuu ya Tanzania, kwa Mwaka 2005/2006 pamoja na Taarifa ya Uchumi kwa Robo Mwaka iliyoishia Tarehe 30 Juni, 2007 ya Benki Kuu ya Tanzania: "*The Annual Report of the Bank of Tanzania for the year 2005/2006 and The Economic Bulleting for the Quarter ending June, 2007 (Vol. XXXIX No. 2) of the Bank of Tanzania"*.

**MHE. LUCY T. MAYENGA:** Mwongozo wa Spika

Mheshimiwa Spika, nimesimama kwa mujibu wa Kanuni Na. 32 Kifungu kidogo cha Kwanza kuweza kuomba mwongozo wako kutokana na umuhimu na unyeti wa Taarifa hii ya Benki Kuu *(BOT)* nilikuwa naomba ruhusa ili Bunge lako Tukufu liweze kujadili kwa wakati muafaka taarifa hiyo. (*Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge nimeombwa nitoe mwongozo kuhusu haki ya Mbunge kudai hati iliyowasilishwa hapa Mezani ili iweze kujadiliwa na hiyo ni haki ya msingi. Nimeiafiki na nitachagua wakati muafaka ambapo Hati hii itajadiliwa. (*Makofi)*

**MHE. DR. WILBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Spika, nilichotaka kukisema kinahusu kifungu cha 32 ambacho mwenzangu ameshakisema.

**SPIKA:** Ni vyema basi. Kwa hiyo, tunaendelea.

**MHE. DR. LUCY S. NKYA (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA UWEKEZAJI NA BIASHARA):**

Taarifa ya Kamati ya Uwekezaji na Biashara kwa Mwaka 2006

**MASWALI NA MAJIBU**

Na. 142

**Barabara ya Mbande – Ruaha Mbuyuni**

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE (K.n.y. MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE)** aliuliza**:-**

Kwa kuwa, barabara ya kutoka Mbande–Mpwapwa–Gulwe–Kibakwe–Chogola–Kinusi Malolo hadi Luaha Mbuyuni inaunganisha *Trunk Road* na *Trunk Road*; na kwa kuwa, barabara hiyo ni muhimu kwani inawasaidia wananchi wa Kilosa, Mpwapwa na Kilolo kiuchumi kwa usafirishaji wa mazao kama vile Maharagwe, Vitunguu, Mbogamboga na Mahindi ambayo yanalimwa kwa wingi sana katika Vijiji vya Malolo, Idodoma, Malolo Mazaganza, Kinusi, Galigali, Matonya, Mang'aliza na Nyanzwa katika Wilaya ya Kilolo:-

Je, Serikali haioni kwamba, iko haja barabara ya kutoka Gulwe mahali inapoishia barabara ya Mkoa hadi Luaha Mbuyuni kupitia kwenye vijiji nilivyovitaja ikapandishwa hadhi kuwa ya Mkoa?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alisema:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa George Boniface Simbachawene, Mbunge wa Kibakwe, kama ifuatavyo:-

Barabara ya Mbande-Mpwapwa-Gulwe-Kibakwe-Chongola-Kinusi-Malolo-Ruaha Mbuyuni ina urefu wa jumla ya KM 198. Sehemu ya Mbande-Mpwapwa-Gulwe yenye urefu wa KM 69 inahudumiwa na Wakala wa Barabara Mkoa wa Dodoma *(TANROADS).* Sehemu ya Gulwe-Kibakwe-Chogola-Kinusi hadi Makao Makuu ni Km 107 iko chini ya Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapwa na inafanyiwa matengenezo kwa kutumia fedha za Mfuko wa Barabara. Aidha, sehemu ya Malolo-Ruaha Mbuyuni KM. 22 inahudumiwa na Halmashauri ya Wilaya ya Kilosa.

Barabara hii ni muhimu kiuchumi kwani maeneo mengi yanayopitiwa na barabara hii ni maarufu kwa kilimo cha mazao ya chakula na biashara kama vile Maharagwe, Vitunguu, Mpunga, Mahindi, Mtama, Ngano, Karanga na Mbogamboga. Pia imepita karibu na Bonde la Umwagiliaji ambalo lipo katika Kijiji cha Malolo. Barabara hii inaunganisha Makao Makuu ya Wilaya ya Mpwapwa na Barabara Kuu *(TANZAM HIGHWAY)* ya Iringa – Morogoro eneo la Ruaha Mbuyuni kupitia Makao Makuu ya Jimbo la Kibakwe.

Mheshimiwa Spika, ili barabara iweze kupandishwa hadhi, vipo vigezo vinavyozingatiwa, miongoni mwa vigezo hivyo ni:

Idadi ya magari yanayotumia barabara hiyo;

Shughuli za kiuchumi zinazofanywa na jamii katika maeneo katika barabara hiyo;

Idadi ya wakazi waishio maeneo yanayopitiwa na barabara hiyo; na

Iwapo barabara hiyo inaunganisha Makao Makuu ya Wilaya moja na nyingine au na Makao Makuu ya Mkoa na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Wizara ya Miundombinu bado inashughulikia mapendekezo mbalimbali kutoka katika Halmashauri mbalimbali nchini ili kujua ni barabara zipi zina hadhi ya kupandishwa daraja na kuwa za Mkoa kutokana na vigezo vilivyowekwa, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kuwa kwa upande wa Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapwa barabara zilizopendekezwa na kuwasilishwa Wizara ya Miundombinu ni:-

1. Gule-Rudi-Chipogoro KM 108
2. Mpwapwa – Lumuma KM 60
3. Makose-Malolo-Idodoma KM 78
4. Gulwe – Seluka KM 64

Na kwa kuwa barabara ambayo Mheshimiwa Mbunge anaizungumzia ni miongoni mwa barabara ambazo Halmashauri ilikwishapeleka mapendekezo ya kupandishwa hadhi Serikalini na hadi sasa Wizara ya Miundombinu inaendelea na zoezi la kuzitambua barabara hizo ili kujua ni zipi ambazo zitakuwa zimekidhi vigezo. Namwomba Mheshimiwa Mbunge awe na subira hadi Serikali itakapokamilisha zoezi kwa kuzingatia Sheria Mpya ya Barabara *(Roads Act*) ambayo ilipitishwa na Bunge lako Tukufu mwaka huu.

**MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, lakini pia niipongeze kwamba Serikali inatambua umuhimu wa barabara hii kwa sababu inaunganisha barabara ya *Trunk Road* kwenda *Trunk Road* kama Sheria ya Barabara tuliyoipitisha juzi inavyosema.

Mheshimiwa Spika, nina maswali mawili madogo ya nyongeza. La kwanza, kwa kuwa umuhimu wa barabara hii ameukiri dhahiri Mheshimiwa Naibu Waziri. Je, ni lini sasa pamoja na hiyo subira angalau kujua tu maana barabara hii ndiyo ukombozi wa watu wa Wilaya ya Mpwapwa kwa upande wa kule Kusini ikitengenezwa barabara hii sisi maisha bora kule yatakuwa ni dhahiri kabisa na tutayapata kabla ya 2010. Je, ni lini hasa Serikali itapitisha barabara hii pamoja na subira hiyo ambayo tunaisubiri. Swali la kwanza?

Lakini la pili, je, barabara hii pamoja na umuhimu wake lakini inakutana mahali ambapo kuna mikoa miwili inakutana. Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu yuko tayari twende na yeye tukaitembelee barabara hii ili kuweza kuweka mazingira mazuri ya namna ambavyo tutajadili namna ya kupandisha barabara hii kwa sababu inakutanisha mikoa miwili?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, kuhusu swali la kwanza, ni kweli Serikali inatambua umuhimu wa barabara hii na mimi ni mmojawapo niliyepita sehemu ya barabara hii, ni muhimu kiuchumi pia kijamii. Barabara hii mpaka sasa hivi bado inaendelea kutengenezwa na Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapwa na kwa mwaka huu nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba imepangiwa fedha angalau kiasi cha shilingi Milioni 70 kwa ajili ya matengenezo ya barabara hii.

Kuhusu kwamba ni lini barabara hii itapandishwa hadhi ni mpaka hapo mchakato wake utakapokamilika ndipo tutakuwa kwenye *position* ya kuelewa kwamba barabara hii lini itapandishwa hadhi kuwa barabara ya Mkoa. Lakini Serikali inaitambua na inaendelea kuitengeneza kwa kupitia Halmashauri.

Kuhusu swali la pili nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tutawasiliana na Wizara ya Miundombinu ili kuona uwezekano wa kutembelea barabara sisi pamoja na Miundombinu au Wizara ya Miundombinu peke yao.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza suala la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri nina swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa swali la msingi linasema ni barabara kutoka Mbande-Mpwapwa na kwa kuwa barabara hii pamoja na kwamba inapitika lakini inahitaji matengenezo makubwa. Sasa je, Mheshimiwa Naibu Waziri atakubaliana nami kwamba TAMISEMI wakishirikiana na yaani Mkoa wahakikishe kwamba wanatenga fedha za kutosha kwa ajili ya kutengeneza barabara hii ya Mbande-Mpwapwa ambaye inaunganisha Makao Makuu pamoja na kujenga Daraja la Hazina?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua kabisa umuhimu wa barabara hii. Ndiyo maana sasa hivi tunashirikiana na wenzetu wa Miundombinu kuhakikisha kwamba barabara hii aidha ipandishwe hadhi au ibaki kwenye Halmashauri.

Lakini ni matumaini yangu kwamba sisi pamoja na Miundombinu kwa kushirikiana tuhakikishe kwamba barabara hii inapandishwa hadhi hadi kuchukuliwa na Mkoa ili ihudumiwe na Mkoa. Niwatoe tu wasiwasi Waheshimiwa Wabunge kwamba zoezi hili linaendelea vizuri sana sisi pamoja na Wizara ya Miundombinu kwa pamoja

tunashirikiana katika kutengeneza barabara hizi na katika kuangalia barabara zile ambazo Halmashauri hazina uwezo wa kuzitengeneza.

143

**Kujenga Hospitali ya Wilaya ya Ngara**

**MHE. PROF. FEETHAM F. BANYIKWA** aliuliza:-

Kwa kuwa, Wilaya ya Ngara haina Hospitali ya Serikali kwa ajili ya kutoa huduma ya tiba kwa wananchi:-

Je, Serikali itajenga lini Hospitali kubwa ya Wilaya ili wananchi waweze kupata huduma hiyo muhimu?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Profesa Feetham Filipo Banyikwa, Mbunge wa Ngara, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, azma ya Serikali ni kuhakikisha kuwa huduma za Afya zinazotolewa kwa wananchi zinaboreshwa na kufikia katika viwango vinavyoridhisha. Kwa Halmashauri ambazo hazina Hospitali za Wilaya huwa zinapata huduma ya Hospitali katika Hospitali Teule *(DDH)*. Wananchi wa Wilaya ya Ngara wanapata huduma hiyo kutoka katika Hospitali ya Murugwanza ambayo inamilikiwa na Kanisa la Anglican. Hivyo Wananchi wa Ngara wanapata huduma zote zinazostahili kutolewa na Hospitali ya Wilaya kutoka katika Hospitali hiyo.

Kwa kuwa ujenzi wa Hospitali mpya ya Wilaya unahitaji fedha nyingi na kwa kuzingatia azma hii, Halmashauri ya Wilaya ya Ngara imepanua Kituo cha Afya cha Nyamiaga kilichoko Ngara Mjini ili kiweze kutoa huduma stahili kwa wakazi wa Mji wa Ngara.

Mheshimiwa Spika, upanuzi huo unafanyika kwa kuongeza wodi ya watoto, wodi ya wazazi, wodi moja ya wanaume na wodi moja ya wanawake kwa ajili ya kulaza wagonjwa wa upasuaji, wodi ya wagonjwa wa kawaida, chumba cha upasuaji, jengo kwa ajili ya wagonjwa wa nje *(OPD)*, jengo la ushauri nasaha na upimaji wa virusi vya UKIMWI, chumba cha mionzi, wodi ya magonjwa ya kuambukiza na chumba cha maiti. Majengo mengine ambayo yamekamilika ni jengo la Afya ya kinywa (*Dental Building*), jengo la jiko na nyumba za watumishi watatu (3).

Kituo hiki kwa sasa kinatoa huduma muhimu zikiwemo huduma za mama na mtoto, upasuaji, kuongeza damu, kuhudumia wagonjwa wa nje na wa ndani, huduma za vipimo vya kimaabara pamoja na ushauri na upimaji wa virusi vya UKIMWI.

Mheshimiwa Spika, lengo la Serikali ni kukipandisha hadhi kituo hiki kuwa Hospitali ya Wilaya. Halmashauri ya Wilaya ya Ngara imekwishawasilisha maombi ya kupandisha hadhi kituo hiki katika Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii. Mnamo mwezi Oktoba mwaka 2007, Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, ilishauri kuwa, upanuzi uendelee hadi hapo itakapotuma wataalamu wake.

Na. 144

**Mpaka Kati ya Tanzania na Msumbiji Kupitia Mto Ruvuma**

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA** aliuliza:-

Kwa kuwa, katika Hotuba ya Bajeti ya Mwaka 2007/2008, Serikali ilithibitisha Bungeni kuwa, pamoja na kuzingatia mpaka wa Tanzania na Msumbiji kupitia Bahari ya Hindi, pia itazingatia kutambua mpaka wa nchi hizo mbili kupitia Mto Ruvuma:-

(a) Je, ni shilingi ngapi zimetengwa kwa ajili ya shughuli hiyo?

(b) Je, shughuli hiyo ya utambuzi wa mpaka kupitia Mto Ruvuma itaanza lini?

(c) Je, katika mradi huo, vijiji vya mpakani katika Mto Ruvuma vilivyopo katika Kata za Muhukuru na Ndongosi, Jimbo la Peramiho vitashirikishwa?

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi napenda kutoa maelezo mafupi na kisha kujibu swali la Mheshimiwa Jenista Joackim Mhagama, Mbunge wa Peramiho, lenye sehemu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba katika mwaka huu wa fedha 2007/2008, Wizara yangu imepanga kufanya kazi ya kutambua mipaka yetu na nchi jirani ikiwemo Msumbiji. Katika mwaka wa fedha 2006/2007, Wizara yangu ilifanya ukaguzi wa mpaka kati ya Tanzania na Msumbiji eneo la nchi kavu kati ya Ziwa Nyasa na Mto Ruvuma.

Baada ya ukaguzi, Mpango wa Kazi (*Action Plan)* ulitayarishwa kwa pamoja na wataalam wa nchi zote mbili.

(a) Mheshimiwa Spika, mpaka umekuwepo tangu awali na hauna utata. Kinachofanyika ni kukagua na kurudisha zile *beacons* zilizoondolewa au kuharibika baada ya kukaa kwa muda mrefu. Aidha, zitawekwa *beacons* mahali ambapo alama hizo zipo mbali sana kutoka moja hadi nyingine ili mpaka uonekane bayana. Kazi hii itagharimu jumla ya shs. 27,000,000/= katika mwaka wa fedha 2007/2008.

(b) Mheshimiwa Spika, shughuli ya utambuzi wa mpaka imekwishaanza tangu mwaka 1988 ambapo sehemu ya mpaka katika Bahari ya Hindi yalipo maji ya kugawana kati ya Tanzania na Msumbiji peke yake imeshashughulikiwa na kufikiwa makubaliano na hatimaye Protokali kutiwa sahihi.

Kutokea alama ya mwisho ya makubaliano hayo, unatakiwa uwepo mstari hadi alama ya makubaliano ya nchi tatu; Tanzania, Msumbiji na Comoro. Alama hii ya utatu bado kujadiliwa baina ya nchi tatu kuwa Comoro haijawa tayari kufanya majadiliano.

Ukaguzi wa pamoja katika sehemu ya nchi kavu ya mpaka kutokea makutano ya Mto Ruvuma na Mto Misinje hadi Ziwa Nyasa umefanyika mwezi Mei 2007 na kuainisha mahitaji ya kupima, kusimika mawe ya mipaka na kufyeka ukanda (Mkuza) wenye upana wa mita 20.

Sehemu ya mpaka ambayo inafuata Mto Ruuma kutoka uingiapo katika Bahari ya Hindi hadi Makutano ya Mto Ruvuma na Mto Misinje haina utata wowote. Isipokuwa nchi zote kupitia wataalam wake zimekubaliana kufanya ukaguzi wa pamoja wa Mto ili kuona iwapo umebadili mapitio yake.

Aidha, sehemu ambapo Mto ni mpana sana kuna sehemu za ardhi kavu kama visiwa ambavyo vinatakiwa kukaguliwa na hatimaye kukubaliana jinsi ya kuvigawa kati ya Tanzania na Msumbiji. Kazi hii ilipangwa kufanyika mwezi Septemba 2007 lakini haikutekelezwa kutokana na ufinyu wa Bajeti. Ni matarajio ya Wizara yangu kuwa kazi hii itatekelezwa katika mwaka wa fedha 2008/2009 kulingana na upatikanaji wa fedha.

(c) Mheshimiwa Spika, Wizara yangu inashirikisha na umma wakati wote inapotekeleza kazi zake za ndani (*Field Work*). Ushirikishwaji huanzia ngazi za Mkoa, Wilaya, Kata hadi Vijiji vinavyoangukia mpakani na nchi zote jirani. Napenda kumhakikishia Mheshimiwa Jenista Joachim Mhagama, Mbunge wa Peramiho kwamba wakati Wizara yangu itakapotambua mpaka katika eneo la Mto Ruvuma, vijiji vya Kata za Mhukuru na Ndongosi vitashirikishwa kikamilifu.

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri na hasa kwa kulithibitishia Bunge kwamba mpaka wa Tanzania na Msumbiji kupitia maeneo aliyoyataja hauna matatizo. Lakini kwa kuwa moja ya jukumu la Wizara hiyo ya Ardhi ni kutambua mipaka lakini vile vile kuhakikisha kwamba maeneo yetu yaliyopo mipakani yanapimwa na kwa maeneo yenye kutumika kama raslimali nzuri kwa Taifa letu la Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Waziri anatambua sasa kwamba eneo la mpakani katika kijiji cha Mhukuru Wizara nyingine mbili ya Miundombinu na Wizara ya Usalama wa Raia imeshafanya kazi nzuri ya kuendeleza mpaka huo isipokuwa upimaji wa viwanja ambavyo sasa unahitaji msaada mkubwa kutoka Wizarani kwake, je Wizara itatekeleza lini mpango huo ili kushirikiana na Halmashauri katika kuendeleza eneo hilo la mpaka?

Mheshimiwa Spika, lakini vile vile kwa kuwa Wizara katika bajeti ya mwaka huu ilisema wazi kabisa utambuzi wa eneo la mpaka hautaishia tu katika eneo alilolitaja Mheshimiwa Naibu Waziri kwa maana ya Mto Ruvuma eneo linaloingilia katika Bahari ya Hindi na amekubali kushirikisha vijiji hivyo nilivyovitaja vya mpakani katika utambuzi wa mpaka huo. Je, ushirikishwaji huo utaishia katika *field work* tu ama pia vile vile kupima maeneo ya ardhi yaliyomo katika vijiji hivyo?

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, la kwanza Wizara yangu inatambua umuhimu wa kupima vijiji, kupima ardhi na maeneo yote yaliyoko mipakani ili kuondoa utata. Naomba kutamka kwamba tutashirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Peramiho ili kuhakikisha kwamba tunapima vijiji vyote vilivyoko katika eneo hilo.

Kuhusiana na viwanja ningependa niwashauri kwamba wawasiliane na Wizara ili tuone kama tunaweza tukawapatia fedha kutoka katika Mfuko wa Upimaji Viwanja kama mkopo ili waweze kupima maeneo hayo. Lakini kwa kuwa hili suala ni nyeti Wizara yangu itakuwa tayari kabisa kushirikiana na Halmashauri katika unyeti huo.

Mheshimiwa Spika, sio eneo moja tu ambalo linahusika katika mpaka katika maeneo haya. Ametambua kwamba Wizara ina umuhimu wa kupima kuanzia Bahari ya Hindi mpaka itakapofikia nchi kavu ambalo tumelitambua inahusisha Mkoa wa Mtwara, linahusisha Wilaya na Jimbo la Tunduru, Namtumbo na hatimaye Peramiho.

Mheshimiwa Spika, ningeomba ushirikiano mkubwa wa Wizara yangu pamoja na maeneo hayo niliyoyataja ili tuweze kuhakikisha kwamba maeneo haya ya mipakani yamepimwa kama tulivyofanya katika maeneo ya mipaka na nchi zingine.

Na. 145

**Deni la Wakulima wa Pamba Dhidi ya KACU**

**MHE. JAMES D. LEMBELI** aliuliza:-

Kwa kuwa, mapema mwaka 2006 kupitia Bunge letu, Serikali iliwaahidi wakulima wa Wilaya za Kahama, Bukombe na Uyui kuwa, itawalipa fedha zao wanazokidai Chama Kikuu cha Ushirika cha Kahama *(KACU)* deni linalofikia shilingi milioni mia moja thelathini (130m./-) linalotokana na Pamba waliyouza kwa chama hicho msimu wa mwaka 2004/2005. *(Makofi)*

Kwa kuwa, deni hilo limekuwa la muda mrefu hivyo kusababisha usumbufu na manung'uniko makubwa miongoni mwa wakulima wa zao hilo. Je, Serikali inatoa kauli gani kuhusu hatma ya deni hilo na suala hilo litakwisha lini?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA (MHE. DR. DAVID M. DAVID)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa James D. Lembeli, Mbunge wa Kahama kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, wakulima wa Wilaya ya Kahama, Bukombe na Uyui wanakidai Chama chao Kikuu cha Ushirika cha Kahama *(KACU)* deni linalofikia kiasi cha shilingi milioni 130.0. Deni hili lililotokana na mauzo ya pamba yao katika msimu wa 2004/2005.

Aidha, deni la *KACU* ni miongoni mwa madeni ambayo Serikali imeyahakiki kwa lengo la kuandaa utaratibu wa kuyalipa. Mwaka 2006 Serikali kupitia Bunge lako Tukufu iliahidi kuyachukua na kuyalipa madeni hayo ili kuwaondolea kero wakulima. Utaratibu uliowekwa na Serikali ni kulipa madeni hayo kwa awamu kulingana na uwezo wa kifedha ambapo utekelezaji wake umepangwa uanze kufanyika kuanzia mwaka wa fedha 2007/2008. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika awamu ya kwanza ya utekelezaji huo, Serikali imeanza mchakato wa ulipaji wa madeni hayo ya Vyama vya Ushirika dhidi ya Mabenki kiasi cha shilingi bilioni 3.3 ili kuvifungulia mwanya wa kukopesheka na hivyo kuendelea kufanya biashara kama inavyotarajiwa. Serikali itaendelea kuangalia uwezekano wa kulipa haraka madeni ya Vyama vya Ushirika kikiwemo cha *KACU* kwa wakulima kama ilivyoahidi kadri uwezo wa kifedha utakavyoruhusu.

**MHE. JAMES D. LEMBELI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Kwa vile Serikali ilianza kwa kuwaahidi kuwalipa wakulima wa zao la Pamba wa Kahama, Bukombe na Uyui mwaka uliopita. Majibu ya Wizara ni kwamba watawalipa pindi pesa zitakapopatikana. Tatizo hapa ni neno "Pindi Pesa Zitakapopatikana". Nina maswali mawili.

La kwanza, je Serikali inaweza kueleza ni lini pesa hii itapatikana mwaka huu, mwaka ujao, mwaka kesho kutwa au mwaka 2010 ili wananchi hawa wasiendelee kuishi kwa matumaini.

Pili, je Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika kwa huruma ile ile aliyoionyesha kwa wakulima wa zao la korosho kule Mtwara kwamba atajiuzulu endapo wakulima hao hawatalipwa haki yao. Je, huruma ataielekeza Kahama, Bukombe na Uyui kwamba atajiuzulu endapo wakulima hawa hawatalipwa fedha zao. (*Makofi)*

**SPIKA:** Kwa lile swali la pili, nadhani kwa kuwa linamhusu Waziri mwenyewe mahsusi nadhani itabidi lisubiri siku nyingine, Naibu wake atajibu lile la kwanza.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA (MHE. DR. DAVID M. DAVID):** Mheshimiwa Spika, Azimio la Bunge Na. 4 la Mwaka 2006 lilikubali kufuta madeni ya Vyama vya Ushirika, lakini pia kulipa madeni ya Vyama vya Ushirika. Zoezi hili linakwenda kwa awamu kutokana na upatikanaji wa fedha. Kwa mfano: Katika Chama hiki cha *KACU*, tayari Serikali ilishasamehe shilingi milioni 22, yaani kwa maana ya Serikali na Taasisi zake. Benki ya *CRDB* inawadai shilingi milioni 353 ambazo zimeishatengwa kwenye Bajeti ya mwaka huu. Kwa hiyo, kama nilivyosema kwamba tunafanya haya mambo kwa awamu, katika Bajeti ya mwaka 2007/2008, Chama hiki kitalipiwa milioni 353. Wakulima wanadai milioni 130 ambazo waliuza Pamba yao na hii ninasema kwamba tutakapopata pesa hata kama tutapata fedha mwaka huu, tuko kwenye mchakato wa kutafuta pesa, tukipata pesa mwaka huu, deni hilo litalipwa. *NSSF* wanadai shilingi milioni 9. Kwa hiyo, tutakapopata fedha, tutalipa. Si rahisi kusema kwamba tutapata mwaka kesho au mwaka huu. Lakini, ninachosema ni kwamba tuko kwenye mchakato wa kupata fedha, tukipata mwaka huu, madeni hayo yatalipwa ili kuimarisha Vyama hivi viweze kujiendesha kibiashara.

**SPIKA:** Kabla hatujaendelea na Wizara inayofuata, natumaini Mheshimiwa Naibu Waziri utalifikisha ombi la Mheshimiwa Lembeli kwenye hilo swali la pili ili Waziri ajue kwamba jinsi alivyoahidi kwenye Korosho, pia ni vizuri ahadi hiyo hiyo kwa usawa ihusu pia zao la Pamba na pengine ihusu pia zao la Tumbaku. *(Makofi/Kicheko)*

Na. 146

**Kuweka Mawasiliano Sehemu za Mapori Makubwa**

**MHE. SAVELINA S. MWIJAGE** aliuliza:-

Kwa kuwa matatizo ya utekaji magari ya abiria na mizigo yanajitokeza katika mapori makubwa yaliyopo katika Mkoa wa Kagera hasa pori la Biharamulo Mpaka Muleba na pori la Kimisi – Karagwe na yanachangiwa sana na ukosefu wa mawasiliano ya kutosha:-

Je, Serikali haioni kuwa sasa ni wakati muafaka wa kushawishi wawekezaji wa mawasiliano ya simu za mkononi kujenga minara ya simu ya kutosha katika maeneo hayo ili kusaidia kuzuia matatizo ya ujambazi na uporaji?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MAUA A. DAFTARI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Savelina S. Mwijage, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba tatizo la utekaji nyara wa magari ya abiria na mizigo lipo hasa katika sehemu za mapori makubwa nchini yakiwemo ya Mkoa wa Kagera na kwamba kwa kiasi kikubwa yanachangiwa na kutokuwepo kwa mawasiliano ya simu. Hali hii imeendelea kuwa kero kubwa kwa jamii siku hadi siku na kuathiri shughuli za uzalishaji, biashara, kilimo na hata kuzorotesha huduma za utalii. Aidha, Serikali inalitambua tatizo hilo na inalifanyia kazi kwa kushirikisha wadau wote husika. Kwa upande wa sekta ya mawasiliano, juhudi za kuboresha huduma za mawasiliano katika maeneo yenye mapori makubwa zinafanyika kuyashawishi makampuni husika kupanga mipango yao inayolenga kupeleka huduma huko kama sehemu ya kupambana na utekaji wa magari ya abiria na mizigo.

Mheshimiwa Spika, kampuni ya *Vodacom* tayari imeanza mchakato wa kiufundi ili kubaini sehemu muafaka kwa ajili ya kujenga mtambo wa mawasiliano. Kwa kuanzia, tathmini imefanyika maeneo ya Benako, Bwanga, Lusahunga na Nyakanazi. Vile vile tathmini za awali zimeanza katika maeneo ya Kashahunga, Nyakahura na itaendelea katika maeneo mengine ili kuweza kutoa huduma kikamilifu katika maeneo yote yenye mapori makubwa. Mheshimiwa Spika, kampuni ya *Celtel* bado inafanya tafiti za masoko katika vijiji vilivyopo jirani na mapori ili kupeleka huduma zao huko na kuondoa matatizo ya mawasiliano katika mapori hayo. Hata hivyo, *Celtel* tayari wanao mpango wa kujenga minara kati ya Biharamulo na Muleba katika eneo la Luhuma ifikapo Juni mwakani na Mkombozi – Kashemwe ifikapo Desema, 2008. Katika Msitu wa Kimisi na Karagwe wana mpango wa kujenga mnara katika eneo la Nyamwara ifikapo mwezi Aprili mwakani. Kwa hivi sasa, Serikali inaendelea kuwasiliana na makampuni ya *TTCL*, Tigo na *Zantel* ambayo bado hayajaweka mipango ya kupeleka huduma mawasiliano katika mapori makubwa kuweza kufanya hivyo ili kulipatia ufumbuzi tatizo hilo kubwa la utekaji wa magari ya abiria na mizigo.Katika kutafuta ufumbuzi wa suala hili, jitihada za pamoja kati ya Wizara yangu na Wizara ya Usalama wa Raia na ile ya Serikali za Mitaa itahitajika. Wananchi nao wanayo nafasi ya kushiriki kikamilifu kusaidia katika utoaji wa taarifa.

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi ili niweze kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa, hali hiyo ya mapori makubwa pia iko kule Mbozi kati ya Kijiji cha Utambalila na Ntungwa na eneo hilo pia majambazi huteka sana na kwa sababu pia hakuna mawasiliano, inakuwa ni vigumu kwa wananchi wanaonusurika kuweza kuwasiliana na Polisi. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri ataliweka pia hilo kwenye mipango na kushawishi makampuni hayo pia yaweze kuweka mitambo ya mawasiliano katika maeneo hayo?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MAUA A. DAFTARI):** Mheshimiwa Spika, nakubaliana naye kwamba kule Mbozi katika sehemu ya Utambalila na Ntungwa kuna maeneo ambayo yana misitu mikubwa na utekaji nyara unakuwepo. Lakini, vile vile kule Loliondo ambako nimezungumza na Mheshimiwa Mbunge nako kuna matatizo ambayo yanafanana. Yote kwa pamoja tayari tumeishawasilisha kwa wawekezaji wa makampuni ya simu waone umuhimu wa kufanya shughuli hizo za mawasiliano kutokana na mipango yao watakapopanga, waweke katika shughuli hizo. Ahsante.

**MHE. FELIX N. KIJIKO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Pamoja na majibu mazuri aliyoyatoa Naibu Waziri, kijiografia Mkoa wa Kagera na Mkoa wa Kigoma iko sambamba na matokeo ama athari za ujambazi unaofanyika hapo unatokana na kuwapokea Wakimbizi na kuwaweka katika Mikoa hiyo kwa muda mrefu. Sasa Je, sina hakika kama Naibu Waziri ataona kama Mkoa wa Kigoma nao una matatizo kama Mkoa wa Kagera, ili mawasiliano yaweze kuwapo barabara nzima kwa sababu matukio ya ujambazi yanazidi kuongezeka?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MAUA A. DAFTARI):** Mheshimiwa Spika, napenda nikubaliane naye kwamba wingi wa Wakimbizi katika maeneo Mheshimiwa Mbunge anayozungumzia ndiyo yanayoleta mtafaruku katika maeneo hayo. Lakini, sina uhakika sana kwamba katika maeneo hayo anayozungumzia kuna mapori makubwa ambayo yatahitaji yashughulikiwe.

Lakini nakubaliana naye kwamba katika barabara hiyo aliyozungumzia kuna umuhimu wa kupeleka mawasiliano ya simu na naahidi kuyachukulia hatua inayofaa.

**MHE. DR. ALI TAARAB ALI:** Mheshimiwa Spika, ahsante! Kwa vile katika Jimbo langu la Konde kuna msitu mkubwa wa Ngezi na nyuma ya msitu huo kuna vijiji ambavyo havipati mawasiliano ya simu (Kwa kweli hakuna uporaji wowote, lakini kuna hoteli za kitalii). Je, Mheshimiwa Naibu Waziri ataniambia lini tutapata mawasiliano ya uhakika ya simu katika vijiji vya Kigomasha, Makangale, Mkiawang'ombe na Tondoni? *(Kicheko/Makofi)*

**SPIKA:** Sina shaka, Mheshimiwa Naibu Waziri unavijua sana vijiji hivyo. Kwa hiyo...! *(Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MAUA A. DAFTARI):** Mheshimiwa Spika, ni kweli navijua sana vijiji hivyo! Mimi mwenyewe binafsi tayari nimepitia msitu mzima ule wa Ngezi kuona ni namna gani tunaweza kupeleka mawasiliano ya simu kwa kupitia kati kati, lakini imekuwa ni vigumu kutokana na *thikness* na urefu wa miti iliyoko pale. Kwa hivyo, tumekubaliana na makampuni ya simu watafute teknolojia inayofaa hata kwa kuzunguka nyuma ya maeneo ambayo msitu wa Ngezi unapita. Kwa maana hiyo, tunategemea Kigomasha, Makangale na sehemu nyingine, mawasiliano yatafika.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa, maeneo ya hoteli za kitalii, mawasiliano ya *Zantel* yanapatikana. Lakini tatizo ni kupita kati kati ya Ngezi ambapo wameniahidi kwamba watashughulikia.

Na. 147

**Mashine ya Ukaguzi wa Abiria na Mizigo**

**MHE. FAIDA MOHAMED BAKAR** aliuliza:-

Kwa kuwa zipo mashine *(Scanners)* za ukaguzi wa mizigo na abiria kwenye sehemu za kusafiria kama vile Viwanja vya Ndege au Bandari; lakini Kiwanja cha Ndege cha Pemba hakina mashine za ina hiyo jambo ambalo ni hatari kwa usalama wa wasafiri na mizigo yao:-

(a) Je, ni kwa nini Kiwanja hicho hakina mashine za ina hiyo?

(b) Je, ni lini Kiwanja hicho kitawekewa mashine hizo?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MAUA A. DAFTARI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Faida Mohamed Bakar, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, uwekaji wa mashine za kukagulia mizigo kwenye Viwanja vya Ndege ni kazi ya Mwenye Kiwanja cha Ndege. Aidha, umiliki, usimamizi na uendeshaji wa viwanja vya Ndege siyo suala la Muungano. Kwa upande wa Tanzania Bara, Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania ndiyo iliyopewa jukumu la kusimamia na kuendesha Viwanja vyote vya Serikali. Kwa upande wa Tanzania Zanzibar, Serikali ya Mapinduzi Zanzibar chini ya Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi ndiyo inayomiliki na kusimamia Viwanja vya Ndege vya Zanzibar vikiwemo Unguja na Pemba. Hata hivyo, Viwanja vyote vya Ndege vya Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar vinadhibitiwa na Mamlaka ya Usalama na Usafiri wa Anga Tanzania *(Tanzania Civil Aviation Authority)* ambacho ni chombo cha Muungano kinachosimamia na kuhakikisha kuwepo

kwa usalama wa abiria na mizigo na pia kusimamia ufungaji wa mitambo ya ukaguzi *(Scanner)* na wakaguzi wenye *screeners.*

Mheshimiwa Spika, ukaguzi wa msingi unaosisitizwa na Shirika la Kimataifa linalosimamia Usafiri wa Anga Duniani *(ICAO)* ni wa kutumia mikono *(Manually Inspection)*. Utumiaji wamashine unapendekezwa pale ambapo abiria wanaopita katika Kiwanja husika ni wengi ili kuondoa msongamano usio wa lazima kwenye Kiwanja, lakini kuendelea kudhibiti usalama.

Mheshimiwa Spika, kiwango cha abiria wanaotumia kiwanja cha Pemba ni kidogo na kwa mujibu wa kanuni za *ICAO*, Kiwanja hicho hakilazimiki sana kwa sasa kufungwa mashine za kukagua abiria, bali ukaguzi unafanywa kwa mikono na unatosheleza. Cha msingi ni wakaguzi kuwa makini ili kuhakikisha kwamba wasafiri waovu hawapati mwanya wa kutishia usalama wa ndege, abiria na mizigo yao au Kiwanja chenyewe.

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kupitia Mamlaka ya Usalama wa Usafiri wa Anga Tanzania itaendelea kuwasiliana kwa karibu zaidi na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ili kuhakikisha kwamba Kiwanja cha Pemba kinaendelea kuwa salama kwa wakati wote wanapokitumia. Mashine za ukaguzi zitafungwa pale ambapo ongezeko la abiria litaonyesha kwamba ukaguzi wa kutumia mikono unashindwa kuhakikisha kwamba Kiwanja cha Ndege cha Pemba kinakuwa salama. Kama hali hiyo itafikiwa, tutalazimika kutumia mashine ndogo za *Walk through Metal Detector* kabla ya kufunga mashine kubwa.

**MHE. FAIDA MOHAMED BAKAR:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Naibu waziri yenye ufafanuzi mzuri, lakini nina swali moja la nyongeza. Kwa kuwa mbali na kutokuwepo *scanner machine* katika *Airport* yetu ya Pemba, lakini pia gari la Zimamoto ni bovu. Tukiulizia, tunaambiwa mashine imechukuliwa imeenda kufanyiwa marekebisho sijui Unguja, kitu kama hicho. Je, Serikali ya Muungano, kwa sababu hili suala la Zimamoto na Kiwanja cha Ndege ni la Mawasiliano ya Zanzibar, lakini ajali ikitokea, ni la Watanzania wote; Je, Serikali itakubaliana nami kwamba sasa ni wakati mwafaka wa kuishauri Serikali ama Wizara ya Mawasiliano Zanzibar kulifanyia matengenezo haraka gari lile la Zimamoto ili kuepusha ajali?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MAUA A. DAFTARI):** Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema katika maelezo yangu ya awali, haya masuala ya Zimamoto ni masuala ambayo si ya Muungano, lakini ni masuala ambayo ajali ikitokezea kama anavyosema Mheshimiwa Faida, inatugusa sote. Kwa maana hiyo, mimi niko tayari kuwasiliana na wenzangu wanaohusika na masuala haya ili waone umuhimu wa kulitengeneza lile gari la Zimamoto, au kama halitengenezeki, basi linunuliwe lingine kwa sababu bei yake ni shilingi milioni 600 tu. *(Makofi)*

Na. 148

**Tatizo la Ugonjwa wa Malaria**

**MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA** aliuliza:-

Kwa kuwa ugonjwa wa malaria bado unaongoza kwa kusababisha vifo vingi nchini na kwa kuwa wananchi wa Jambiani, Zanzibar wamefanikiwa kutokomeza ugonjwa huo kwa asilimia kubwa sana kwa kufanya usafi wa maeneo yao *(Environmental Sanitation)* na utumiaji wa vyandarua:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuiga mfano wa Jambiani kwa nchi nzima?

(b) Je, Serikali ina mpango wowote wa kutoa vyandarua vya bei nafuu sehemu zote zilizoathirika na ugonjwa huo?

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla sijajibu swali namba 148, naomba nitoe salaam za rambi rambi kwa Mheshimiwa Prof. Jumanne Maghembe ambaye amefiwa na dada yake wiki iliyopita. Salaam hizi nazitoa kwa niaba ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, marehemu alikuwa mfanyakazi wa Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii. Baada ya salaam hizo, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Victor Kilasile Mwambalaswa, Mbunge wa Lupa, lenye vingele (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mafanikio yaliyopatikana huko Zanzibar yamekuwa ni changamoto kubwa sana kwetu. Afua zilizotumika siyo usafi wa mazingira tu, bali ni pamoja na matumizi ya vyandarua vilivyotiwa viuatilifu vinavyoua mbu na njia nyingine ni unyunyiziaji wa ukoko wa viuatilifu katika kuta ndani ya nyumba. Mpango wa matumizi ya vyandarua vyenye viuatilifu unatekelezwa Tanzania Bara vile vile kwa kutoa punguzo la vyandarua hivyo kwa makundi yanayoathirika zaidi na malaria yaani watoto na wanawake wajawazito.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kupitia Mpango wa Taifa wa Kudhibiti Malaria, inao Mwongozo wa Kudhibiti Mbu Waenezao Malaria *(Integrated Malaria Vector Control)* ambao tayari inautekeleza lakini utekelezaji wake utaimarishwa zaidi kuanzia mapema mwaka 2008. Njia mbalimbali zitatumika kudhibiti mbu waenezao malaria ikiwa ni pamoja na kunyunyiza dawa ya kuua mbu katika kuta ndani ya nyumba *(Indoor Residual Spraying)*, kuua viluwiluwi vya mbu, kurekebisha mazingira ili kuzuia mazalia ya mbu, matumizi ya vyandarua vyenye viuatilifu *(ITN)* na matumizi sahihi ya dawa mseto.

Mheshimiwa Spika, kwa kutumia uzoefu uliopatikana Visiwani Zanzibar na mahali penginepo duniani, unyunyiziaji wa dawa ya kuua mbu majumbani umeshaanza katika Wilaya ya Muleba. Zoezi hili litatumika kama mfano *(Pilot Study)* kwa Wilaya nyingine nchini.

Serikali pia imeandaa mpango wa kuhakikisha kuwa vyandarua vya bei nafuu vinapatikana sehemu zote nchini. Katika mpango huo, kampeni maalum inayoitwa *Under Five Catch Up Campaign* imeandaliwa kwa mwaka 2008. Katika kampeni hiyo vyandarua vya kudumu *(Long Lasting Insecticide Treated Nets)*, vitatolewa bila malipo kwa watoto wote wenye umri kati ya mwaka mmoja hadi mitano. Kadhalika kwa kupitia Mpango wa Taifa wa Hati Punguzo ambao unaendeshwa nchi nzima tangu mwaka 2004, Serikali pia inaendelea kuhakikisha kuwa akinamama wajawazito na watoto wenye umri chini ya mwaka mmoja wanapata vyandarua kwa bei nafuu. Mchango wa mama mjamzito sasa umepungua kutoka Sh. 2,750/= alizokuwa analipa awali hadi Sh. 500/= kwa chandarua chenye viuatilifu vinayodumu muda mrefu.

**MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Napenda kumshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake ambayo ni fasaha na nimeelewa vizuri. Pamoja na majibu hayo, nina maswali mawili ya nyongeza; Ugonjwa wa malaria unaua kuliko UKIMWI na UKIMWI umetangazwa kwamba ni janga na una mikakati chungu mzima ya kuutokomeza. Je, ni kitu gani ambacho kinaufanya ugonjwa wa malaria ambao unaua kuliko UKIMWI nao usitangazwe kama janga?

Mheshimiwa Spika, swali la pili: katika miaka ya 1960, Halmashauri zilikuwa na vikosi maalum ambavyo vilikuwa vina magari, vinasaidiwa na *Development Partners* katika kunyunyizia maeneo ambayo mbu wanazalia na kutokomeza ugonjwa huo. Je, ni sababu gani ambayo inafanya mpango huo usifufuliwe wa Halmashauri kuwa na vikosi vya kunyunyizia dawa?

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, naomba nikubaliane na Mheshimiwa Mwambalaswa kwamba ugonjwa wa malaria unachukua maisha ya watu wengi zaidi kuliko hata UKIMWI. Mikakati ya kupambana nao ipo, lakini kama inafikiriwa kwamba kuutangaza kwamba ni janga basi mikakati itazidi, basi hilo tutaliangalia. Swali la pili kuhusu kunyunyiza; Katika majibu yangu ya swali la msingi nimeeleza afua mbali mbali zinazotumika na Mheshimiwa Mwambalaswa anazungumzia kuhusu kunyunyiza dawa katika maeneo mbali mbali. Hiyo imeonekena kwamba ina madhara na mazingira kwa sababu zile dawa hazichagui mimea wala samaki, wala dagaa, ndiyo maana tumeona tujikite katika afua zingine. Afua kama ya kutumia vyandarau vyenye viuatilifu kwenye maeneo ambayo inafanya kazi vizuri, imepunguza malaria kwa aslimia 60. Sasa ukichanganya na nyingine kama kunyunyizia ndani ya kuta za nyumba, tunafikiri kwamba ukichanganya hizo pamoja na matumizi mengine ya dawa, tunaweza tukafika tunapotaka kufika.

Na. 149

**Wimbi la Watumishi wa Afya Kuacha Kazi**

**MHE. HERBERT J. MNTANGI** aliuliza:-

Kwa kuwa kumekuwa na wimbi kubwa la watumishi wa afya kuacha kazi hasa Madaktari, Madaktari Wasaidizi, Manesi na hata Wakunga kutoka Hospitali, Vituo vya Afya, Zahanati za Taasisi za Dini kama vile Hospitali Teule Muheza na kadhalika, hivyo kuathiri huduma za afya kwa wagonjwa hata kusababisha vifo na kwa kuwa Hospitali Teule ya Muheza ambayo inaendeshwa kwa ubia kati ya Serikali na Kanisa la *Anglican* Tanzania imeathiriwa sana na tatizo hilo:-

(a) Je, Serikali inafahamu ni Madaktari, Madaktari Wasaidizi, Manesi na watendaji wengine wangapi waliohama na kuacha kazi kwa miaka minne iliyopita kutoka Hospitali Teule ya Muheza?

(b) Je, Serikali inafahamu kwamba, baadhi ya sababu za hali ya kuacha kazi kwa wafanyakazi hao ni kutofautiana kwa mishahara, marupurupu na pensheni kwa watumishi walioajiriwa na Kanisa na wale walioajiriwa na Serikali?

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Herbert Mntangi, Mbunge wa Muheza kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa kumekuwa na wimbi kubwa la watumishi wa Afya hususan Madaktari, Madaktari Wasaidizi, Maafisa Wauguzi na Wauguzi kuhama kutoka katika hospitali, Vituo vya Afya, Zahanati za binafsi na Mashirika ya Dini na kwenda Serikalini na baadhi yao hasa Madaktari na Wauguzi kwenda nje ya nchi. Aidha, ni kweli kwamba katika hali kama hii huduma zinazotolewa na hospitali hizo za binafsi na zile za Mashirika ya Dini ikiwemo Hospitali Teule Muheza zinaathirika.Kwa mujibu wa taarifa tulizonazo, jumla ya watumishi 74 wakiwemo Madaktari, Madaktari Wasaidizi, Wauguzi na watendaji wengine walihama na kuacha kazi katika kipindi cha miaka minne iliyopita.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali inafahamu kwamba baadhi ya sababu za kuhama au kuacha kazi kwa watumishi wa afya sehemu mbalimbali ikiwemo Hospitali Teule ya Muheza zinazohusiana na maslahi ya kiutumishi. Mheshimiwa Spika, katika kukabiliana na hali hiyo Wizara yangu imekuwa ikitoa ushauri kwa watumishi wanaopewa ajira ya Serikali kuendelea kutoa huduma kwenye vituo vyao vya awali hususan vituo vinavyotoa huduma za afya kwa ubia na Serikali kama Hospitali Teule ya Muheza. Hata hivyo, ushauri ambao Serikali imekuwa ikiutoa ni kwa uongozi wa hospitali binafsi kama ile ya Muheza kufanya mawasiliano na Halmashauri za Wilaya ya Muheza ili kubaini Hospitali ya Muheza ina nafasi ngapi zilizoidhinishwa katika ikama, halafu Halmashauri iombe nafasi hizo kujazwa. Kimsingi, watumishi wengi katika Hospitali ya Muheza wanalipwa na Serikali. Hata hivyo, tungependa kuona kuwa watumishi wanaofanya kazi Hospitali Teule ya Muheza wanaendelea kufanya kazi hapo hapo Muheza hata kama watakuwa wameingia katika ajira na Serikali. Kwa kutambua kwamba watumishi ni rasilimali muhimu kuliko zote katika uendeshaji wa hospitali, tunaendelea kusisitizia waajiri wa

hospitali teule wajitahidi kutumia miongozo ya mishahara ya Serikali ikiwa ni pamoja na kuboresha maslahi ya watumishi.

**MHE. HERBERT J. MNTANGI:** Mheshimiwa Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa majibu mazuri aliyoyatoa. Hata hivyo, naomba kuuliza swali moja dogo la nyongeza. Kwa kuwa Mheshimiwa Waziri ametufahamisha kwamba na sisi tunafahamu hivyo kwamba mishahara ya watumishi wale madaktari na manesi inatoka Serikalini; Je, ni kwa nini basi wafanyakazi hao wasiingizwe katika mfumo wa ajira ya Serikali ili vile vile waweze kuingizwa katika mfamo wa malipo ya pensheni ambao ni kikwazo kikubwa kinachoweka tofauti kati ya mishara yao na mishahara ya wale walioajiriwa na taasisi?

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema wakati najibu swali la msingi, Hospitali Teule ya Muheza kama ilivyo katika Hospitali Teule nyingi, watumishi wengi ni waajiriwa wa Serikali kwa sababu mishahara inalipwa na Serikali. Kwa hiyo, wako katika mfamo wa Serikali kwa maana ya kwamba mishahara inapopanda na wenyewe inapanda na hata pensheni kwa sababu ni waajiriwa wa Serikali, wako katika mfumo kama wafanyakazi wengine.

**MHE. DR. WILBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu ya Mheshimiwa Wazirikama ilivyo kwa Hospitali Teule ya Muheza, mazingira hayo hayo yako kwa Hospitali Teule ya Karatu inayoendeshwa na KKKT, *Northern Diocese* na matatizo hayo hayo yako pia kwenye hospitali nyingi zinazoendeshwa na madhehebu yote ye Dini. Je, Waziri atakubali sasa kwamba ili kuondoa mvutano kati ya watumishi wanaokuwa Serikalini na wale wanaokuwa kwenye Taasisi za Madhehebu ya Dini ambao nao pia wanatumikia na kuwahudumia Watanzania hawa hawa, badala ya Madhehebu ya Dini kupewa kazi ya kuwatafuta hao wahudumu na kuwafanya walinganishwe maslahi, Serikali ndiyo ifanye kazi hiyo na kuwapangia kwenye Hospitali hizi ili Watanzania wapate huduma bila ya kuwa na mashaka na utata wakati wote ambapo watumishi hawa wanahamia Serikalini?

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, naomba nimshukuru Mheshimiwa Slaa kwa ushauri aliotupa na ni ushauri ambao nakiri tunaufanyia kazi. Baada ya kuongeza mishahara ya watumishi wa Sekta ya Afya mwaka jana, hili wimbi lililozungumziwa na Mheshimiwa Mntangi ndiyo kwanza limeanza kujitokeza kwa wingi. Na sisi kama Serikali tumekuwa tukijiuliza kwamba hizi Hospitali Teule na Hospitali nyingine za Misheni nyingi zipo kwa ajili ya kuhudumia wananchi na si biashara. Kwa hiyo, tumeona ipo haja ya kuangalia mfumo mzima wa jinsi tunaweza tukawasiliana na tuwe na utaratibu mzima ili kuhakikisha kwamba hizo Hospitali zinaendelea kufanya kazi, vinginevyo tukiacha hali kama ilivyo, nyingi zitafungwa hasa ukizingatia kwamba wahisani wengi waliokuwa wanazisaidia huko nyuma wameondoka.

Na. 150

**Mavazi ya Jeshi la Polisi**

**MHE. MOHAMMED AMOUR CHOMBOH** aliuliza:-

Kwa kuwa, katika kufanya kazi zake vizuri Jeshi la polisi linahitaji zana za kutendea kazi zenye kukidhi haja ya wakati tulio nao sasa; na kwa kuwa miongoni mwa zana hizo ni pamoja na mavazi au sare za Polisi:-

Je! Serikali haioni sasa kuna haja ya kubadilisha sare za Polisi na kuwapa zenye mvuto wa kiaskari kuliko zilivyo sasa ambazo ni kama nguo za raia wa kawaida?

**NAIBU WAZIRI WA USALAMA WA RAIA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa ruhusa yako, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mohammed Amour Chomboh, Mbunge wa Magomeni, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 173 cha kanuni za kudumu za Jeshi la Polisi *(PGO)* kinaainisha kanuni za sare *(dress regulations)* za maofisa na askari wa Jeshi la Polisi katika makundi mbalimbali kulingana na majukumu yao kama vile wakati wa sherehe za kitaifa, gwaride, doria, *operation*, na kadhalika. Kwa mfano askari wa kikosi cha usalama wa barabarani wanavaa sare nyeupe ili iwe rahisi kuonekana wanapokuwa kazini, askari wa kikosi cha kutuliza ghasia wanavaa sare za rangi ya kijani kavu *(jungle green)*.

Nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba sare za Jeshi la Polisi ni sehemu ya vitendea kazi ambavyo vinahitaji kuboreshwa ili kuendana na mazingira ya kazi katika jeshi la polisi. Kwa kutambua hilo Wizara yangu kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi imeanzisha mchakato wa kuboresha sare hizo ili zikidhi haja na mazingira ya kazi za Jeshi la Polisi. Sare hizo zitaanza kutumika muda mfupi ujao.

**MHE. MOHAMMED AMOUR CHOMBOH:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Baada ya majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza. *Uniform* au sare za Polisi ni nguo ambazo anatakiwa azivae kila wakati anapokuwa kazini. Na mara nyingi sana tunapowaona baadhi ya askari wetu utakuta sare zao nyingine zimechoka kiasi ambacho zinavunja hali hasa ya lile Jeshi lenyewe.

Je! Wizara huwa inawapa pea ngapi hawa maaskari kwa ajili yakubadilisha sare zao hizo? Swali la pili; katika kuweka heshima ya Jeshi la Polisi hapo zamani ilikuwa ni marufuku Askari akivaa sare ya Polisi kumpakiza Askari mwenzake kwenye baiskeli, Je! Sheria hiyo bado ipo au imepitwa na wakati sasa?

**NAIBU WAZIRI WA USALAMA WA RAIA:** Mheshimiwa Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Waziri wa Usalama wa Raia, naomba kujibu swali la nyongeza lenye (a) na (b) la Mheshimiwa Chomboh, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa kawaida Askari wetu wanakuwa na sare zaidi ya moja na hivi sasa Jeshi la Polisi linachukua hatua kuhakikisha Askari wetu hao wanakuwa na sare nyingi na kama nilivyosema katika jibu la msingi ni kwamba sasa mchakato wa kutengeneza sare rasmi zinazofaa na kuvutia zaidi zimo mbioni na hivi karibuni sare hizo zitakamilika.

Kuhusu suala la Pili, Mheshimiwa Spika, kuhusu kupakiana haikuwa Sheria ni utaratibu wa Jeshi la Polisi na bado utaratibu huo upo.

Na. 151

**Matumizi ya Baiskeli Vijijini**

**MHE. JAMES P. MUSALIKA** aliuliza:-

Kwa kuwa, baiskeli ni nyenzo muhimu ya usafiri kwa Watanzania zaidi ya asilimia themanini (80%) waishio vijijini na kwa kuwa baiskeli inakidhi hali halisi ya uduni wa miundiombinu vijijini ambapo barabara za kupitisha magari hazipo; na kwa kuwa mvua nyingi zilizonyesha mwaka huu zimesababisha magari ya abiria na mizigo yasifike kabisa vijijini:-

(a) Je! Serikali itakubaliana nami kuwa, usafiri uliopo vijijini kwa sasa ni baiskeli kuliko magari?

(b) Je!, Serikali itakubali kwamba, kifungu cha 101 cha sheria ya barabarani na 30 ya mwaka 1973 *(the road traffic Act Cap. 168 R.E 200)* kinaruhusu mtu kubebwa kwenye kibao maalum au *carrier* nyuma ya baiskeli?

(c) Je! Serikali ipo tayari kutofautisha usafiri na usafirishaji kwa njia ya baiskeli unaofanywa mijini ili kuondoa kero wanazofanyiwa wananchi wengi vijijini kwa sasa na Jeshi la Polisi?

**NAIBU WAZIRI WA USALAMA WA RAIA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Usalama na Raia, napenda kujibu swali la Mheshimiwa James Philipo Musalika, Mbunge wa Nyang'wale, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali inafahamu kuwa wananchi wengi wa vijijini wanatumia usafiri wa baiskeli katika shughuli zao za kawaida.

(b) Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa sheria ya usalama barabarani namba 30 ya mwaka 1973, (*The road Traffic Act, Cap 168 R.E.* 2002) kifungu cha (101) kinaruhusu

mtu mmoja mwenye umri wa miaka (7) na kuendelea kubebwa kwenye kiti maalum kilichopo nyuma ya baiskeli.

(c) Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa sheria ya usalama barabarani namba 30 ya mwaka 1973 *Cap.* 168 (*Revised Edition* 2002) hairuhusu baiskeli kutumika kama chombo cha biashara. Matumizi yanayotambulika na sheria hiyo ni yale ya binafsi ya mtu anayemiliki baiskeli hiyo awe Mjini au Kijijini.

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua umuhimu wa usafiri wa baiskeli katika shughuli mbalimbali za Kijamii na Kiuchumi kwa Wananchi wake hasa wa Vijijini. Kwa kutambua hilo katika Bunge la Bajeti la mwaka huu Mheshimiwa Waziri Mkuu alitoa taarifa ya matarajio ya Serikali kuruhusu baiskeli na pikipiki kutumika kama vyombo vya kibiashara vya usafirishaji. Nawaomba Waheshimiwa Wabunge na Wananchi wawe na subira wakati Serikali inalifanyia kazi suala hili kwa manufaa ya wananchi wetu hasa waishio vijijini baada ya sheria hiyo kufanyiwa marekebisho ambayo yatakidhi matarajio ya Wananchi.

**MHE. KABUZI F. RWILOMBA:** Ahsante Mheshimiwa Spika, kuniruhusu kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza.

Katika Wilaya ya Geita maeneo ambayo yanaweza kupitika kwa magari ni Barabara tano tu Barabara karibu 31 zinapitika kwa baiskeli, sasa kusubiri Sheria ipite ili wananchi waweze kufanya shughuli zao, Mheshimiwa Waziri haoni kwamba ni huko ni kukwamisha maendeleo na kazi ya wananchi wa Geita?

Katika jibu lake amesema wananchi wavute subira, Je! Kwa kuwa sisi tunahitaji kufanya shughuli na kuendelea Mheshimiwa Waziri anaweza akaomba Polisi na wenyewe wavute subira mpaka sheria itakapokuja ili tuweze kuendelea na shughuli? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA USALAMA WA RAIA:** Mheshimiwa Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Waziri wa Usalama wa Raia, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema utaratibu huu uliopo ni wa kisheria kwa hivyo Askari Polisi wanatekeleza wajibu wao kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Spika, tatizo hili ni tatizo kubwa na kwa kuwa ni la eneo la MTAMBUKA linalohusu mamlaka mbalimbali ikiwemo polisi, kodi ya mapato, mamlaka ya leseni na usafirishaji, shirika la bima la Taifa, mamlaka za Jiji, Manispaa na Halmashauri za Wilaya na kwa kuwa matumizi ya chombo chochote cha usafiri kwa msingi wa biashara ya kubeba abiria au mizigo yanahusisha mikataba kati ya mmiliki wa chombo hicho na abiria hivyo iwapo sheria itaruhusu mmiliki wa pikipiki au baiskeli kubeba abiria na mizigo kwa malipo basi mmiliki huyo atatakiwa kuwa na yafuatayo:-

Tiketi au stakabadhi ya malipo inayothibitisha kuwepo kwa mkataba wa huduma hiyo ya usafiri, bima inayomkinga abiria endapo ajali itatokea, cheti cha ukaguzi wa ubora wa usalama wa baiskeli na pikipiki, malipo ya kodi yatokanayo na mapato ya biashara hiyo, wahakiki ya kuwa na leseni ya dereva wa baiskeli na pikipiki, leseni ya kufanyia biashara hiyo.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo vyombo hivi hivi sasa kuna uwezekano wa asilimia hamsini ya kutokea ajali wakati wa matumizi yake, sembuse inapotumika kibiashara ambapo shughuli zitaongezeka kwa hivyo ajali zitaongezeka suala zima hapa Mheshimiwa Spika, kuchelewa kwetu ni kuifanya sheria hii iboreke vizuri kwa manufaa ya watu wetu kuepusha vifo, kuepusha ajali na sheria itumike vizuri (*Makofi*)

**MHE. LUCAS L. SELELII:** Nashukuru sana Mheshimiwa Spika kwa kuniona, kwa kifupi kabisa Mheshimiwa Waziri mkuu katika kikao cha Bajeti aliahidi na wananchi walisikia kwa sababu bunge lako linatangazwa moja kwa moja na *Television* ya Taifa na vyombo vingine vya habari, aliahidi mwezi Novemba ambao ni huu kwamba sheria hii ingeletwa, sasa Mheshimiwa Waziri Mkuu anatuahidi ni lini sasa maana yake Novemba ndiyo tumemaliza anaahidi ni lini sheria hii italetwa?

**NAIBU WAZIRI WA USALAMA WA RAIA:** Mheshimiwa Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Waziri wa Usalama wa Raia naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Selelii, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema kwamba suala hili ni (Mtambuka), na ni suala nyeti na linahusu maisha ya watu wetu ndiyo sababu ambazo hufanya kuchelewa tusiweze kuleta katika Bunge hili la Novemba, nataka kumhakikishia kwamba Bunge lijalo mswada huu utafikishwa mbele ya Bunge hili, kwa sababu hatua zimefikia mwishoni kabisa.

Na. 152.

**Muungano wa Afrika.**

**MHE. ZUBEIR A. MAULID** aliuliza:-

Kwa kuwa, kumekuwa na kampeni ya msukumo mkubwa kutoka kwa baadhi ya uongozi wa Mataifa ya Afrika kutaka kuiunganisha Afrika ili kuwa na Afrika yenye Serikali moja; na kwa kuwa, nchi yetu iko kwenye harakati za kuanzisha Shirikisho la Afrika Mashariki litakaloundwa na nchi tano (5) katika Muungano wa Kisiasa.

Je!, kura za maoni zitakazotumika ili kupata ridhaa ya wananchi juu ya Muungano wa Afrika kama ilivyo kwa ule wa Afrika Mashariki?

**MHE. DR. CYRIL A. CHAMI-NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Nje na Ushiriakiano wa Kimataifa naomba kujibu swali na Mheshimiwa Zubeir A. Maulid, Mbunge wa Kwamtipura, kama ifuatavyo:-

Wazo la kuwa na Serikali moja ya Afrika siyo geni na halikuanza leo, lilianza tangu nchi za Afrika zilizopoanzakupata uhuru. Viongozi wa mwanzo kama hayati Kwame Nkrumah wa Ghana walianzisha wazo hilo na kuungwa mkono na viongozi wengi wa wakati huo. Hata hivyo, viongozi wengi kama hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, muasisi wa Taifa letu, walitaka Serikali hiyo ianzishwe hatua kwa hatua kwa kufuata mwenendo wa Maendeleo Barani Afrika.

Mheshimiwa Spika, kwa kipindi kirefu wazo hilo halikuwa linazungumzwa hadi hivi karibuni lilipoanzishwa upya na kiongozi wa Libya Muammar Gaddafi. Baada ya kuibua upya wazo hilo, Kamati mbalimbali ziliundwa na Wakuu wa Umoja wa Afrika kutoa mapendekezo ya kina zaidi kuhusu manufaa ya kuwa na Serikali moja Barani Afrika na muda muafaka wa kuunda Serikali hiyo.

Mheshimiwa Spika, nchi zote za Afrika zinaliona wazo la kuwepo na Serikali moja barani Afrika ni wazo zuri. Tofauti zinajitokeza juu ya muda muafaka wa kuunda Serikali hiyo. Nchi chache za Kiafrika zikiongozwa na mtoa wazo hilo, kiongozi wa Libya na kuungwa mkono na Serikali ya Senegal, Gabon, Guinea Conackry na kadhalika. zina msimamo kuwa Serikali moja ya Afrika ianzishwe mara moja. Idadi kubwa ya nchi za Kiafrika zikiongozwa na kundi la nchi za *SADC* na nchi za Mashariki mwa Afrika zina msimamo kuwa uundwaji wa Serikali ya Afrika uende hatua kwa hatua na utekelezaji huo uanze kwa kuimarisha Jumuiya za Kiuchumi za Kikanda *(Regional Economic Communities (R*ECs) na kushughulikia kwanza matatizo ya ndani ya nchi za Afrika ikiwa ni pamoja na tatizo la migogoro, umaskini, miundombinu, usafiri na kujitosheleza kwa wataalam.

Mheshimwa Spika, mkutano wa Tisa wa Wakuu wa Nchi uliamua iundwe Kamati ya Mawaziri watakaofuatilia masuala mbalimbali yanayohusu uundwaji wa Serikali hiyo na kutoa taarifa kwenye Mkutano wa Kumi na Mbili wa Baraza la Mawaziri utakaofanyika Addis Ababa, Ethiopia, mwezi Januari, 2008.

Mheshimiwa Spika, masuala muhimu yatakayofuatiliwa na Kamati ya Mawaziri kuhusu uundwaji wa Serikali mmoja ya Umoja wa Afrika ni pamoja na:-

(i) Nadharia ya Serikali moja Barani Afrika;

(ii) Uhusiano utakaokuwepo kati ya Serikali hiyo ya Muungano na Serikali za nchi mbalimbali pamoja na Jumuiya za Kikanda(*RECs*);

(iii) Tathmini ya utendaji kazi kati ya Kamati ya Baraza la Mawaziri, Kamisheni ya Afrika pamoja na vyombo vingine vyote vya umoja huo; na

(iv) Kutathmini hatua za kuchukuliwa kuelekea kwenye Serikali moja ya Afrika pamoja na muda wa utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, ni dhahiri kuwa wazo la kuunda Serikali ya Muungao wa Afrika lina ridhaa ya wananchi kama nilivyoeleza hapo juu, Serikali ya Tanzania ilikwishakusanya maoni kutoka vyombo mbalimbali ambavyo vinawakilisha wananchi na kupata msimamo wa nchi. Msimamo huo wa Tanzania na ile ya nchi mbalimbali za Afrika ndiyo iliyowafanya Wakuu wa nchi za Afrika kutoa uamuzi wa kuunda Kamati ya Mawaziri ambayo itatoa taarifa yake mwenzi Januari, 2008 na uamuzi wa mwisho utafanyika.

Mheshimiwa Spika, Kwa hivyo hatua ya kukusanya maoni ya wananchi imekwishapita na tungoje maamuzi ya Wakuu wa nchi wa Umoja wa Afrika yatakayotokana na taarifa ya Kamati ya Mawaziri.

Na. 153.

**Uharibifu wa Mazingira Mikoa ya Kagera na Kigoma**

**MHE. DR. CHRISANT M. MZINDAKAYA** aliuliza:-

Kwa kuwa tuliiomba *UN* kufanya tathmini ya uharibifu wa mazingira uliotokana na wakimbizi katika Mikoa ya Kagera na Kigoma:-

(a) Je, kazi hiyo imefanyika?

(b) Kama ndiyo, thamani ya uharibifu huo ni kiasi gani?

**MHE. DR. CYRIL A. CHAMI-NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Mzindakaya, Mbunge wa Kwela, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, matatizo ya uharibifu wa mazingira katika Mikoa ya Kagera na Kigoma yalipelekea Ofisi ya Makamu ya Rais, kuliomba Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia mazingira *(UNEP)* mnamo mwezi Aprili, 2003 kusaidia kufanya tathmini ya kupambana na madhara ya Wakimbizi kwa Mazingira. Mwezi Juni

mwaka huo huo, *UNEP* walikubali na kufanya tathmini ya madhara yaliyosababishwa na wakimbizi kwa mazingira kati ya Oktoba na Novemba, 2003.

(b) Mheshimiwa Spika, tathimini ya *UNEP* juu ya madhara ya wakimbizi wa Kimataifa na wale wa ndani kwa mazingira yaani *Impact of Refugees and Internally Displaced Persons on the Environment in Tanzania Assessment Report* ilichapishwa mwezi Machi, 2005. Tathimini ililenga maeneo ya misitu, maji, ardhi, wanyamapori, udhibiti wa taka na mfumo wa udhibiti wa maafa.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya maeneo yaliyoathirika kwa mujibu wa tathmini hiyo na ujio wa wakimbizi ni kama vile uharibifu wa misitu ya hifadhi, matumizi mabaya ya ardhi kutoka na na wakimbizi kushiriki katika kilimo, uharibifu wa vyanzo vya maji kutokana na umwagaji ovyo wa maji taka katika vyanzo vya maji na ufuaji katika mito na athari kwa wanyamapori kutokana na uwindaji na uvuvi haramu.

Hata hivyo tathmini hiyo haikuweza kutoa thamani halisi ya uharibifu huo kwa maana ya kiasi halisi cha fedha kilichopotea.

Mheshimiwa Spika, badala yake tathmini hii ilitoa pendekezo la mradi utakaolenga katika maeneo matatu. Eneo la kwanza ni kuboresha sera zilizopo na kuimarisha mipango ya upokeaji wa wakimbizi; Pili kuwepo mipango madhubuti ya kuongoa maeneo yaliyoathirika kwa ujiop wa wakimbizi na Tatu ni kujenga uwezo wanchi katika kupambana na majanga ikiwa ni pamoja na ujio wa wakimbizi kwa wingi.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla ujio wa wakimbizi hawa unafuatia Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuwa mstari wa mbele katika kuhakikisha amani inapatikana katika eneo la Maziwa Makuu, kama njia muhimu ya kuyanusuru mazingira yetu. Juhudi za Serikali yetu zimeanza kuzaa matunda kwani nchi jirani zinazozalisha wakimbizi kama Burundi na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo zimefanya chaguzi zake za kidemokrasia kwa amani na wakimbizi wengi wameendelea kurejea makwao. Hali hiyo itapunguza kwa kiasi kikubwa matatizo yaliyokuwa yakisababishwa na wakimbizi.

**MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE**: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Naibu Waziri, lakini nina swali moja dogo la nyongeza, baada ya tathmini hii kufanyika na kubaini hasara mbalimbali kama alivyozitaja. Je! Umoja wa Mataifa pamoja na mipango hii iliyozungumzwa na Serikali imekiri kutusaidia katika jambo lipi katika kulipa fidia ya madhara haya yaliyipatikana?

**MHE. DR. CYRIL A. CHAMI-NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA:** Mheshmiwa Spika kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa naomba kumjibu Mheshimiwa Simbachawene swali lake la nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika ujio wa wakimbizi katika nchi yetu ni jambo ambalo linatokana na kwa lazima kutokana na matatizo wanayapata katika nchi zao, na nchi ya Tanzania inakubali kuwapokea kwa sababu ya ubinadamu wetu, kwa sababu hatuwezi

kuwaacha wakafa wakati sisi ni nchi za amani na tunawapenda na tunawaambia kwamba Afrika ni mmoja.

Kwa hiyo mpaka sasa hivi hakuna mkakati ambao umefanywa na umoja wa Mataifa wa kutulipa fidia, lakini kama Mheshimiwa Mbunge anaona kwamba kuna namna mimi nitafurahi kabisa kupata mawazo yake ili tuweze kuona namna ya kuweza kushawishi Umoja wa Mataifa ili kwa kweli kusaidia na sio kulipa fidia, fidia unalipwa wakati labda unapoambiwa utoe huduma fulani kwa niaba ya Umoja wa Mataifa lakini maadamu tulikubali kwa hiari yetu wenyewe nafikiri mkakati hapa ni kuomba misaada mbalimbali ya kuwasaidia wakimbizi hawa waweze kurudi kwao na wenyeji wa Tanzania waweze kuyanusuru mazingira na kuweza kurudia katika hali nzuri ya maisha ambayo waliyokuwa nayo kabla wakimbizi hawajaingia katika nchi yetu.

**MHE. PONSIANO D. NYAMI:** Nashukuru Mheshimiwa Spika, kwa kuwa swali la msingi limetaja Mikoa ya Kagera na Kigoma, lakini pia katika Mkoa wa Rukwa kuna maeneo ya Mishamo na Katunda ambako kuna wakimbizi wa kutoka hukohuko Burundi na ni wengi sana na wao pia wameharibu mazingira kwa kiwango kikubwa.

Je! Tathmini hiyo iliyofanyika ilijumuisha pia na maeneo hayo ya Mkoa wa Rukwa au ilizingatia tu Mikoa ya Kigoma pamoja Kagera?

**MHE. DR. CYRIL A. CHAMI-NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa naomba kumjibu Mheshimiwa Mbunge swali lake la nyongeza kama ifuatavyo:-

Tathmini hii ilifanywa katika Mikoa ya Kigoma na Kagera kama nilivyosema katika jibu la swali la msingi, lakini Ofisi ya Makamu wa Rais iliombwa tathmini ifanyike katika Mikoa hiyo sio kwamba ndiyo imekuwa pekee ambayo ilikuwa imeathirika na tatizo la wakimbizi bali ilikuwa ni kama *pilot study* baada ya pale taasisi mbalimbali ambazo zinahusika na mazingira hapa nchini mojawapo ikiwepo na baraza la mazingira la Taifa limetoa miongozo kuwa Mikoa yote ambayo imeathirika na wakimbizi kama hiyo aliyoitaja ya Rukwa, Tabora na Mikoa mingine ya eneo la Magharibi mwa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, *NEMC* imetoa maelezo ya namna Mikoa hiyo inavyoweza kuangalia athari ambazo zimetokana na wakimbizi katika maeneo hayo na mchakato unaendelea lengo likiwa ni kuhakikisha kwamba wakimbizi hawa wanarudi mara moja katika nchi zao mara hali inapokuwa nzuri lakini vilevile lengo likiwa ni namna ya kuwasaidia wananchi wa Tanzania ambao wameathirika katika Mikoa yote hiyo ambao imekumbwa na wimbi la wakimbizi katika nchi yetu ya Tanzania.

**MHE. MHONGA S. RUHANYWA**: Ahsante Mheshimiwa Spika, kwa kunipa nafasi kuuliza swali moja la nyongeza, Mheshimiwa Naibu Waziri ametuambia kwamba

tathmini mbalimbali imefanyika hasa katika misitu, maji na wanyama pori, Je! Kuna mkakati yeyote ya kuhifadhi mazingira au kuboresha mazingira ambayo tayari yameshaharibiwa?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS MAZINGIRA**: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Ruhwanya kama ifuatavyo:-

Kwanza nichukue nafasi hii kuzipongeza taasisi mbalimbali ambazo zimesaidiana na Serikali katika kushughulikia hili suala la wakimbizi na uharibifu wa mazingira na taasisi hizo ni pamoja na *Relief Development Society, RODOSO, CARE TANZANIA, AFRICARE, Tanzania Christian Relief for Refugee Service, Christian Relief and Development Samaritan Enterprises Keepers Organisation.*

Mheshimiwa Spika, tunaliangalia hili suala katika maeneo mawili. Moja ni kujenga uwezo wa Halmashauri katika maeneo ambayo wakimbizi wapo katika kutekeleza mkakati wa Serikali wa kuhifadhi ardhi na vyanzo vya maji ili hili jambo liwe la kawaida kuainisha masuala hayo ya wakimbizi katika mipango yao ya kawaida, lakini vilevile tunaliangalia suala hili la uharibifu wa mazingira katika maeneo ya Magharibi mwa Tanzania kupitia mpango mkubwa ambao utaanza hivi karibuni wa hifadhi wa bonde la ziwa Tanganyika.

Na ninapenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kwamba kikwazo kilichokuwepo ilikuwa ni nchi ya *DRC- Congo* kutoridhia sasa hakipo tena kwani *DRC* sasa imeridhia mkataba huo, nakushukuru.

Na. 154.

***Dual Citizenship***

**MHE. BENSON M. MPESYA** aliuliza:-

Mheshimiwa Spika kabla sijauliza swali langu namba 154, kwa ridhaa yako naomba nitoe salaamu zangu za rambirambi kwa waumini wote wa kanisa la Wa-*Adventist* la Wasabato pale Mbeya Mjini kwa kufiwa na Askofu wao Mkuu pamoja Katibu wao Mkuu kwa ajali ya gari iliyotokea juzi. Naomba mwenyezi Mungu azilaze roho za marehemu pahali pema peponi. *Amin*

Kwa kuwa, kutokana na dhana ya utandawazi inaonekana kuwa suala la *Dual Citizenship* haliwezi kuepukika tena Tanzania:-

(a) Je! Ni sababu zipi za msingi zinazomzuia mtu kwa uzuri na mapenzi yake kuwa na uraia wa nchi mbili?

(b) Je! Kuna faida gani za kiuchumi na kijamii ambazo zitapungua ikiwa Mtanzania atapata uraia wa nchi nyingine?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Mpesya, Mbunge wa Mbeya Mjini, naomba kutoa maelezo ya utangulizi kama ifuatayo:-

Mheshimiwa Spika, uraia wa nchi mbili una maanisha mtu kuwa na uraia wa nchi mbili kwa wakati mmoja. Aidha, suala la uraia nchini linaongozwa na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 na sheria ya uraia Na. 6 ya mwaka 1995 na Kanuni zake za mwaka 1997.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, uraia ni suala la Muungano kama ilivyoainishwa katika Ibara ya 4(3).

Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa maelezo hayo kwa ufupi sasa naomba kujibu swali la Mheshimiwa Benson Mpesya, Mbunge wa Mbeya Mjini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, sababu inayomzuia Mtanzania kwa hiari yake na mapenzi yake kuwa na uraia wa nchi mbili ni sheria ya Uraia Na. 6 ya mwaka 1995, ambayo inatamka wazi kuwa endapo raia wa Tanzania ataupata uraia wa nchi nyingine kwa njia yeyote, isipokuwa kwa ndoa ataupoteza uraia wa Tanzania.

(b) Mheshimiwa Spika, hakuna faida zozote za kiuchumi na kijamii ambazo zitapungua endapo Mtanzania atapata uraia wa nchi nyingine. Ukweli ni kwamba Watanzania wengi wanaoomba iruhusiwe kuwa na uraia wa nchi ya pili, wanafanya hivyo ili wafaidike na maslahi ya kiuchumi hususani ya elimu, tiba na ajira ambayo yatapatikana bure au kwa gharama nafuu kutokana na kuwa raia wa nchi husika wanakoishi.

Mheshimiwa Spika, pamoja na maelezo hayo, suala la uraia wa nchi mbili bado linafanyiwa kazi na Serikali pindi litakapokamilika Bunge lako Tukufu litafahamishwa kwani suala hili ni la Muungano hivyo linahitaji majadiliano ya kina na makubaliano ya pande zote mbili za Muungano. *(Makofi)*

**MHE. BENSON M. MPESYA**: Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri nina maswali mawili madogo ya nyongeza:-

(1) Kwa kuwa Watanzania wengi wana wasiwasi na hofu kwamba uraia wa nchi mbili unaweza ukatumika kama kichaka cha maovu dhidi ya Serikali yetu na wanatoa mfano wa huyu mtuhumiwa wa Rada kwamba kinachomsaidia asikamatwe mpaka sasa hivi ni kwa sababu ya kuwa na uraia wa nchi mbili, Je! Serikali itakapokuwa inalifanyia kazi hili itatilia maanani sababu kama hizi?

(2) Kwa kuwa mahali palipo na hazina yako ndipo palipo na roho yako, nchi zetu changa hazina yake kubwa ni wataalamu wake wachache walionao, serikali itadhibiti vipi kuhakikisha kwamba hizi *best brain* za nchi zetu haziendi kwenye nchi tajiri pindi tutakaporidhia uraia wa nchi mbili?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya waziri wa mambo ya ndani ya nchi, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya mheshimiwa Mpesya kama ifuatavyo:-

Kwanza Mheshimiwa Spika, kama nilivyowaeleza katika jibu langu la msingi suala hili bado halijafanyiwa kazi, lakini ningependa kumthibitishia Mheshimiwa Mbunge kwamba uraia wa nchi mbili haizuii Serikali ya tanzania kukamata na mwadhibisha Mtanzania yeyote yule atakayekuwa amevunja sheria za nchi yetu, lakini kama nilivyoeleza suala hili ni suala la Muungano ni suala ambalo tutachukua mawazo ya watu wengi na baada ya hapo tutalifikisha katika Bunge hili Tukufu ili Bunge liamue vipi tuende.

Suala la *first brains* kuondoka hapa Nchini, hayo ndiyo maswala ambayo tunaangalia katika mchakato mzima wa kuamua kama uraia wa nchi mbili uwepo au usiwepo. Ningependa Mheshimiwa Mbunge asiwe na hofu, Serikali iko makini tutaifanyia kazi suala hili la tutalileta hapa Bungeni pale litakapokuwa tayari.

Na. 155

**Uwezo wa Idara ya Zimamoto**

**MHE. FATMA MUSSA MAGHIMBI** aliuliza:-

Kwa kuwa, hivi karibuni katika maeneo ya *Area "D"* ilitokea ajali ya moto ambapo nyumba moja iliungua na kuteketea kabisa pamoja na vitu vyote vilivyokuwemo, na kwa kuwa ilichukua muda mwingi sana kuwapata watu wa Zimamoto na hata walipopatikana Dereva wa gari hilo hakupatikana, na ikabidi Askari Polisi asaidie kuli – *operate* gari hilo na ilikuwa kazi ngumu kwa Askari huyo kulitumia. hata hivyo, moto huo ulizimwa na Askari wa Polisi kusaidiana na wananchi.

Je, Serikali haioni haya ya kubinafsisha huduma hiyo ya Zimamoto kutokana na uwezo mdogo wa Idara hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, kabla sijajibu swali la Mheshimiwa Fatma M. Maghimbi Mbunge wa Chake Chake, ningependa kutoa ufafanuzi wa awali kwamba kwa kuwa, Bunge hukutana hapa Dodoma

Wizara yetu imechukulia kuwa *Area D* ambayo imetajwa katika swali hili ni *Area D* ya hapa Dodoma.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kutoa pole kwa Bwana John Lwoga aliyeunguliwa nyumba yake maeneo ya *Area D*, Manispaa ya Dodoma tarehe 11/12/2006. Baada ya kusema hayo napenda kutoa jibu la swali la Mheshimiwa Fatma Mussa Maghimbi, Mbunge wa Chake Chake kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kulitokea tukio la moto wa nyumba tarehe 11/12/2006 maeneo ya *Area D* Manispaa ya Dodoma. Taarifa ya moto huo wa nyumba ilipokelewa kwenye Kituo cha Zimamoto na Uokoaji Manispaa ya Dodoma saa saba kasoro dakika kumi usiku. Gari la kuzima moto Na. SM 2882 liliondoka kituoni kwenda kwenye tukio. Lilitumia dakika sita kufika kwenye eneo la tukio. Hali waliyokuta iliwa siyo nzuri kwa kuwa moto ulikuwa umeshawaka kwa kasi ambayo ilisababisha madhara makubwa ya kuungua vitu.

Mheshimiwa Spika, Kituo cha Zimamoto Manispaa ya Dodoma kina upungufu wa Askari wa Zimamoto wakiwemo madereva. Kuna madereva watatu tu. Kila *shift* ina dereva mmoja. Siku ya tukio magari mazima ya kusima moto yalikuwa matatu. Dereva (Askari Polisi) aliombwa aendeshe gari moja la kuzima moto Na. SM 2784 hadi kwenye tukio, alipofika na gari hilo ni Wazimamoto wenyewe ndio ambao waliendesha mitambo ya kuzima moto. Askari Polisi hana ujuzi wa kuendesha *pump* ya kuzima moto.

Mheshimiwa Spika, lengo la Serikali ni kukimarisha shughuli za Vikosi vya Zimamoto na Uokoaji nchini kote. Kupitishwa kwa Sheria ya Zimamoto Na. 14 ya Mwaka 2007 ni hatua moja wapo nzito katika kutekeleza azma ya kuhakikisha tunakuwa na Zimamoto ya kisasa yenye uwezo wa kukabiliana na majanga mbalimbali yakiwemo ya moto.

Mheshimiwa Spika, kutokana na maelezo hayo hakuna sababu ya kubinafsisha shughuli za Zimamoto na Uokoaji.

Mheshimiwa Spika, ningependa kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge, kwamba kampuni binafsi zilizosajiliwa zinaruhusiwa kutoa huduma maalum kama za kuzima moto na kuokoa, na tayari zipo kampuni tatu ambazo zinatoa huduma hizo. Kampuni hizi ni *Ultimate Security*, *Knight Support* na *Security Group*. Nayapongeza na kuyashukuru Makampuni hayo kwa ushirikiano wao mzuri kila linapotokea janga la moto hususani katika Mkoa wa Dar es Salaam.

**MHE. NURU AWADH BAFADHILI:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa kazi hii ya kupambana na uzimaji moto ni kazi ya Serikali.

(a) Je, inapotokea wananchi wakashirika sana kusaidia Serikali inawapa motisha gani wananchi hawa?

(b) Kwa mujibu wa majibu aliyotoa Mheshimiwa Waziri amesema wakati ajali hiyo ilipotokea magari yalikuwa yapo ya kutosha isipokuwa kulikuwa na matatizo ya wafanyakazi. Je, Serikali haioni kuna kila sababu ya kuongeza wafanyakazi wengine ili kusaidia katika matukio kama hayo?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, ningependa kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba ni jukumu la Serikali kusaidia na kuokoa mali za watu pale inapotokea janga la moto. Lakini pia ni jukumu la wananchi kwa ujumla kusaidia kutokana na utu na ubinadamu tulionao Watanzania. Ningependa kuendelea kutoa rai kwa wananchi pale ambapo linatokea tatizo kama hilo wajitolee kwa moja mmoja kuwasaidia Watanzania wenzao. Kuhusu tatizo la wafanyakazi ni kweli kwamba kuna upungufu wa askari zimamoto katika baadhi ya maeneo hapa nchini na Serikali yako kwa kupitia Bajeti ya mwaka huu inayo mpango wa kuongeza hawa askari zimamoto. (*Makofi*)

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, ingawa muda wa maswali sasa umepita, lakini mtakumbuka tulianza na shughuli mbalimbali za uwasilishaji taarifa na kadhalika. Kwa hiyo, nitaruhusu swali la mwisho linaloelekezwa Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo nalo linaulizwa na Mheshimiwa Kaika Telele, Mbunge wa Ngorongoro.

Na. 156

**Usikivu wa Radio Tanzania na Televisheni ya Taifa – Ngorongoro**

**MHE. KAIKA S. TELELE** aliuliza:-

Kwa kuwa usikivu na muonekano wa *Radio Tanzania Dar es Salaam* (*RTD*) na Televisheni ya Taifa (TVT) ni hafifu sana katika maeneo mengi ya Tarafa ya Loliondo, Salen na Ngorongoro na kwa kuwa vyombo hivyo vya habari ni muhimu sana katika kuelimisha na kuhamasisha wananchi katika masuala ya maendeleo ya taifa letu na kwa kuwa, wananchi wa Vijiji vya Tarafa hizo wanapatikana sana na Jamhuri ya Kenya ambapo *KBC* inasikilizwa sana:-

(a) Je, ni sababu zipi zinasababisha *RTD* isisikike na TVT isionekane katika maeneo hayo?

(b) Je, Serikali haioni kwamba wananchi wake wakisiliza *KBC* kwa miaka mingi watathamini zaidi mambo ya Kenya na kupunguza uzalendo kwa nchi yao wenyewe?

(c) Je, Serikali, inawaambia nini wananchi wa Ngorongoro kuhusu hoja zao hizo?

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO (MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Kaika S. Telele, Mbunge wa Ngorongoro, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo. Sehemu (a) na (c) yanajibiwa kwa pamoja kama ifuatavyo:-

(a) Kwanza kabisa nakubaliana na Mheshimiwa Kaika S. Telele, Mbunge wa Ngorongoro, kuwa usikivu wa *Radio Tanzania (RTD)* na mwonekano wa Televisheni ya Taifa ni hafifu sana siyo tu katika maeneo ya Tarafa za Liliondo, Salen na Ngorongoro, bali pia katika baadhi ya maeneo mengine ya nchi yetu.

Sababu moja ya msingi ya kutosikika na kutoonekana vizuri kwa *Radio Tanzania* na Televisheni ya Taifa ni nguvu ndogo ya mitambo na umbali wa urefu kutoka mahali ambapo mitambo ya kurushia matanganzo imefungwa. Mitambo ya kurushia matangazo ya *Radio Tanzania* na Televisheni ya Taifa ambayo maeneo ya Loliondo, Salen na Ngorongoro yanatarajia kupokea imefungwa katika miji ya Arusha na Dodoma.

Mheshimiwa Spika, ufungaji wa mitambo ya *Radio* aina ya *FM* tayari umekamilika katika miji ya Dodoma na Arusha. Hali hii itaongeza nguvu na kufanya baadhi ya maeneo ya Mkoa wa Manyara ambao umepakana na Arusha yakiwemo ya Tarafa za Loliondo, Salen na Ngorongoro kupokea matangazo ya *Radio Tanzania* kwa usikivu mkubwa.

Mikoa mingine ambayo ufungaji wa mitambo mipya ya *Radio FM* ipo kwenye hatua ya mwisho kuweza kurusha matangazo yake ni pamoja na Mbeya, Tabora, Kigoma, Mwanza, Bukoba, Musoma na Tanga. Katika kipindi cha wiki moja kuanzia sasa baadhi ya Mikoa hiyo itaanza kupokea matangazo ya *Radio Tanzania* kwa usikivu unaokubalika. Aidha, awamu ya pili ya ufungaji wa mitambo mipya ya *FM* katika Mikoa mingine iliyobaki utahusisha moja kwa moja Mkoa wa Manyara.

(b) Hatuamini kuwa kusikiliza kwa *KBC (Kenya Broadcasting Cooperation)* kunaweza kuleta athari kwa wananchi na Maendeleo ya Taifa. Bado Watanzania wa Tarafa ya Loliondo, Salen na Ngorongoro wataendelea kuthamini nchi yetu na kubaki kuwa wazalendo kama walivyo hivi sasa.

**MHE. KAIKA S. TELELE:** Mheshimiwa Spika, pamoja na maelezo mazuri na ya kutia matumaini ya Mheshimiwa Naibu Waziri nina swali moja kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa tunatambua uwezo na umaarufu wa Mkurugenzi wa *Radio Tanzania* Ndugu Tido Mhando, aliyekuwa mtangazaji wa *BBC* na kwa sababu alifanyakazi kubwa na nzuri alipokuwa *BBC.* Je, Serikali iko tayari kumwezesha Mkurugenzi huyu ili aweze sasa kufanyakazi hii ya TVT na *RTD* iweze kusikika na kuonekana vizuri maeneo ya tarafa ya Loliondo, Salen na Ngorongoro na maeneo mengine ya nchi yetu ambayo usikivu ni hafifu? (*Makofi*)

**SPIKA:** Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri ingawa sidhani kwamba Serikali itafanya hivyo kama zawadi kwa Tido Mhando. Nadhani tuna haki tu wananchi ya Radio yetu kuisikia.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO (MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali moja la Mheshimiwa Kaika Telele, Mbunge wa Ngorongoro kama ifuatavyo:-

Uwezo na umaarufu wa Ndugu Tido Mhando, kama alivyosema unafahamika alifanyakazi nzuri kule *BBC* na ndiyo maana Serikali ikamwona na hatimaye kumwajiri kama Mkurugenzi Mkuu wa Shirika letu la Utangazaji *(Tanzania Broadcasting Cooperation (TBC).*

Mheshimiwa Spika, niseme tu kwamba tangu Tido Mhando ameanza kufanyakazi hii Serikali imemwezesha kwa kiwango kikubwa sana ikiwa ni pamoja na kurekebisha muundo wa shirika lenyewe ambalo muundo wake umebadilika kidogo. Lakini kubwa zaidi yeye na timu yake wanafanyakazi vizuri sana. Ndiyo maana nimesema ile Mikoa ya Kigoma, Tabora na Bukoba, mpaka Jumapili wiki hii usikivu wa *Radio Tanzania* utakuwa umeongezeka kwa kiwango kikubwa. Mheshimiwa Spika na wewe kule kwako Urambo hata ukiwapigia simu Tabora leo tarehe 13/11/2007 usikivu wa *Radio Tanzania* umeongezeka kwa kiwango kikubwa sana kwa sababu jana tumefunga mitambo ya kisasa katika mji wa Tabora.

Kazi hii inaendelea na dhamira ya Serikali ni kuwezesha timu yetu mpya ya *Tanzania Broadcasting Cooperation* kuweza kufunga mitambo hii nchi nzima ili *Radio Tanzania* na Televisheni ya Taifa iweze kusikika vizuri na kwa Televisheni ya Taifa bila hata kutumia ungo. Huo ndiyo mkakati ambao tunao. Hiyo, kazi inafanywa na Wizara na Tido Mhando na timu yake ya Watalaam katika shirika letu la *TBC.*(*Makofi*)

**MHE. SUZAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri amekiri uwepo wa *poor reception* katika maeneo mengi ya nchi hii ya TVT na kwa kuwa TVT ilipata *tender* ya kuonyesha mechi ya ligi za Uingereza na kwa maana hiyo washabiki wake wengi hawaioni kutokana na hiyo *poor receiption*. Je, Serikali haioni kwamba kwa kufanya hivyo hawaitendei haki wale wapenzi wa mechi za mpira hasa ukizingatia kwamba vijana wengi wanajifunza kwa kuangalia mechi katika Televisheni zetu na kwa nini basi mechi hizo zisirudishwe kwenye *ITV* na *Channel Ten* ambazo kwa kweli zinaonekana sana nchi nzima? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO (MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge Suzan Lyimo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, usikivu wa Televisheni zote bado ni mdogo nchi nzima. Wengi wanaopokea matangazo ya Televisheni zetu zote tulizokuwa nazo hapa bado ni

wakazi wengi wa mijini kuliko vijijini. Wakazi wengi wa mijini kama mnavyofahamu wengi ni chini ya asilimia 20. Kwa hiyo, *tender* waliyopata Televisheni ya Taifa ni kuendelea kutoa burudani ya mpira ambayo wanafanyakazi nzuri hiyo katika maeneo mengi ya mijini na yale maeneo ya vijijini ambayo wenye *generators* na wenye nyungo wanaweza ku-*access* matangazo yale vizuri zaidi.

Mheshimiwa Spika, lakini nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba kazi inayofanywa na Televisheni ya Taifa katika yale maeneo yanayosikika katika hiyo asilimia 20 ni kubwa sana na isingeweza kufanywa na Televisheni nyingine yoyote. (*Makofi*)

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge maswali yamekwisha na muda wa maswali umepita, sasa kama kawaida yetu ni matangazo.  Nitaanza na wageni, wageni wetu mtakapotamkwa wale mnaohusika basi muweze kusimama ili Waheshimiwa Wabunge waweze kuwatambua.

Mheshimiwa Dr. Lucas Siyame, Naibu Waziri Ofisi ya Waziri  Mkuu, anao wageni watatu ambao nitawataja mmoja ni Mwenyekiti wa Mamlaka ya Mji mdogo wa Mbozi Bwana Mussa Lungwe,  pale alipo asimame na Bwana Adamu Mwashiga ambaye ni Afisa Mtendaji wa Mji Mdogo wa Mbozi na Bwana Justine Munishi Meneja wa Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka pale Mbozi, karibuni sana.

Mheshimiwa Ludovick Mwananzila, Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi anao wageni wawili kama ifuatavyo, Mheshimiwa Diwani Epharaem Kauzeni wa Kata ya Matayi na ni Msaidizi wa Mbunge wa Jimbo la Kalambo, karibu sana Mheshimiwa Diwani. Bwana Ernest Lupamba, Mwenyekiti wa Kijiji cha Matai B,  yule pale karibuni sana.

Mheshimiwa Beatrice Shellukindo wa Kilindi anao wageni wafuatao: Bi. Sheila Michael ambaye alikuwa mkufunzi wake yule pale *your welcome to the chamber please*. Halafu na Helen Michael  binti wa Mkufunzi huyo, *the daughter of Sheila Michael, she is not there, you are welcome*. Wageni wa Mheshimiwa Silvanus Mwijage, kama ifuatavyo: Stella Silvanus ambaye ni mwanaye, Savelina Mkinzile ambaye ni Bibi au nyanya yake, karibu sana bibi.  *(Makofi)*

Tunao pia wafanyakazi 22 wa Shirika la Posta nchini ambao wapo katika mafunzo maalum ya shughuli za posta.  Wafanyakazi wa Shirika la Posta tafadhali, wale pale karibuni sana. Tuna mgeni mmoja wa Mheshimiwa John Lwanji ambaye ni Mwenyekiti wa CCM Kitanula, Bwana Juma Hamis Kambi. Tuna wanafunzi 30 kutoka Chuo cha Madini hapa Dodoma, tunaomba wasimame tafadhali, tunawakaribisha wataalam wetu  wa madini ni kitu muhimu sana katika maendeleo ya nchi yetu. Ni matumaini yetu mtajifunza kwa makini ili sekta hiyo izidi kuwa ni ya tija kwa nchi yetu, karibuni sana.

Tunao wanafunzi wa kidato cha sita shule ya Sekondari Bihawana pamoja na walimu wanne. *Bihawana High School,* wale pale karibuni sana, karibuni vijana

tunafurahi kuwaona mfanye kazi kwa bidii, msome kwa bidii, Tanzania inawahitaji sana mkifanya vizuri. Tunao wanafunzi 11 wanaochukua mafunzo kazini ofisi ya Bunge, wale wanaochukua mafunzo Ofisi ya Bunge wasimame ratiba yao haiwaruhusu kuwa hapa wakati huu. Kuna wageni wa Mheshimiwa Maida Abdallah, Bi. Fatuma mdogo wake kutoka Dodoma wageni wa Mheshimiwa Maida na Hilham Said mwanawe Mheshimiwa.

Nafurahi pia kumkaribisha mgeni wa Mheshimiwa James Musalika yeye ni mtaalam wa ushauri wa *Aman Forum* ambaye anatoka Makao Makuu ya *Amani Forum* Nairobi Dr. Mutai Muji, yule pale karibu sana Dr. Mutai tunafurahi kukaribisha hapa na pia tunashukuru kwa kazi nzuri sana inayofanywa na *Amani Forum* hapa Afrika Mashariki.

Mikutano ya Kamati, Mheshimiwa Omar Kwaagw’ anahitaji kwamba wajumbe wote wa Kamati ya Huduma za Jamii wakutane leo katika ukumbi wa Pius Msekwa saa nne na nusu Kamati ya Huduma za Jamii katika Ukumbi wa Pius Msekwa, nadhani wanakutana na wadau kwa sababu ukumbi huo ni mkubwa.

Mheshimiwa Job Ndugai, Mwenyekiti wa Kamati ya Maliasili na Mazingira ameniomba niwatangazie wajumbe wa Kamati ya Maliasili na mazingira kwamba leo saa tano asubuhi kutakuwa na kikao cha Kamati ukumbi Na. 227 gorofa ya pili. Kwa hiyo, Kamati ya Maliasili ya Mazingira saa tano asubuhi ukumbi Na. 227 gorofa ya pili.

Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi ameniomba niwatangazie wajumbe wote Kamati ya Fedha na Uchumi kuwa leo saa nne unusu katika ukumbi Na. 231 kutakuwa na kikao kwa hiyo Kamati ya Fedha Uchumi, mara baada ya matangazo haya ukumbi Na. 231.

Mheshimiwa Mohamed Missanga, Mwenyekiti wa Kamati ya Miundombinu, anaomba wajumbe wote wa Kamati ya Miundombinu wakutane leo saa tano asubuhi, ukumbi Na. 432 gorofa ya nne. Kwa hiyo, Kamati ya Miundombinu ukumbi 432 saa tano asubuhi hii.

Mheshimiwa George Malima Lubeleje, Mwenyekiti, Kamati ya Katiba Sheria na Utawala anaomba wajumbe wote wa Kamati ya Katiba Sheria na Utawala, pamoja na wajumbe wa Kamati ya Huduma za Jamii wakutane kwenye kikao cha pamoja saa saba mchana chumba ukumbi 432.

Mheshimiwa Estherina Kilasi, Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali, anaomba wajumbe wa Kamati hiyo ya Hesabu za Serikali wakutane saa saba kamili katika ukumbi Na. 227.

Mheshimiwa William Shellukindo, Mwenyekiti wa Kamati ya Uwekezaji na Biashara, anahitaji wajumbe wote wa Kamati hiyo ya Uwekezaji na Biashara, wakutane saa saba mchana ukumbi Na. 231.

Mheshimiwa Dr. Raphael Chegeni Mwenyekiti wa Kamati ya Utendaji ya *CPA Tanzania* anaomba wajumbe wote wa Kamati ya Utendaji ya *CPA Tanzania Branch* kukutana leo saa tano asubuhi ukumbi Namba 133 gorofa ya kwanza.

Naomba wajumbe wote wa Kamati ya Kanuni na Kamati maalum niliyoiteua kushughulikia Kanuni tukutane kesho, kesho saa saba mchana tupitie kwa mara ya mwisho rasimu ya Kanuni za Bunge, kwa lengo la kuziwalisha Alhamisi tarehe 15 Novemba, 2007 ndani ya Bunge, kwa hiyo wajumbe wote wa Kamati ya Kanuni na Kamati maalum niliyoiteua kushughulikia Kanuni tukutane saa saba katika ukumbi wa Spika, kesho Jumatano tarehe 14 Novemba, 2007. Katibu wa Bunge anatangaza kwamba rasimu ya mwisho ya Kanuni mpya za Bunge toleo la 2007 tulizokuwa tunazifanyia kazi hivi sasa zinatawanywa. Tafadhali uziangalie kwa siku mbili hizi ili kuweza kuzipitia kwa urahisi kesho kutwa tarehe 15 Novemba, 2007.

Waheshimiwa Wabunge, bado kuna usumbufu katika ukaguzi pale kwenye geti, kuu la kuingilia tumefanya mashauriano. Katibu wa Bunge amekutana na wahusika katika Idara ya Usalama wa Taifa. Utaratibu mpya unahitaji kufanyiwa kazi kidogo kwa maana ya kwamba sasa hivi ukaguzi wote unafanyika pale pale getini, lakini tulidhani wale wanaopita kwa magari ingewezekana kabisa, chombo kinachohusika katika vipimo kikishafanya kazi yake basi kufungua boneti na mambo mengine kama hayo ifanyike mahali pa egesho ili kusiwe na msululu mrefu.

Lakini nakumbushwa kwa wale ambao wakishashuka wanapita kwa miguu hawana vitambulisho. Kwa hiyo, watu wa usalama pamoja na kwamba wameanza kuwazoea baadhi yenu Waheshimiwa Wabunge, lakini si rahisi kwa mtu aliyefundishwa mambo haya ya ulinzi akaamini kwamba yeyote aliyevaa kinadhifu pale ni Mbunge. Kwa hiyo, tunakumbushwa tafadhali sana vile vitambulisho vyetu kuvaa shingoni ni muhimu sana itapunguza sana sehemu ya adha ya ukaguzi na kadhalika.

Kuhusu hoja ya kukaguliwa na Mbwa sasa hili hatuna uwezo nalo mbwa wanatumika kunusa vitu vya hatari. Kwa hiyo, wale ambao hawapendi kusogelewa na mbwa sijui tufanyaje. Nadhani labda Mheshimiwa Galinoma na wale wengine wa Iringa wawasaidie tu kwa sababu mbwa sio mnyama mbaya hasa mbwa aliyefugwa. Naona Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani anacheka zaidi. Lakini kwa kifupi suala zima tunalifanyia kazi na tunategemea ugeni wa Mkurugenzi Mkuu Usalama wa Taifa ili tukamilishe utaratibu mpya ambao utakuwa mzuri na kero zitapungua. *(Makofi)*

Kuhusu humu ndani ya ukumbi kuna Mheshimiwa Mbunge nadhani nimtaje tu Mheshimiwa Rosemary Kirigini ghafla amehama kiti chake. Upo utaratibu ni vizuri Spika akafahamishwa kuhama tu ni kweli tunazo nafasi niseme tu kwamba Mheshimiwa Spika hataki kujua sababu ya kuhama ila ni vizuri tu kufahamishwa kwa sababu hata vitambulisho vimekaa kulingana na sehemu ambazo mlipangiwa awali. (*Makofi*)

Nawashukuru kwa usikivu nasikitika mambo yamekuwa marefu lakini siku nyingine ndivyo inavyokuwa. Sasa tunaendelea, Katibu kwa shughuli inayofuata.

## HOJA ZA SERIKALI

## AZIMIO

### Azimio la Bunge la Kuridhia Marekebisho ya Mkataba wa Kuanzisha Jumuiya ya Afrika Mashariki

**WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha mapendekezo ya kuridhia Azimio la Marekebisho ya Mkataba Ulioanzisha Jumuiya ya Afrika Mashariki yaani Mkataba wa Mwaka 1999.

Mheshimiwa Spika, kabla sijawasilisha Azimio naomba kwa niaba ya wananchi wa Kibaha Vijijini kuungana na Waheshimiwa Wabunge walionitangulia kutoa salaamu zangu za rambirambi kwa familia ya Marehemu Salome Mbatia na wengineo waliopata nao ajali. Pia kutoa rambi rambi kwa wahanga wa ajali iliyomhusisha Waziri wa Ulinzi Mheshimiwa Prof. Juma Kapuya na kumtakia yeye mwenyewe nafuu mapema. Wazazi na Ndugu wa Waheshimiwa Wabunge mbalimbali na Watanzania wengine ambao wamepata ajali katika maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, aidha, napenda kutoa pole kwa wale waliopata ajali mbalimbali akiwemo Mheshimiwa Mudhihir M. Mudhihir na kwa wagonjwa wakiwemo Mheshimiwa Sophia Simba, Mheshimiwa Zainab Vulu na wengineo kwa kweli nawatakia kila heri wapone haraka.

Mheshimiwa Spika, naomba kuchukua nafasi hii kwanza kabisa kuishukuru Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje ambayo jana katika mkutano iliongozwa na Makamu Mwenyekiti wake Mheshimiwa Mussa Zungu, Mbunge maarufu wa Ilala. Naishukuru Kamati hii kwa kupitia Azimio ninalowasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu leo hii.

Mheshimiwa Spika, leo nimesimama kuwasilisha kama nilivyosema awali Mapendekezo ya Azimio la Kuridhia Marekebisho ya Mkataba Ulioanzisha Jumuiya ya Afrika Mashariki Mwaka 1999. Nafanya hivyo kwa mujibu wa Ibara ya 23 (3) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977 inayotoa mamlaka kwa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuridhia Mikataba na makubaliano mbalimbali ya kimataifa kwa niaba ya wananchi wa Tanzania.

Kama Waheshimiwa Wabunge wanavyofahamu dira kuu ya mkataba wa kuanzishwa kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki Mkataba wa 1999 ni kuwa na kanda ya Afrika Mashariki iliyostawi yenye ushindani, iliyo salama na iliyoungana kisiasa. Aidha, malengo yake ni kupanua na kuimarisha ushirikiano kiuchumi, kijamii, kiutamaduni na kisiasa ili kuboresha maisha ya watu waishio Afrika Mashariki.

Ili kufikia dira na malengo niliyoyataja, Mkataba wa Jamuiya ya Afrika Mashariki, una sehemu nne za mtangamano yaani *integration stages.* Sehemu hizi ni Umoja wa Forodha, Soko la Pamoja, Sarafu Moja na hatimaye Shirikisho la kisiasa.

Jumuiya tayari iko katika hatua ya Umoja wa Forodha na maandalizi ya majadiliano ya Soko la pamoja yameanza.

Mheshimiwa Spika, Jumuiya ya Afrika Mashariki pia imetunga Mikakati Mitatu ya Maendeleo yaani *Strategic Development Programmes.* Mkakati wa kwanza ni wa mwaka 1997 hadi 2000 ambapo kazi kubwa ilikuwa kuanzisha upya Jumuiya ya Afrika Mashariki na mafanikio ya mkakati huo wa maendeleo ni kutiwa saini kwa Mkataba wa Jumuiya ya Afrika Mashariki wa mwaka 1999. Mpango wa pili ni kati ya mwaka 2001 na 2005 ambapo mafanikio makubwa yalikuwa kuanzishwa kwa Umoja wa Forodha. Mkakati wa tatu ni wa mwaka 2006 hadi 2010 yaani awamu hii tuliyokuwa nayo hivi sasa ambapo Jumuiya ya Afrika Mashariki inategemea kukamilisha majadiliano ya Soko la Pamoja na pia kuanza utekelezaji wa miradi ya maendeleo iliyopewa kipaumbele katika sekta mbalimbali kama vile kilimo na chakula cha uhakika au chakula cha kutosha, kuendeleza viwanda, utalii, miundombinu, afya, elimu, nishati, mazingira na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafaniko yote haya, tangu mwaka 1999, Mkataba wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, ilijikita katika mfumo wa Jumuiya ya Afrika Mashariki yenye nchi tatu yaani Kenya, Uganda na Tanzania. Aidha, katika baadhi ya maeneo Mkataba wa Jumuiya ya Afrika Mashariki haukutilia maanani baadhi ya tofauti za kiutawala katika nchi wanachama.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, kwenye Ibara ya 3 na Ibara ya 48 za Mkataba, nchi wanachama zimetajwa kuwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Jamhuri ya Uganda na Jamhuri ya Kenya. Hivyo basi ingawa waanzilishi wa Afrika Mashariki wanaamini kwamba Jumuiya ya Afrika Mashariki ni sehemu tu ya jitahada za kupata Umoja wa Afrika nzima na ingawa mkataba wenyewe pia unatambua katika Ibara ya 3 sehemu ya pili, uwezekano na utaratibu wa kuingiza wanachama wengine. Mkataba umeendelea kutaja nchi tatu tu, kama vile hakutatokea wakati ambapo nchi zingine zitataka kujiunga. Aidha, Ibara ya 48 ya Mkataba wa Jumuiya ya Afrika Mashariki inayohusu Wabunge wa Bunge la Afrika Mashariki, imetaja bayana kuwa Bunge hilo litakuwa na Wajumbe 27 tu wa kuchaguliwa, 9 kutoka kila nchi mwanachama. Maana yake ni kwamba wanapokuwa na wanachama wapya, nchi hizo au wanachama hao hawawezi kuchagua na kupeleka Wabunge wao kwenye Bunge la Afrika Mashariki bila ya kwanza kufanya marekebisho ya mkataba wa Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa mujibu wa Ibara ya 150 wa Mkataba huo.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa mifumo ya utawala, nchi wanachama za Afrika Mashariki zinatofautiana hapa na pale juu ya mambo ya utawala na hususan juu ya nafasi ya Mwanasheria Mkuu katika Serikali. Wakati katika baadhi ya nchi wanachama, Mwanasheria Mkuu anatambulika kama Waziri na Mjumbe wa Baraza la Mawaziri katika nchi zingine au katika wanachama wengine, Mwanasheria Mkuu si Waziri bali ni Mjumbe Mwalikwa wa Baraza la Mawaziri au *Ex-Official Member* wa Baraza la Waziri. Tofauti hii imesababisha Baraza la Sekta au La Kisekta la Sheria yaani *Legal and Judicial Affairs Council* la Baraza la Mawaziri la Jumuiya la Afrika Mashariki kushindwa kufanya kazi sawa sawa.

Mheshimiwa Spika, katika Mkataba wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, kama tunavyofahamu, kuna Baraza la Kisekta la Sheria ambalo nimelitaja. Wajumbe wa Baraza hili ni Mawaziri na kama nilivyoeleza awali wakati katika nchi zingine Mwanasheria Mkuu anatambulika kama Waziri kwa nchi wanachama ikiwemo nchi yetu. Katiba haimtambui *Attorney General* au Mwanasheria Mkuu kama Waziri. Kwa hiyo basi, siku zote kama vikao vya Baraza hili la Sheria la Kisekta vikihudhuriwa na Mwanasheria Mkuu peke yake bila ya Waziri basi akidi au *quorum* haitimii na maamuzi ya kikao hicho hayatambuliki kisheria.

Mheshimiwa Spika, chimbuko la leo kwa kweli linatokana na kupanuka kwa Jumuiya yenyewe; uzoefu uliopatikana katika kipindi hiki cha miaka karibuni tisa ya Jumuiya; na uamuzi wa Wakuu wa nchi za Afrika Mashariki kwenye tamko lao yaani *Community* la Mkutano Maalum wa kilele wa Wakuu wa Nchi yaani *Summit* uliofanyika Mjini Arusha tarehe 20 mwezi wa nane mwaka 2007.

Mheshimiwa Spika, Wakuu wa nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki, katika Mkutano huo maalum, uliofanyika Mjini Arusha tarehe 20 mwezi wa nane mwaka 2007, kama nilivyosema awali, walitoa tamko yaani *Communique* na kutia saini makubaliano ambapo pamoja na mambo mengine waliidhinisha mapendekezo ya Baraza la Mawaziri wa Jumuiya ya Afrika Mashariki kuhusu kufanya marekebisho kwenye Mkataba wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, kwa mujibu wa Kifungu au Ibara ya 150 ya Mkataba ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, Kifungu kinachotoa mwongozo wa kufanya marekebisho pindi panapotokea sababu za kufanya hivyo.

Mheshimiwa Spika, Marekebisho ya Mkataba uliyoanzisha Jumuiya ya Afrika Mashariki, yanahusisha vifungu vya 1, 13, 17, 19, 48, 62 na 65 vya Mkataba. Aidha, Napenda niseme pamoja na vifungu vyote hivi, marekebisho haya yamelenga au yanahusu maeneo makuu yafuatayo:-

(i) Kutambuliwa kwa Mwanasheria Mkuu kama Mjumbe halali wa Baraza la Mawaziri. Marekebisho yanafanyika au yamefanyika ili kumwezesha Mwanasheria Mkuu kushiriki kwenye vikao vya Baraza la Mawaziri wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

(ii) Idadi ya Wajumbe wa Bunge la Afrika Mashariki. Marekebisho yamefanyika ili kuruhusu wakati wowote ule nchi mwanachama au wanachama wapya kuweza kufanya uchaguzi na kupeleka wawakilishi wao kwenye Bunge la Afrika Mashariki.

(iii) Eneo ambalo pia ni kubwa linahusu Naibu Mawaziri kuruhusiwa kuhudhuria vikao vya Bunge la Afrika Mashariki wakati Mawaziri wenye dhamana hawapo. Hivyo basi, marekebisho yamefanyika ili kuwawezesha Manaibu Mawaziri kuhudhuria vikao vya Bunge la Afrika Mashariki kwa niaba ya Mawaziri wenye dhamana.

Mheshimiwa Spika, nataka sasa nipitie kwa ujumla maeneo mengine yaliyorekebishwa au katika ujumla wake maeneo ambayo yamerekebishwa na vifungu husika ambavyo nimevitaja.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha kwanza, kinahusu tafsiri au *interpretation.* Kifungu hiki kinahusu tafsiri ya Mwanasheria Mkuu au kama ilivyowekwa kwa lugha ya Kiingereza *Attorney General, means the Attorney General of the Partner State,* kwa hali ilivyo sasa. Marekebisho yanafanywa kuwa na tafsiri ya Mwanasheria Mkuu kwenye Mkataba.

Kifungu cha 13, kinahusu uanachama katika Baraza la Mawaziri yaani *Membership of the Council* na katika hali ya sasa wanatajwa kwamba wanachama ni wale Mawaziri wanaohusika na masuala ya ushirikiano wa Afrika Mashariki kadri nchi wanachama zinavyoona inafaa. Sasa marekebisho yanafanywa ili isomeke kama kwamba ni Waziri mwenye dhamana ya shughuli za Afrika Mashariki wa kila nchi mwanachama na pia Waziri mwingine yeyote yule ambaye nchi mwanachama itaona inafaa na pia Mwanasheria Mkuu.

Mheshimiwa Spika kwa Kiingereza, marekebisho haya yanasema kwamba *The Council shall consist of:-*

*(a) The Minister responsible for East African Community Affairs of each Partner State;*
*(b) Such as the Minister's of the Partner State as each Partner State may determine; and*

*(c) The Attorney General of each Partner State.*

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 17, kinahusu Kamati ya Uratibu au *Composition of Coordination Committee.* Hii ni Kamati ya Makatibu Wakuu kama ilivyo hivi sasa, ni Kamati ya Makatibu Wakuu wanaohusika na Ushirikiano wa Afrika Mashariki. Marekebisho haya madogo yamefanywa ili kusema kwamba Makatibu Wakuu hawa au Kamati hii ni ya Makatibu Wakuu wanaohusika au Makatibu Wakuu wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 19, kinahusu pia hawa hawa Makatibu Wakuu na marekebisho yake yanafanywa kama ambavyo nimesema awali kwamba katika mkataba huu kinachofanywa ni kwamba badala ya kutaja *Permanent Secretary responsible for Regional Corporation* nasema *Permanent Secretary responsible for East African Community Affairs in each partner State.*

Mheshimiwa Spika, marekebisho makubwa ambayo niliyasema huko nyuma wakati nawasilisha, yanahusu kifungu cha 48 kinachohusu uanachama au Wabunge wa Bunge la Afrika Mashariki.

Kama nilivyosema awali, hivi sasa Mkataba wa Jumuiya ya Afrika Mashariki unataja bayana kwamba Wabunge wa kuchaguliwa ni 27 tu pamoja na hao kuna Wabunge ambao sio wa kuchaguliwa na kama inavyosema:-

*"The Members of the Assembly shall be 27 elected Members, and five Ex-Official Members, consisting one Minister's responsible for Regional Corporation from each Partner State and two Secretary General and Council to the Community.*

Mheshimiwa Spika, marekebisho yanafanywa ili kisomeke ifuatavyo:-

(a) *Membership of the Assembly shall comprise of,* yaani Bunge hili Wabunge wake watakuwa Wabunge 9 wa kuchaguliwa kutoka kila nchi; na
(b) Wale Wabunge ambao wanaingia kwa nyadhifa zao yaani *Ex-Official Members* ambao kwanza ni Mawaziri wenye dhamana ya masuala ya Afrika Mashariki kutoka nchi wanachama. Kwa lugha nyingine unaweza kusema ni Mawaziri Wadogo yaani *Assistant Ministers* na *Deputy Ministers* au Naibu Mawaziri na Mawaziri wa Nchi.

Mheshimiwa Spika, kwa Kiingereza ni kwamba marekebisho haya yanafanywa katika kifungu cha 48 kama ifuatavyo:-

(a) *Membership of the Assembly shall comprise of 9 Members elected of each Partner State; and*

*(b) Ex-Official Members consisting of one the Minister responsible for East African Community Affairs from each Partner State. Assistant Minister or Deputy Minister or Minister of State responsible for East African Community Affairs from each Partner State provided that an Assistant Minister, Deputy Minister or Minister of State may only participate in the meetings of the Assembly when the substantive Minister responsible for East African Community Affairs is for any reason unable to participate; and*

*(c) Secretary General and Counsel to the Community.*

Mheshimiwa Spika, kama ambavyo nimesema wakati nawasilisha, tunatofautiana katika miundo ya kiutawala ambapo katika baadhi ya nchi wanachama hawatumii neno Naibu Waziri wanatumia neno la Waziri Mdogo au *Assistant Minister* ambapo katika baadhi ya nchi wanachama tunatumia Naibu Waziri na pia katika nchi zote karibuni kuna Mawaziri wa Nchi. Kwa hiyo, marekebisho haya yamefanywa ili kuwawezesha Waheshimiwa Naibu Mawaziri au Mawaziri Wadogo au Mawaziri wa Nchi, inategemea na nchi ambayo wanatoka kuweza kushiriki katika masuala ya Bunge la Bunge la Afrika Mashariki kwa kuingia ndani ya Ukumbi wakati Mawaziri wenye dhamana hawapo.

Mheshimiwa Spika, hali ilivyo hivi sasa tofauti na Bunge letu hapa la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Naibu Mawaziri au Mawaziri Wadogo wao hawaingii kwenye Ukumbi wa Bunge na kushiriki katika Bunge. Kwa hiyo, marekebisho haya yamefanywa ili kuondoa hali hii ambayo kwa kweli haileti tija sana.

Mheshimiwa Spika, pia katika kifungu cha 62, pamefanywa marekebisho na labda niseme kwamba kwa hali ilivyo hivi sasa Muswada wa Sheria ukipitishwa basi unasomwa kama ifuatavyo:-

*"Enacted by the East African Community and be assented to by the President of the United Republic of Tanzania, The President of the Republic of Kenya and the President of the Republic of Uganda".*

Mheshimiwa Spika, hii ina maana kwamba imetiwa saini na kuridhiwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Rais wa Jamhuri ya Kenya na Rais wa Jamhuri ya Uganda na yaani zile nchi zimetajwa na Marais wetu wametajwa kwa nchi zile tatu na maana yake ni kwamba panapokuwa na idadi kubwa zaidi ya wanachama zaidi ya nchi zile tatu sasa haiwezekani kuwaruhusu wale wanachama wapya, Marais wao kuweza kutia saini Miswada ya Sheria ile.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, marekebisho yanafanywa ili isomeke kama ifuatavyo:-

*Enacted by the East African Community and assented to by the Heads of State".*

Mheshimiwa Spika, hii inamaanisha kwamba imetiwa saini na kuridhiwa na Wakuu wa Nchi zile za Jumuiya ya Afrika Mashariki. Kwa hiyo, ikiwa ni watatu sawa, ikiwa ni watano sawa, ikiwa Jumuiya itapanuka zaidi ya watano sawa ili isilazimishwe tena kufanya marekebisho kama haya.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 65, ni marekebisho yale yale kama ambavyo yamefanywa kwenye Makatibu Wakuu pia kwenye upande wa Mawaziri msisitizo umekuwa katika kusema kwamba hawa ni Mawaziri wa Jumuiya ya Afrika Mashariki au masuala ya Jumuiya ya Afrika ya Mashariki na siyo Mawaziri wa Ushirikiano wa Kikanda yaani *Regional Corporation.* Hili linatokana na tamko la Wakuu wa Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki kwamba msisitizo na mkazo uwekwe katika Jumuiya ya Afrika Mashariki na wala si Kanda. Kwa hiyo, Mkataba umefanyiwa marekebisho katika sehemu nyingi kuhakikisha kwamba kunakuwa na maneno ambayo yanaendana na maamuzi na matamko ya Wakuu wa nchi zetu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kueleza na kutoa ufafanuzi wa maeneo ambayo yanatakiwa au yamefanyiwa marekebisho na yameletwa mbele ya Bunge lako ili Bunge liliridhie marekebisho haya, naomba sasa kusoma Azimio la Bunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Azimio la Bunge la Kuridhia Marekebisho ya Mkataba wa Kuanzisha Jumuiya ya Afrika Mashariki.

**KWA KUWA**, Viongozi Wakuu wa Jumuiya ya Afrika Mashariki waliingia Mkataba wa Marekebisho ya Mkataba wa Kuanzisha Jumuiya ya Afrika Mashariki katika Mkutano wa Kilele uliofanyika tarehe 20 Agosti, 2007, Jijini Arusha;

**NA KWA KUWA**, Ibara ya 150 ya Mkataba wa Jumuiya ya Afrika Mashariki inatoa mwongozo wa namna ya kufanya marekebisho katika mkataba huo pindi kunapotokea sababu za msingi kufanya hivyo;

**NA KWA KUWA**, zimekuwepo sababu za msingi zinazolazimu kufanya marekebisho katika mkataba wa kuanzisha Jumuiya ya Afrika Mashariki ili:-

(a) Kuwezesha mwanachama mpya, wanachama wapya wa Jumuiya ya Afrika Mashariki kushiriki kikamilifu katika Jumuiya;

(b) Kuwezesha Naibu Waziri, Waziri Mdogo au Waziri wa Nchi wanachama kuwa Mjumbe wa Bunge la Afrika Mashariki endapo Waziri mwenye dhamana ya masuala ya Afrika Mashariki hatakuwepo; na

(c) Kuwezesha Mwanasheria Mkuu wa Serikali wa nchi Mwanachama kuwa Mjumbe katika vikao vya Baraza la Mawaziri wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

**NA KWA KUWA**, taratibu za kisheria za Kimataifa zinasisitiza umuhimu wa nchi Mwanachama wa Mkataba wowote wa Kimataifa kuzingatia na kuheshimu masharti ya Mkataba huo;

**NA KWA KUWA**, nchi yetu inayo wajibu kama ilivyo kwa nchi nyingine duniani kuzingatia na kuheshimu Mikataba ya Kimataifa ambayo Jamhuri ya Muungano imefanya ikiwa ni pamoja na Mkataba wa kuanzisha Jumuiya ya Afrika ya Mashariki wa mwaka 1999;

**NA KWA KUWA** hatua mojawapo ya kuzingatia na kuheshimu Mkataba wowote wa Kimataifa ni kwa Bunge la Jamhuri ya Muungano kuridhia Mikataba hiyo;

**HIVYO BASI,** kwa kuzingatia umuhimu na manufaa ambayo Tanzania itapata ikiwa ni sehemu ya nchi mwanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na kwa mujibu wa Ibara ya 150(6) ya Mkataba wa Kuanzisha Jumuiya ya Afrika Mashariki wa mwaka 1999 na Ibara ya 63(3)(e) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, Sura ya Pili, Bunge hili katika Mkutano wa Tisa, sasa linaazimia kuridhia Marekebisho ya Mkataba wa Kuanzisha Jumuiya ya Afrika Mashariki, mwaka 2007 (*Amendment of the Treaty for the Establishment of the East African Community, 2007).*

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja ya kuliomba Bunge lako kuridhia.

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MHE. MOHAMED R. ABDALLAH (K.n.y. MHE. ANNA M. ABDALLAH - MWENYEKITI WA KAMATI YA MAMBO YA NJE):** Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha maoni ya Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje kuhusu Azimio la Bunge la Kuridhia Marekebisho ya Mkataba wa Kuanzisha Jumuiya ya Afrika Mashariki, mwaka 2007 (*Amendment of the Treaty for the Establishment of the East African Community, 2007).*

Mheshimiwa Spika, kabla sijawasilisha maoni haya, kwa niaba ya Kamati, naomba kutoa salamu za rambirambi kwako binafsi, Bunge hili, wananchi wa Mkoa wa Kilimanjaro na Taifa kwa ujumla, kwa kuondokewa na mpendwa wetu Mheshimiwa Salome Joseph Mbatia ambaye alikuwa Naibu Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto. Ndugu yetu huyu alikuwa mzalendo na mchapakazi na mauti yake yamemfika akiwa katika ujenzi wa Taifa hili. Namwomba Mwenyezi Mungu ailaze roho ya marehemu mahali pema peponi, amen.

Aidha, kwa niaba ya Kamati, naomba kutoa salamu za pole kwa Mheshimiwa Mudhihir Mohamed Mudhihir, Mbunge wa Mchinga, Mheshimiwa Profesa Juma Kapuya, Mbunge wa Urambo Magharibi na Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa na Mheshimiwa Zaynab Matitu Vulu, Mbunge wa Viti Maalum kwa kupata ajali mbaya kwa mwaka huu wa 2007.

Mheshimiwa Spika, baada ya salamu za pole, pia kwa niaba ya Kamati yangu, napenda kutoa pongezi zangu za dhati kwa Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kuchaguliwa kwa kishindo kuwa Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi, ngazi ya Taifa. Aidha, nawapongeza Waheshimiwa Wabunge na wana CCM wengine kwa kushinda katika nyadhifa mbalimbali katika Chama cha Mapinduzi. Nawatakia mafanikio mema katika kukijenga Chama chetu na Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, baada ya salamu hizo napenda kuwashukuru Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje, kwa kunipa heshima ya kuwasilisha maoni ya haya mbele ya Bunge lako Tukufu. Kwa heshima na taadhima, naomba niwatambue kwa kuwataja majina kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Anna M. Abdallah, Mwenyekiti, Mheshimiwa Mussa H. Zungu, Makamu Mwenyekiti. Wajumbe ni Mheshimiwa Ame Pandu Ame, Mheshimiwa Balozi Hamisi S. Kagasheki, Mheshimiwa Teddy L.Kasella-Bantu, Mheshimiwa Yono S. Kevela, Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa na Mheshimiwa Hassan C. Kigwalilo. *(Makofi)*

Wajumbe wengine ni Mheshimiwa Juma H. Killimbah, Mheshimiwa Ali Ameir Mohamed, Mheshimiwa Mhonga S. Ruhwanya, Mheshimiwa Beatrice M. Shellukindo, Mheshimiwa John M. Shibuda, Mheshimiwa Zaynab M. Vulu, Mheshimiwa Dr. James M. Wanyancha, Mheshimiwa Abubakar Khamis Bakary, Mheshimiwa Mohammed G.

Dewji, Mheshimiwa Dr. Zainab A. Gama, Mheshimiwa Balozi Abdi H.Mshangama, Mheshimiwa Mudhihir M. Mudhihir na mwisho mimi mwenyewe Mohamed R. Abdallah. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kamati ilielezwa umuhimu wa kufanyia marekebisho Mkataba ulioanzisha Jumuiya ya Afrika Mashariki kutokana na mapungufu yake kuonekana baada ya kuanza utekelezaji wake.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya mambo muhimu yanayohitajika katika kuboresha mkataba huo ni:-

(1) Kuwezesha nchi ambayo si mwanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki kuweza kujiunga na kushiriki kikamilifu katika Jumuiya;

(2) Kuwezesha Naibu Waziri, Waziri Mdogo au Waziri wa Nchi wanachama kuwa mjumbe endapo Waziri mwenye dhamana ya masuala ya Afrika Mashariki hatakuwepo; na

(3) Kumwezesha Mwanasheria Mkuu wa Serikali wa nchi mwanachama kuwa mjumbe katika Kikao cha Baraza la Mawaziri la Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Spika, maoni na ushauri wa Kamati, baada ya kujadili Azimio hili kwa kina, Kamati inatoa maoni na ushauri ufuatao:-

(1) Kila nchi mwanachama iwe na idadi inayolingana katika vikao mbalimbali vya maamuzi katika Jumuiya ili kuwepo na usawa katika maamuzi yanayofikiwa.

(2) Pamoja na kwamba mkataba haujainishwa ukomo katika idadi ya nchi zitakazoomba kujiunga na Jumuiya, ni vema mkataba ukataja ukomo katika idadi ya nchi zinazoweza kujiunga na Jumuiya hii kwa kuwa inaweza kupoteza maana ya kuitwa Jumuiya ya Afrika Mashariki ikiwemo kushindwa kukabiliana na changamoto zinazoweza kujitokeza kutokana na ukubwa wa Jumuiya.

(3) Ili kuondoa utata katika uchaguzi wa Wabunge wa Bunge la Jumuiya ya Afrika Mashariki, ni vema zitungwe sheria na taratibu zitakazofuatwa na nchi zote wanachama kwa lengo la kupunguza uwezekano wa nchi moja mwanachama kuweka pingamizi katika utekelezaji wa shughuli za Bunge la Afrika Mashariki kama ilivyotokea hivi karibuni.

Mheshimiwa Spika, mwisho, kwa mara nyingine, naomba kuwapongeza Wakuu wa nchi Wanachama kwa busara na hekima, kwa kuona umuhimu wa marekebisho haya kwa manufaa ya nchi za Jumuiya kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, naomba kumpongeza Mheshimiwa Dr. Ibrahim Msabaha, Mbunge, Waziri wa Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Naibu Waziri Mheshimiwa Dr. Diodorus B. Kamala, Mbunge, Katibu Mkuu, Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Maofisa wengine kwa kuwasilisha Azimio hili mbele ya Kamati kwa ufanisi mkubwa.

Mheshimiwa Spika, baada ya maoni hayo, Kamati katika ujumla wake haina pingamizi juu ya kuridhiwa kwa Azimio hili na inaliomba Bunge lako Tukufu likubali kuridhia Azimio hili kwa manufaa ya Jumuiya ya Afrika ya Mashariki.

Mheshimiwa Spika napenda kuwashukuru tena wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje, kwa maoni na ushauri waliotoa kwa maslahi ya nchi yetu na Jumuiya ya Afrika ya Mashariki kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, baada ya maoni haya, Kamati inaunga mkono hoja na naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MHE. ABUBAKAR KHAMIS BAKARY – MSEMAJI WA KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili nami niweze kutoa au kuwasilisha maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu Azimio la Bunge la Kuridhia Mkataba wa Marekebisho ya Mkataba wa Kuanzisha Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Spika, naomba kwanza nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kutujalia sote kuwa wazima na wenye afya.

Pili, nichukue nafasi hii kwa kuwapa pole wale wenzetu wote waliopatwa na ajali mbalimbali na hususani familia za wale ambao watu wao wamepoteza maisha yao. Mwenyezi Mungu azipumzishe roho zao mahali pema peponi, amen. Kwa wale waliokuwa wagonjwa basi Mwenyezi Mungu awajalie wapone haraka.

Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii vilevile kutoa pole kwa kiongozi wetu wa Upinzani, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed na kumwombea Mwenyezi Mungu apate nafuu haraka iwezekanavyo.

Mheshimiwa Spika, sote tunajua kwamba mnamo tarehe 20 Agosti mwaka 2007, Viongozi Wakuu wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, walikubaliana kwa pamoja kuufanyia marekebisho mkataba wa kuanzisha Jumuiya hiyo katika Ibara zake za 1, 13, 17, 19, 48, 62 na 65. Madhumuni yao ilikuwa ni kuufafanua zaidi katika baadhi ya maeneo na tafsiri zao kama vile tafsiri ya Mwanansheria Mkuu, Ibara ya kwanza na kuhusu maelezo zaidi ya Ibara ya 62 kuhusu uwekaji wa saini na kukubalika kwa sheria zinazotungwa na Bunge la Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Spika, pili, ni kuwawezesha Wanasheria Wakuu ambao hawana hadhi ya Uwaziri, kama vile Mwanasheria Mkuu wa Kenya na Mwanasheria Mkuu wa Tanzania kuwa pia ni wajumbe wa Baraza la Mawaziri la Afrika Mashariki kama Ibara ya 13 ya Mkataba inavyotaka.

Mheshimiwa Spika, tatu, ni kuwawezesha, chini ya Ibara ya 48 ya mkataba huu, nchi za Rwanda na Burundi ambazo zimejiunga hivi karibuni na Jumuiya hii kufanya uchaguzi wa Wabunge wao watakaoingia katika Bunge la Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Spika, nne, ni kuwawezesha pia Naibu Mawaziri au Waziri wa nchi mwenye dhamana ya Afrika Mashariki ambao hapo zamani walikuwa hawawezi kushiriki vikao vya Bunge la Afrika Mashariki, sasa waweze kushiriki pale ambapo Waziri mwenye dhamana ya Afrika Mashariki hayupo.

Mheshimiwa Spika, tano, kuwa na jina linalobainisha kuwa Taasisi inayotajwa inahusika na masula ya Afrika Mashariki kama Ibara ya 19 na 65 inavyotaka.

Mheshimiwa Spika, masuala haya yanayolenga kurekebisha Mkataba wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, ni muhimu kwa kuhamasisha zaidi wanachama wapya wanaoingia na pia kwa kuimarisha utendaji mzuri katika Taasisi za Jumuiya hiyo. Hivyo ni lazima na muhimu marekebisho haya yafanywe ili shughuli za Jumuiya ziweze kutendeka ipasavyo na kwa ufasaha zaidi.

Mheshimiwa Spika, zaidi ya hayo, ni kuwa Waheshimiwa Wakuu wa nchi hizi za Jumuiya wamesharidhia marekebisho hayo yafanywe.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani baada ya kutafakari yote hayo na baada ya kuona umuhimu na ulazima wa marekebisho hayo kwa ajili ya kuimarisha Jumuiya na vilevile kuwapa fursa wenzetu wanachama wapya katika Jumuiya hii ili nao waweze kushiriki kikamilifu katika shughuli za Jumuiya, basi tunakubali na kuridhia kuwa Bunge hili Tukufu liridhie kufanyika kwa mabadiliko hayo kama Ibara ya 63(3)(e) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano inavyoelekeza.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuyasema hayo, kwa niaba ya Kambi ya Upinzani naomba kuwasilisha, ahsanteni sana. *(Makofi)*

**MHE. YONO S. KEVELA:** Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii kukushukuru sana kwa kuwa mchangiaji wa kwanza katika Azimio la Bunge la Kuridhia Mkataba wa Marekebisho ya Mkataba wa Kuanzisha Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Spika, lakini kabla sijaanza kuchangia, nichukue nafasi hii kwanza kuwashukuru sana Wabunge wenzangu na viongozi mbalimbali wa Chama na Serikali katika ngazi ya Wilaya, Mkoa na Taifa kwa ujumla kwa jinsi walivyotoa msaada mkubwa katika msiba wangu mkubwa uliotokea wa kufiwa na watoto wangu wawili, ukweli nawashukuru sana.

Mheshimiwa Spika, pia napenda kutoa pole kwa kuondokewa na Naibu Waziri, Mheshimiwa Salome Mbatia. Kwa kweli msiba huu uliotupata kwa kweli ulikuwa ni

mkubwa sana. Nakumbuka sio siku nyingi kabla ya tukio la msiba wa mtoto wangu alikuja pale nyumbani kutoa ubani, akanifariji, baada ya siku mbili nikasikia na mwenzangu tena tatizo hilo limemtokea. Kwa kweli natoa pole sana kwa familia ya wahusika na Taifa kwa ujumla, kwa kweli nilishtuka sana sana Mungu aiweke roho yake mahali pema peponi, amen.

Mheshimiwa Spika, lakini mbali ya hapo, nichukue nafasi hii vile vile kutoa pole kwa Wabunge wenzangu ambao wamepata matatizo ya ajali mbalimbali, hasa ndugu yangu Mudhihir na wengine wote ambao siwezi kuwataja mmoja kwa mmoja. Kwa mfano Mheshimiwa Vulu, naye amepata matatizo, ni Mwanakamati mwenzetu, kwa kweli nawapa pole sana.

Mheshimiwa Spika, lingine ni suala la pongezi, nataka nitoe pongezi kwa Chama cha Mapinduzi kwa jinsi kilivyofanya mchakato na kupata viongozi katika ngazi ya *NEC* na kupata Kamati Kuu. Kwa kweli natoa pongezi kwa Mwenyekiti wetu wa Kitaifa, Katibu Mkuu na viongozi mbalimbali ambao kwa kweli wamepita katika mchakato sio mdogo ulikuwa mzito, kwa kweli nawapongeza sana.

Mheshimiwa Spika, niingie kwenye hoja ya kuchangia Azimio la Bunge la Kuridhia Mkataba wa Marekebisho ya Mkataba wa Kuanzisha Jumuiya ya Afrika Masharikiuanzishwaji wa Afrika Mashariki. Hoja hii ni muhimu sana. Mimi bahati nzuri ni Mjumbe wa Kamati ya Mambo ya Nje na Wizara hii inanihusu, uridhiaji wa mkataba huu ni muhimu sana. Toka Jumuiya hii ivunjike mwaka 1977 ni kipindi kirefu hatuijafufua.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu ni kwamba, zile sababu ambazo zilisababisha kuvunjika kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki mwaka 1977, inatakiwa tuziangalie kwa makini sana isije kuwa tunaanzisha kitu kizuri yakatokea yale yale ya mwaka 1977, ikavunjika tena. Kwa hiyo, maadamu huu umoja tunauanzisha kwa lengo zuri la kijamii, kisiasa na kiuchumi, ni vizuri tuwe waangalifu sana.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kwamba wengine wanasema tusiingize nchi nyingi, kwa sisi watu ambao tuko Kusini tunapenda huu umoja ukishaanza na wenzetu kama wa Malawi, Msumbiji na Zambia wakijiunga, ingekuwa ni kitu kizuri sana. Hata hivyo, kwa sababu ni Kaskazini wenzetu Uganda, Kenya, Burundi na Rwanda ndio tuko pamoja nilikuwa na hofu kwamba pengine maendeleo yasije yakawa Kaskazini sisi wa Kusini tukasahaulika kama ilivyokuwa kwa Darfur. Kwa hiyo, nashauri ni vizuri umoja huu tukishauanzisha na nchi nyingine hizi za Kusini kama Msumbiji, Zambia, Malawi, tuzikaribishe kwa sababu na sisi tuko huko huko mipakani ingetusaidia sana kuinua hali ya huku Kusini kwa sababu hii *Mtwara Corridor* imeanzishwa kwa sababu ya hiyo hiyo kwamba Mikoa ya Kusini mara nyingi huwa inasahauliwa.

Mheshimiwa Spika, lingine nataka nichangie kuhusu suala la jinsi Manaibu Mawaziri na huyu Mwanasheria Mkuu kuhusika kwenye ujumbe, ni kitu muhimu sana kwa sababu na mimi nilikuwa nashiriki, hawa watu ni muhimu kushiriki. Kwa hiyo,

naunga mkono hoja hii moja kwa moja kwamba mapendekezo yaliyotolewa ni mapendekezo ya msingi, kwa hiyo, sioni kama kuna sehemu ya kurekebisha hapo.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu ni mchangiaji wa kwanza, nategemea labda nitakuwa mchangiaji wa mwisho ili nijiandae vizuri, naona nikitoa hoja nyingine, itakuwa sio nzuri zaidi bora niachie Wabunge wenzangu wachangie.

Mheshimiwa Spika, kwa haya machache, nakushukuru sana na pia nawashukuru Wabunge wenzangu kwa kunisikiliza, ahsanteni sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Kevela. Napenda kuungana na wote kurudia tena kukupa salamu zangu za rambirambi kwa matatizo yaliyokukuta. Naungana na Wabunge wote kuendelea kukupa pole na nikuhakikishie kwamba tunakukumbuka katika sala zetu na dua zetu, ahsante sana.

**WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Spika, napenda nichukue nafasi hii, kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia na hususan Mheshimiwa Mohamed Rished Abdallah, ambaye amesoma kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati, Mheshimiwa Abubakar Khamis, kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, na Mheshimiwa Yono Stanley Kevela.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mohamed Rished Abdallah, kwa niaba ya Kamati amezungumzia umuhimu wa nchi wanachama kuwa na idadi sawa kwenye ujumbe au *delegation* inayokwenda kwenye vikao vya Afrika Mashariki ili kulinda maslahi ya wanachama panapofanywa maamuzi basi maamuzi hayo yafanywe katika hali ya usawa.

Mheshimiwa Spika, tumelipokea hili, lakini napenda nimuhakikishie Mheshimiwa Mohamed Rished Abdallah na Waheshimiwa Wabunge na wananchi kwa ujumla kwamba mfumo wa kufanya maamuzi katika Jumuiya ya Afrika Mashariki hairuhusu nchi yenye idadi kubwa ya wajumbe yaani *delegation* kuwa ndio kigezo cha wao kuweza kushinda katika maamuzi. Kwa maana nyingine, mfumo wa maamuzi katika Jumuiya ya Afrika ya Mashariki sio wa kupiga kura bali ni ule mfumo wa maridhiano kwa wote kwa Kiingereza wanasema *decision making by consensus.* Kila nchi ni lazima ikubaliane na jambo linalofanyiwa maamuzi. Nadhani mfumo huu ni mzuri kwa kulinda maslahi ya nchi wanachama.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, pamoja na ushauri ambao Mheshimiwa Mohamed Rished Abdallah ameutoa lakini naomba asiwe na hofu yeye au Waheshimiwa Wabunge au wananchi kwa ujumla kwamba ule mfumo wenyewe unalinda maslahi ya wanachama. Kama jambo likianza kwa mujibu wa mkataba nchi moja ikatoa msimamo kwamba wao hawakubaliani na msimamo huo au na jambo hilo, lile jambo ndio linakuwa limekwisha pale mpaka muunde nguvu ya kuwashawishi mpaka wakubali. Nadhani hili ni jambo zuri na hasa kwenye Jumuiya yetu ambayo tumepita kwenye matatizo mengi kwenye Jumuiya ya zamani na sasa tunaianzisha upya.

Mheshimiwa Spika, jambo ambalo Mheshimiwa Mohamed Rished Abdallah, amelizungumzia ni ukomo wa wanachama. Tumelipokea hili. Niseme tu, kwa mujibu wa Mkataba wa Afrika ya Mashariki, unaruhusu wanachama wapya kujiunga kama wanakubaliana na malengo na kama watapita kwenye mchakato wa usaili wa kuhakikisha kwamba wanatimiza vigezo ambavyo vinawekwa au vimewekwa na Jumuiya. Lakini la msingi zaidi ni kwamba lazima wawe wamepakana kijiografia na moja ya nchi wanachama wa sasa. Sasa hilo, kwa maana nyingine unaweza ukasema tunaweza tukajikuta Jumuiya imechukua Bara zima la Afrika. Kama itatokea hivyo, hakuna ubaya kwa sababu kama mnavyofahamu siku zote sera zetu, misimamo yetu imekuwa kupigania Umoja wa Bara la Afrika na nchi hii inatambulika Kimataifa kwenye nyanja hiyo.

Mheshimiwa Spika, lakini kwa sasa kama nilivyosema, utaratibu wa kujiunga ni huo. Kama nilivyosema awali hata sisi waanzilishi wa Jumuiya hii tunaelewa kwamba lengo kuu zaidi ni kupata umoja wa nchi zote za Afrika lakini tutapataje umoja huu, ni kwa hatua kwa hatua, *stage by stage* na muungano huu wa Jumuiya ya Afrika Mashariki ni moja ya mifano ya Umoja wa Kanda ambao hatimaye tunaamini nchi zote za Afrika zinaweza zikaja pamoja na kuungana.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, labda niseme tu kwamba kwa mujibu wa historia yetu, sera zetu na misimamo yetu, si vibaya ikitokea nchi zingine zaidi zinazotaka kujiunga. Nimeelewa hofu iliyopo isije pakawa na wigo mkubwa mno, *management* yake ikawa kidogo ina matatizo lakini naamini viongozi wetu wanaweza kuhimili vishindo vya upanuzi wa aina hiyo. Lakini kwa sasa Jumuiya na taratibu zake za kujiunga na chama ni kama ambavyo nimezieleza.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mohamed Rished Abdallah, amezungumzia pia juu ya umuhimu wa kutunga sheria moja inayotoa mwelekeo na utaratibu mmoja wa namna ya kuchagua Wabunge wa Bunge la Afrika Mashariki. Kwa kweli msingi wa hoja yake hii nzito, ni dhahiri unatokana na matukio ya mwaka wa jana ambapo moja ya nchi mwanachama baadhi ya watu waliona kwamba uchaguzi haukufanyika nchini mwao walikwenda Mahakama ya Afrika ya Mashariki kutaka waliochaguliwa Ubunge kwenye nchi hiyo wasitambulike kama ni Wabunge na pia kuiomba Mahakama iseme pamoja na mambo mengine kwamba nchi ile mwanachama haikufanya uchaguzi kwa mujibu wa mkataba wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Spika, katika kesi ile maombi yote mawili yalipatikana. Kwanza palitokea zuio la kuwazuia Wabunge wale wasiapishwe na kwa maana nyingine Wabunge wote hawakuapishwa na tukakaa zaidi ya miezi 6 bila ya Bunge la Afrika Mashariki. Lakini la pili pia katika uamuzi wa mwisho wa Mahakama, Mahakama pia ilisema kwamba nchi ile mwanachama haikufanya uchaguzi kwa mujibu wa Mkataba wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Spika, hoja ya Mheshimiwa Mohamed Rished Abdallah, ni hoja muhimu sana. Labda niliarifu Bunge lako Tukufu kwamba hata katika Jumuiya yenyewe katika Baraza la Mawaziri upo mpango wa kuwasilisha Sheria au Rasimu au Muswada wa Sheria kwenye Bunge la Afrika Mashariki ili itungwe sheria inayozungumzia namna

gani basi uchaguzi unaohusu Wabunge wa Bunge la Afrika ya Mashariki ufanyike katika nchi wanachama. Kwa hiyo, nadhani hatua hiyo kama alivyosema Mheshimiwa Rished Abdallah, itakapofikiwa itaondoa uwezekano huu wa matatizo ambayo yametokea mwaka wa jana.

Mheshimiwa Spika, mchangiaji wa pili alikuwa Mheshimiwa Abubakar Khamis, mzungumzaji kwa niaba ya Kambi ya Upinzani. Napenda kumshukuru kwa kuunga mkono hoja hii ya Kuridhia Azimio la Marekebisho ya Mkataba wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Spika, mchangiaji wa tatu, ni Mheshimiwa Yono Stanley Kevela. Kwanza amezungumzia umuhimu wa Jumuiya katika dunia ya sasa na mimi napenda niungane naye kwa kusisitiza pia umuhimu wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na kwamba unapokuwa na Jumuiya kama Jumuiya ya Afrika ya Mashariki, hata baadhi ya mambo ambayo tunaweza kuyadhani ni ya ndani lakini yanahusisha pia wanachama wenzetu wa Jumuiya, kwa hiyo, nadhani kama alivyosema yeye, ni muhimu sana sote tuwe makini katika ushiriki wetu katika Jumuiya ya Afrika ya Mashariki. Ninakubaliana naye kwamba tusirudie makosa yaliyotokea katika Jumuiya ya zamani ambayo ilivunjika mwaka 1977. Pia amesema kwamba yeye angependa tukaribishe nchi nyingine ziwe wanachama, nimeeleza kwamba kimsingi Jumuiya ina utaratibu wa kuingiza wanachama wapya.

Mheshimiwa Spika, napenda basi nichukue nafasi hii, kuwashukuru tena Waheshimiwa watatu wote hawa ambao wamechangia ambao ni Mheshimiwa Mohamed Rished Abdallah, Mheshimiwa Abubakar Khamis na Mheshimiwa Yono Stanley Kevela, kwa kuunga mkono hoja ambayo nimeleta mbele ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, nawaomba tena Waheshimiwa Wabunge, wakubaliane nami katika kupitisha Azimio hili la Kurekebisha Mkataba wa Jumuiya ya Afrika ya Mashariki.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Azimio la Bunge la Kuridhia Mkataba wa Marekebisho ya Mkataba wa Kuanzisha Jumuiya ya Afrika Mashariki lilipitishwa na Bunge)*

## TAARIFA YA KAMATI

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO – MWENYEKITI WA KAMATI YA UWEKEZAJI NA BIASHARA:** Mheshimiwa Spika, kwanza, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili kuweza kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Uwekezaji na Biashara ya mwaka 2006.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 88(11) ya Kanuni za Bunge, Toleo la 2004, naomba kwa niaba ya Wajumbe wenzangu wa Kamati ya Uwekezaji na

Biashara, nitoe taarifa kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Kamati kwa kipindi cha mwaka mmoja uliopita wa 2006.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa hii ni taarifa ya kwanza ya mwaka mzima ya Kamati ya Uwekezaji na Biashara, nawajibika kunukuu majukumu yake kama yalivyoainishwa katika Kanuni ya 95(1)(2) ya Kanuni za Bunge, Toleo la 2004.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni hiyo, Kamati ya Uwekezaji na Biashara inasimamia shughuli za Wizara mbili nazo ni Wizara ya Nishati na Madini na Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko.

Mheshimiwa Spika, majukumu ya Kamati katika Wizara hizo ni kushughulikia bajeti ya Wizara hizo, kushughulikia Miswada ya Sheria na Mikataba inayopendekezwa kuridhiwa na Bunge ambayo chanzo chake ni Wizara hizo, kushughulikia taarifa za kila mwaka za utendaji na Hesabu zilizokaguliwa za Mashirika ya Umma yaliyo chini ya Wizara hizo na kufuatilia utekelezaji unaofanywa na Wizara hizo kwa mujibu wa Sehemu ya Pili, Ibara ya 63(3)(b) ya Katiba. Ibara hiyo inatamka kama ifuatavyo na napenda kunukuu:-

"Bunge itakuwa ndicho chombo kikuu cha Jamhuri ya Muungano ambacho kitakuwa na madaraka, kwa niaba ya wananchi, kuisimamia na kuishauri Serikali ya Jamhuri ya Muungano na vyombo vyote katika utekelezaji wa majukumu yake kwa mujibu wa Katiba hii". Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Uwekezaji na Biashara, imetekeleza majukumu yake ya Kikatiba ya kuisimamia na kuishauri Serikali kama ifuatavyo:-

(i) Kamati imeshirikiana na Wizara zote kuelewa maeneo yote ya utekelezaji wa majukumu yake. Aidha, Kamati imepata fursa ya kushiriki katika semina na mikutano ya kuelimishwa juu ya majukumu ya Wizara hizo na vyombo chini ya Wizara hizo.

(ii) Kamati imeshiriki katika mchakato wa Bajeti za Wizara hizo za mwaka wa 2006/2007.

(iii) Kamati imepata fursa ya kutembelea maeneo ya utekelezaji wa Mashirika chini ya Wizara hizo na pia makampuni binafsi katika sekta ya Nishati, Madini, Viwanda, Biashara na Masoko.

(iv) Vilevile, Kamati imepata wasaa wa kushiriki katika Maonyesho ya Biashara ya Kimataifa katika Uwanja wa Maonyesho ya Kimataifa wa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere mwezi Julai, 2006.

(v) Kamati pia imepata nafasi kwa baadhi ya Wajumbe wake kushiriki katika ziara za mafunzo nje ya nchi, chini ya Wizara zinazosimamiwa na Kamati hii.

(vi) Fursa pia imetolewa na Wizara zote kwa baadhi ya Wajumbe wa Kamati hii kushiriki katika semina zinazohusu Wizara hizo ndani ya nchi.

(vii) Kamati vilevile imeshiriki katika mchakato wa kupitia Miswada ya Sheria ya Wizara hizo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu eneo la uwekezaji kwa ujumla, hapa tunapenda kueleza kuwa uwekezaji mkubwa nchini ambao unalenga kwenye uzalishaji bidhaa moja kwa moja uko katika maeneo ya madini, nishati na viwanda. Kwa hiyo, Kamati ilipata nafasi ya kutembelea maeneo yenye uwekezaji mkubwa au yanayoandaliwa kwa ajili ya uwekezaji kama vile maeneo ya miradi ya gesi asilia, maeneo ya makaa ya mawe na chuma, maeneo ya madini ya Tanzanite na kadhalika.

Kamati vilevile imepata nafasi ya kutembelea Mashirika ya Umma yaliyobinafsishwa na pia yale ambayo yanaandaliwa kubinafsishwa kuona jinsi mikataba inavyotekelezwa na hali ya utekelezaji wa shughuli za Mashirika hayo.

Aidha, Kamati imepata nafasi ya kutembelea wawekezaji wadogo wadogo wazalendo katika maeneo ya uchimbaji wa madini ya Tanzanite Mererani na uchimbaji wa chumvi, Mkoani Lindi, na kadhalika.

Kamati pia imepata nafasi ya kukutana na wawekezaji mbalimbali kutoka ndani na nje ya nchi hasa katika sekta ya madini na nishati na kupata maelezo ya nia zao za kuwekeza hapa nchini, mfano kwenye gesi asilia, makaa ya mawe na chuma, nishati ya kupikia kwa makaa ya mawe, nishati ya upepo au wind energy na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza majukumu ya kusimamia na kufuatilia utekelezaji wa shughuli zinazofanywa na Wizara pamoja na Taasisi, Mashirika na Asasi mbalimbali. Kamati imeweza kutekeleza majukumu hayo kwa kutoa maoni na ushauri katika sekta zake kama inavyofuata hapa chini:-

Mheshimiwa Spika, Kamati inatambua kwamba sekta ya nishati ni moja ya sekta muhimu sana katika maendeleo ya Taifa letu kwa kuwa utekelezaji wa shughuli nyingi unategemea sekta hii. Kwa mantiki hiyo, Kamati mara baada ya kutembelea maeneo mbalimbali yanayojihusisha na sekta hii, imeweza kutoa maoni na ushauri utakaoweza kuboresha sekta hii kama ifuatavyo:

Mheshimiwa Spika, kuhusu Shirika la Umeme Tanzania (*TANESCO*), Kamati imefarijika na hatua za dharura ambazo Serikali ilichukua nusu ya pili ya mwaka 2006 ili kuepusha nchi isikumbwe na janga la kukosa nishati ya umeme. Aidha, *TANESCO* iliingia mikataba na wawekezaji binafsi wa nje kuleta mitambo ya kuzalisha umeme wa dharura kwa kutumia gesi asilia na dizeli.

Mheshimiwa Spika, Kamati pia imeridhishwa na utendaji wa baadhi ya makampuni yaliyoitikia wito wa Serikali kwa haraka kama vile kampuni ya kuzalisha umeme ya Aggreko, ambayo ilianza uzalishaji umeme wa dharura bila kuchelewa, hivyo kusaidia mapema kuondoa kero na wasiwasi mkubwa uliozikumba sekta za viwanda, biashara na utoaji huduma nchini.

Mheshimiwa Spika, baada ya kufuatilia taarifa za Serikali na za Shirika la Umeme Tanzania *(TANESCO)*, Kamati haikuridhishwa na utendaji kazi wa Kampuni ya R*ichmond Development Corporation* ya Marekani na mrithi wake *Dowans Holdings S.A.* ya Falme za Nchi za Kiarabu *(UAE)* kwa kushindwa kukamilisha mradi wa umeme wa dharura katika muda muafaka, yaani ndani ya kipindi ambacho nchi ilikuwa inakabiliwa na tatizo la upungufu wa umeme. Kwa mujibu wa taarifa za Kamapuni ya *DOWANS*, ufungaji wa mitambo ya kuzalisha na kuingiza umeme wa megawati 100 kwenye gridi ya Taifa ulitegemewa kukamilika mwezi Juni, 2007, badala ya Februari 2, 2007 kama iliyosainiwa kwenye mkataba, miezi kadhaa baada ya hali ya dharura kumalizika.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa tunapowasilisha taarifa hii, *DOWANS* wamekamilisha kazi hiyo. Kwa mujibu wa Mkataba wa *Richmond/DOWANS* walitakiwa kuilipa *TANESCO* kiasi cha Dola za Marekani 10,000 kwa siku kutokana na uchelewashaji wa ufungaji wa mitambo ya umeme wa dharura. Kamati ingependa kufahamu ni kiasi gani cha fedha ambacho *TANESCO* imelipwa na *DOWANS* mpaka hivi sasa kwa mujibu wa mkataba.

Mheshimiwa Spika, utendaji kazi usioridhisha wa *Richmond* na ushahidi bayana uliojitokeza polepole wa kampuni hiyo kutokuwa na uwezo wa kutosha kifedha na kukosa kabisa uzoefu katika miradi ya umeme, umezua maswali mengi miongoni mwa wananchi kuhusu umakini uliotumika katika kuiteua kampuni hiyo kutekeleza mradi nyeti Kitaifa wa aina hiyo na wenye gharama kubwa wa Sh. Billioni 172.9.

Mheshimiwa Spika, viwingu vya mashaka vilivyotanda juu ya suala hili haviwezi kuondoka kwa kuvifumbia macho au kwa kuvipuuzia bali kwa kuvifanyia kazi kwa uwazi na ukweli ili kukidhi matakwa ya demokrasia na utawala bora. (*Makofi*)

Kamati imepata taarifa kupitia vyombo vya habari kwamba Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), imechukua hatua za kuchunguza uwepo wa rushwa katika zoezi zima lililopelekea *Richmond* kuteuliwa. Pamoja na uchunguzi huo wa TAKUKURU ulioliangalia suala hili kijinai, bado yako maswali ya msingi nje ya sheria ya jinai yanayohusu miiko, maadili na taratibu za kazi za Serikali, uadilifu, umakini na uwajibikaji katika utendaji kazi, ambayo hayakuangaliwa na yanadai majibu ya uhakika:-

(a) Je, ni sababu zipi za msingi zilizopelekea Serikali kuacha kuifanyia uchunguzi wa awali *(due diligence)* kampuni hiyo ya *Richmond* tofauti na kampuni

nyingine zilizoshiriki kwenye zabuni hiyo ili kujua uwezo wa kampuni hiyo kifedha, kitaalamu na kiutendaji?

(b) Njia mojawapo ya haraka ya kujua umakini na uhodari wa kampuni yoyote ile, ni kukagua tovuti yake. Je, Serikali ilipata fursa ya kuikagua tovuti ya kampuni hiyo ambayo ni *(http://www.rdevco.com/economy.html)?*

(c) Serikali ilikuwa na taarifa za kutosha kuhusu uwezo duni kiutendaji wa *Richmond* hasa baada ya kampuni hiyo kushindwa, bila sababu za msingi, kutekeleza mradi wa bomba la mafuta kutoka Dar-es-Salaam hadi Mwanza mwaka 2005 kinyume cha makubaliano *(Memorundum of Understanding)* kati ya Serikali na kampuni hiyo. Je, ni sababu zipi za msingi zilizoisukuma Serikali kuufumbia macho udhaifu wa *Richmond* uliojidhihirisha kwenye mradi mwingine mkubwa wa Kitaifa, yaani mradi wa bomba la mafuta?

(d) Taarifa za awali za Serikali zimeeleza kuwa madai ya *Richmond* kuwa na uhusiano wa karibu na kampuni yenye jina kubwa duniani ya *Pratt & Whitney*, ndiyo yaliyoishawishi Serikali kuipa *Richmond* ushindi kwenye zabuni hiyo. Je, Serikali ilipewa ushahidi wowote wa kimaandishi kuhusu uhusiano wa kisheria wa kampuni hizo mbili? Je, kwa nini basi mkataba wa mwisho wa kuzalisha umeme wa dharura nchini, haukuitaja wala kuihusisha kwa namna yoyote ile kampuni ya *Pratt & Whitney?*

(e) Serikali ilitaka kampuni yenye uwezo wa kuingiza nchini mitambo ya umeme wa dharura kwa kutumia gesi kwa kipindi maalum cha mwaka mmoja hadi miwili. Je, ni sababu zipi zilizoifanya Serikali iruhusu kufunguliwa *LC* ya uingizaji wa mitambo ya kampuni ya *Richmond*?

(f) Ni kiasi gani cha hasara nchi imepata kwa mradi huu kutokamilika ndani ya muda wa dharura ya umeme?

Mheshimiwa Spika, maswali haya hayana budi kupatiwa majibu ya uhakika ili wananchi waridhike. Kutokana na ugumu uliojitokeza awali wa kupata mkataba kati ya Serikali na *Richmond*, Kamati kwa kutumia Kanuni ya 104 na 105 na Kanuni za Bunge, Toleo la 2004 inapendekeza Bunge lako Tukufu liunde Kamati Teule itakayokuwa na uwezo kisheria kuupata mkataba huo na kuchunguza mchakato mzima uliopelekea Kampuni hiyo ya *Richmond* kuteuliwa. Kamati itakayofanya kazi hii itatumia vigezo vipana zaidi kuliko vile vya makosa ya kijinai vilivyotumiwa na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU). (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Kamati inaona umuhimu wa kuwepo taarifa bayana kuhusu mchakato mzima wa kumpata mzabuni yeyote zikihusisha mambo ya kitaalam kama *specifications*, thamani, uwezo na uzoefu wa mzabuni husika.

Mheshimiwa Spika, Mpango Kabambe Wa Umeme, Kamati imebaini kuwa tatizo la umeme limekuwa sugu na linaathiri maendeleo ya kijamii na kiuchumi hapa nchini. Kamati inashauri Serikali iandae mpango madhubuti wa muda wa kati na muda mrefu (*Power System Master Plan)* ukionyesha ni namna gani nchi itakavyokabiliana na tatizo hili la mfumo mzima wa uzalishaji na usambazaji wa umeme. Hii itaipunguzia Serikali gharama ya kuingia mikataba ya dharura kwa lengo la kupata ufumbuzi wa tatizo la umeme. Aidha, mpango huo ujumuishe pamoja miradi kama ya *Stiglers Gorge* ya kuzalisha umeme wa megawati 2100 na zaidi, makaa ya mawe ya Mchuchuma, umeme wa nishati ya upepo, maporomoko ya maji pamoja na vyanzo vingine vya umeme.

Mheshimiwa Spika, Kamati inatambua hali mbaya ya kifedha inayolikabili Shirika la Umeme Tanzania ambapo gharama za uendeshaji zinazidi mapato ya Shirika. Hivyo basi, Kamati inaunga mkono Mpango Maalumu wa Kurekebisha Hali Mbaya ya Fedha ya Shirika la Umeme (*Financial Recovery Plan)* ya *2006 – 2010* ambao unalenga kulikwamua Shirika kifedha. Aidha, Kamati inaishauri Serikali kuidhamini *TANESCO* ili iweze kukopeshwa na vyombo au Taasisi za fedha badala ya kutegemea Bajeti ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, katika harakati za kuongeza uzalishaji wa umeme nchini, Kamati inaishauri Serikali iharakishe kukamilisha mpango wake wa kukinunua Kituo cha Uzalishaji Umeme (*Independent Power Transmission Limited (IPTL)* pamoja na zoezi la kukigeuza kituo hicho kitumie gesi asilia badala ya mafuta mazito. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Shirika la Maendeleo ya Petroli (*TPDC*) Kamati inatambua kwamba Shirika la Maendeleo ya Petroli (*TPDC)* lina umuhimu mkubwa katika kufanikisha utafiti na hatimaye upatikanaji wa mafuta na gesi asilia nchini. Kwa hiyo, Kamati inaishauri kuwa Shirika hilo lipewe fedha za kutosha kwa ajili ya utekelezaji mzuri wa majukumu yake.

Mheshimiwa Spika, Kamati imeona kwamba kuwe na utaratibu wa kuibakizia fedha *TPDC* (*Retention)* ili Shirika libaki na kiasi fulani cha fedha hizo zinazotokana na mauzo ya gesi asilia utaratibu ambao unatumika kwenye baadhi ya Wizara na mashirika mengine ambayo yana mapato ya aina hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Kamati inakumbusha kwamba utaratibu uliotangazwa na Serikali wakati wa Hotuba ya Bajeti ya Serikali 2006/07 kwamba *TPDC* ishiriki katika kuagiza mafuta nje ili kudhibiti bei za mafuta, utekelezwe haraka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Kamati imesikitishwa na madai ya fidia na kusitishwa mkataba wa uagizaji wa mafuta kati ya Shirika la Maendeleo ya Petroli (*TPDC*) na *ADDAX* mwaka 1999/2000. Hali hii imelifanya Shirika la Maendeleo ya Petroli (*TPDC*)

kutozwa riba kubwa *(Compound interest)* kutokana na kutokuwa na uwezo wa kulipa deni hilo la Dola za Marekani 1,898,562. Kutokana na hali hiyo, Serikali inalazimika kulipa riba ya Dola za Marekani 62,929 kwa Wakili wa madai *M/S Hunton Williams* kila mwaka huku deni la msingi likiendelea kuongezeka. Kamati inaishauri Serikali itafute fedha ili deni hilo la msingi lilipwe lote haraka kwa shabaha ya kuondoa gharama za malipo ya riba juu ya riba na hivyo kuligharimu Taifa fedha nyingi.

Mheshimiwa Spika, Serikali pia iliahidi kuwa Shirika la *TPDC* litahusika na mpango mzima wa Hifadhi ya Taifa ya Mafuta *(Strategic Oil Reserves).* Kamati inashauri kwamba mpango huo utekelezwe kwa kiasi inavyostahili kwa kuiwezesha *TPDC* kifedha ili itekeleze kazi hiyo na Bunge lipewe taarifa hatua kwa hatua. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu Jengo la Mafuta *(Mafuta House)* ambalo lilitolewa bure kwa Shirika la Hifadhi ya Jamii (*NSSF*) baada ya *TPDC* kushindwa kulimalizia; Kamati inashauri kuwa, jengo hilo liendeshwe kwa ubia kati ya Mashirika hayo mawili pamoja na Shirika la Nyumba la Taifa (*NHC*) kulingana na kila shirika lilivyochangia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu kutokuanza kwa utafutaji wa mafuta katika baadhi ya vitalu vinavyomilikiwa na makampuni ya *Shell International* na *Antrim Resources* eneo la Zanzibar, unaotokana na kutokukamilika kwa upatikanaji wa ufumbuzi wa matatizo yaliyopo kati ya Serikali ya Muungano na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Kamati inashauri Serikali ya Muungano iharakishe kukamilisha mazungumzo kati yake na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ili muafaka upatikane na kampuni husika ziweze kuanza kazi ya utafutaji wa mafuta. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, *Mnazi Bay*- Visima Vya Gesi, Asilia, Kamati imeridhishwa na juhudi zinazofanywa na Kampuni inayotafiti kuwepo kwa gesi asilia eneo la *Mnazi Bay* Mkoani Mtwara. Kampuni hiyo yenye visima viwili vya gesi asilia (*MB1* na *MB2*) ambapo mpaka sasa imegundua gesi nyingi sana katika kisima cha pili ambacho kitaiwezesha Kampuni hiyo kuzalisha umeme hadi megawati 200 na zaidi. Kampuni hiyo hivi sasa inachimba kisima cha tatu (*MB3).* Kwa sasa *Artumas* inazalisha umeme wa MW 18 kwa ajili ya Mikoa ya Lindi na Mtwara. Kamati inaipongeza kampuni hii kwa kutimiza malengo yake kwa wakati. Aidha, Kamati inaishauri Serikali kujiandaa na upatikanaji huo wa umeme kwa kuhakikisha kwamba miundombinu ya kusafirishia umeme huo inakuwepo ili kuondoa tatizo la nishati ya umeme kwa Mikoa ya Kusini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sekta ya madini ni moja kati ya sekta zilizojipatia umaarufu mkubwa kwa kuweza kuitangaza nchi yetu na kukuza Pato la Taifa. Kamati imeweza kubaini mambo mbalimbali katika sekta hii na inatoa maoni na ushauri ufuatao:-

Mheshimiwa Spika, Kamati inapenda kumpongeza Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete kwa hatua aliyochukua ya kuunda Tume Maalum ya kufuatilia mikataba

ya madini iliyoingiwa na wawekezaji hapa nchini. Aidha, Kamati imefarijika sana na uamuzi huo na inaamini kwamba suala la umilikaji wa machimbo ya madini kwa njia halali utadumishwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Kamati imeona kwamba wananchi wengi walioondolewa katika maeneo ya uchimbaji wa madini wameachwa bila kupatiwa fidia kama walivyoahidiwa. Kamati inashauri kwamba Serikali ihakikishe kwamba wananchi hao wanapatiwa fidia zao kulingana na kanuni na taratibu zilizowekwa. Aidha, Kamati inatoa angalizo kwamba kama fidia zilitolewa lakini haikuwafikia walengwa basi hatua zichukuliwe kurekebisha dosari hiyo.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa hivi sasa wananchi walio katika maeneo ya uchimbaji wa madini wameonekana kukosa faida zitokanazo na uchimbaji wa madini. Kamati inashauri kwamba mikataba ya madini iwe na kipengele kinachotoa fursa kwa wakazi wa maeneo husika kuwa na hisa katika makampuni ya uchimbaji wa madini, hasa kupitia Halmashauri zao za Wilaya. Hapa tunazingatia kwamba ardhi sasa inathamani na inaweza kutumiwa kama sehemu ya hisa zao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri Serikali kuelekeza Makampuni ya Madini kutoa kipaumbele cha ajira kwa Watanzania hususan waliopo maeneo ya uchimbaji wa madini.

Mheshimiwa Spika, kuhusu michango ya maendeleo inayotolewa na Makampuni ya uchimbaji wa Madini, Kamati inashauri kwamba michango hiyo iingizwe kwenye Makubaliano *(Memorandum of Understanding)* kati ya Makampuni ya Madini na Halmashauri za Wilaya ili sasa isiwe hisani bali iwe ni jukumu la msingi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kiasi kikubwa cha madini husafirishwa nje ya nchi kwa ajili ya kusafishwa na kukatwa kutokana na kutokuwepo kwa viwanda hivyo hapa nchini. Kamati inaishauri Serikali iharakishe utekelezaji wa uamuzi wa kuanzisha uwekezaji katika viwanda vya kusafisha na kukata madini hapa nchini badala ya madini hayo kusafirishwa kwenda nje ya nchi yakiwa hayajachakatwa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu uchimbaji wa *gemstones*, Kamati inashauri kwamba uchimbaji huo ufanywe na wazalendo/kampuni za kizalendo kwa kushirikiana na kampuni nyingine za nje kwa ubia isipokuwa mikataba iliyopo sasa hivi iendelee kuheshimiwa.

Mheshimiwa Spika, sekta ya Viwanda Kamati, inathamini mchango wa sekta ya viwanda ambayo inachangia kwa kiasi kikubwa ukuaji wa uchumi, kuongeza ajira na

kuvutia wawekezaji nchini. Ni katika mantiki hiyo, Kamati mara baada ya kutembela maeneo mbalimbali yanayojihusisha na sekta hii imeweza kutoa maoni na ushauri utakaoweza kuboresha sekta hii kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Kamati inatambua kwamba nchi yetu ina malighafi nyingi zinazoweza kutumika katika kuendesha viwanda vyetu. Hivyo Kamati inashauri kwamba, Serikali ihakikishe kuwa kwa kiasi kikubwa viwanda vyetu vinatumia malighafi zinazopatikana hapa nchini sambamba na kuhamasisha uzalilishaji wa malighafi hizo kama vile kwenye viwanda vya nguo, mafuta ya kupikia na kadhalika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Kamati inaamini kwamba, zipo faida kubwa zinazopatikana kutokana na ushindani wa biashara. Kwa kuwa kuna baadhi ya Makampuni makubwa yanatumia mbinu mbalimbali za kuuwa Makampuni madogo yanayozalisha bidhaa zinazofanana na zao kwa njia ya kuleta ushindani wa kibiashara ambao si sawa, Kamati inashauri kwamba itolewe elimu ya Sheria kuhusu Ushindani Halali (*Fair Competition)* ili kuweza kulinda Viwanda vichanga kwa mfano hali ya mgogoro wa biashara ya sigara baina ya Kampuni ya sigara Tanzania (*TCC*) na Kampuni ya Sigara ya *Mastermind (Mastermind Tobacco Tanzania Ltd).* Ni mfano mmoja wa ushindani ambao si ushindani halali.

Mheshimiwa Spika, kuhusu viwanda vya korosho vilivyonunuliwa na wazalendo kushindwa kupata mikopo kutoka kwenye mabenki kutokana na viwanda hivyo kutofanyiwa tathimini upya kwani bei za kununulia viwanda hivyo ilikuwa ndogo kwa sababu haja ya Serikali ilikuwa kwamba viwanda hivyo visifungwe bali vifufuliwe kwa njia yoyote ile. Viwanda hivyo kutokuwa na hati miliki kunavifanya visikopeshwe.

Kamati inashauri kwamba Serikali iviwezeshe viwanda vya korosho vilivyonunuliwa na wazalendo kufanya kazi na kuhakikisha kwamba vinafanyiwa tathimini na kupata hati miliki haraka baada ya masharti muhimu kukamilika ili kuweza kutumia Hati hizo kupata mikopo kwa maana benki zinahitaji dhamana za vitu ambyo vya kudumu.

Mheshimiwa Spika, Viwanda vilivyopo sasa vinasimamiwa kisekta kwa maana ya kwamba viwanda chini ya Sekta nyingine haviangaliwi na Wizara yenye jukumu la Viwanda. Utaratibu huu si mzuri kwa hiyo Kamati inaishauri Serikali kuwa, viwanda vyote visimamiwe na Wizara moja ambayo ni Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko. Hali hii itawezesha kuweka utaratibu mzuri wa kuratibu shughuli za maendeleo ya viwanda na masoko nchini wakati Wizara za kisekta zikiendelea kusimamia maeneo hayo kiutalaam. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Biashara na Masoko, Kamati inatambua kwamba masoko ni moja ya maeneo muhimu sana ambayo yanategemewa na sekta nyingine kama vile viwanda, madini na biashara, kwa kuwa uwepo wa masoko unawezesha bidhaa

zinazotengenezwa ndani ya nchi kupata wanunuzi ndani na nje ya nchi. Kwa ajili ya kuboresha Sekta ya Masoko, Kamati inatoa maoni na ushauri ufuatao:-

Mheshimiwa Spika, Kamati imeona kwamba utaratibu wa ujenzi wa masoko katika maeneo mbalimbali ni mzuri ila inaishauri Serikali iendelee na utaratibu huo na kuhakikisha kwamba masoko yanajengwa haraka mfano soko la Segera na Makambako, na kutumika kwa muda muafaka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Kamati baada ya kutembelea viwanda vya korosho katika Mikoa ya Lindi na Mtwara, imebaini kwamba ununuzi wa korosho unafanywa kwa bei za chini sana na hivyo kuonekana kuwakandamiza sana wakulima wadogo na kuwanufaisha wanunuzi. Kamati inashauri kwamba bei ya ununuzi wa korosho uendane na bei ya bidhaa hii katika Soko la Dunia ili kumuwezesha mkulima mdogo kupata faida baada ya kuondoa gharama zake za uzalishaji. Hili likifanyika litawapa ari na moyo wakulima hao kuweza kuendeleza na kuzalisha/kutunza maeneo ya korosho na hivyo kujiongezea kipato na vile vile pato la taifa kukua.

Mheshimiwa Spika, kuhusu uzalishaji wa chumvi, Kamati inaishauri Serikali itilie maanani uzalishaji chumvi nchini hasa inayozalishwa Mkoani Lindi kwa kuwaongoza wazalishaji wadogo wanunue mashine za kusagia chumvi na kuwezesha chumvi hiyo kutumika hapa nchini badala ya kuagiza chumvi kutoka nje.

Mheshimiwa Spika, Shamba la Mpira la Kihuhwi ambalo lina tataizo la ulipaji mishahara wafanyakazi liangaliwe vizuri sana kwa sababu mpira huo bado unahitajika na ni mali ghafi nzuri sana kwenye kiwanda chetu cha *General Tyre*. Kiwanda cha *General Tyre* ambacho kinamilikiwa kwa pamoja na Serikali yetu na kampuni ya *Continental Tyre,* ni kiwanda muhimu sana na kwa kuwa ubinafsishaji wake una matatizo, ni vizuri Serikali ikaelewa waziwazi kwamba *Brand Name* iliyoko pale siyo ya Tanzania kwa hiyo huwezi kubinafsisha kiwanda hiki sawa sawa na viwanda vya maguni pamoja na ngozi na ni vizuri tusije tukawapoteza wawekezaji hawa wa Ujerumani kwa sababu *General Tyre* ni jina la Kimataifa, kwa hiyo kubaki nalo inatusaidia.

Kwa hiyo, katika hali Serikali ichukue hatua za kuhakikisha kwamba usimamizi wake wa ubinafsishaji unakuwa kwenye mikono ya watu ambao wamepewa kazi hiyo, ambayo ni Wizara ya Viwanda na Biashara pamoja na Wizara ya Fedha ili tusije tukawavuruga Wajerumani kwa sababu bodi yao ina Wajerumani mle ndani na wanashangaa kusikia watu mbalimbali wengi wanaingilia shughuli za kampuni hiyo.

Mheshimiwa Spika, Kamati imeona kuwa upo umuhimu wa Serikali kuandaa utaratibu mzuri wa kuwawezesha wajasiriamali wadogowadogo si tu kuwapatia mikopo bali kuwaendeleza ili waweze kufikia viwango vinavyotakiwa ikiwa ni pamoja na kuwatafutia masoko ya kuuza bidhaa zao.

Mheshimiwa Spika, haya ni mapendekezo na maoni na ushauri katika maeneo ya kila sekta. yako maeneo ya jumla kwenye ukurasa wa 16 hayo naomba Waheshimiwa Wabunge wazingatie na wanaweza kutoa maoni kwa sababu ya muda sitaweza kuyazungumza yote isipokuwa nitadokeza yako maeneo kama kumi hivi. Moja, ni ukaguzi wa hesabu za mashirika. Utaratibu wa kukagua hesabu za mashirika unaongozwa sasa hivi na *International Financial Reporting Standards,* kwa hiyo mashirika yanatoka kwenye utaratibu wa *Tanzania Financial Reporting Standards* kuna ucheleweshaji hapa wa uteuzi wa wakati kwa hiyo tunashauri Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu aweke utaratibu ambao unaharakisha kuteua wakaguzi ili mashirika yawe na hesabu za wakati.

Mheshimiwa Spika, lingine linahusu Mtwara *Development Corridor* na *Central Development Corridor*. Maeneo hayo yanaongozwa na Kamati za Mawaziri wa Nchi ambazo zinashiriki. Tunadhani utaratibu huu sasa ubadilishwe badala yake ziundwe kamisheni ya maeneo hayo ili kwenda na wakati. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, eneo lingine linahusu *gas* asilia. Kutokana na kuongezeka kwa gesi na upatikanaji na uzalishaji na matumizi ya gesi kuongezeka, Kamati inashauri kwamba Serikali itunge sheria mpya ya matumizi ya gesi asilia ili iweze kusimamia nishati hii muhimu kwa ufanisi.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine linahusu Sheria za Mashirika yaliyoko chini ya sekta hizi nilizotaja hapa. Sheria hizi ni za siku nyingi sana na zimepitwa na wakati, zimeorodheshwa katika kiambatanisho namba (3), tunaishauri Serikali itengeneze *Legislative Program* ili sheria hizo ziweze kwenda na wakati.

Mheshimiwa Spika, naomba kuchukua fursa hii kukushukuru wewe kwa kututeua sisi kuwa Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji na Biashara mwezi Januari, 2006 kwa mujibu wa Kanuni ya 87(4) ya Kanuni za Bunge. Pia naomba niwashukuru Wajumbe wenzangu waliofanya kazi bila kuchoka na kuyafikia maeneo yote yanayoonyeshwa kwenye Taarifa hii. Michango na maoni yao yamewezesha kufikia hapa tulipofika kwenye taarifa hii. kwa hiyo nawashukuru kwa dhati kabisa.

Mheshimiwa Spika, naomba niwatambue Wajumbe hao kwa majina nao ni Mheshimiwa Dr. Harrison G. Mwakyembe, M/Mwenyekiti. Wafuatao ni wajumbe nao ni Mheshimiwa Muhammad A. Chomboh, Mheshimiwa Yahya K. Issa, Mheshimiwa Asha M.Jecha, Mheshimiwa Siraju J. Kaboyonga, Mheshimiwa Mwajuma H. Khamis, Mheshimiwa Vuai A. Khamis, Mheshimiwa Fuya G. Kimbita, Mheshimiwa Eng. Stella M. Manyanya, Mheshimiwa Fatma A. Mikidadi na Mheshimiwa Herbert J.Muntangi.

Wajumbe wengine ni Mheshimiwa Mohammed H. Mnyaa, Mheshimiwa Luhanga Joelson Mpina, Mheshimiwa Mbaruk K. Mwandoro, Mheshimiwa Savelina Silvanus Mwijage, Mheshimiwa Dr. Lucy S. Nkya, Mheshimiwa Christopher O. Ole-Sendeka,

Mheshimiwa Lucy F. Owenya, Mheshimiwa Ahmed Ally Salum, Mheshimiwa Haji J. Sereweji, Mheshimiwa Ahmed Mabkhut Shabiby, Mheshimiwa Mohammed S. Sinani, Mheshimiwa Abdallah Salum Sumry na mimi William H. Shellukindo, Mwenyekiti.

Mheshimiwa Spika, kwa mara nyingine tena, naomba kutoa shukrani zangu kwako kwa kunipa nafasi ili niweze kuwasilisha taarifa ya Kamati kwa kipindi cha Mwaka mmoja (2006) uliopita wa Bunge hili jipya.

Mheshimiwa Spika, Kamati ina angalizo lifuatalo, Kamati yangu imebaini kuwa Taarifa za Kamati zinawasilishwa Bungeni wakati bajeti zimekwishapitishwa, hivyo ushauri unaonekana kutokwenda na wakati na hivyo kutotekelezwa. Kamati yangu inashauri kwamba Taarifa za Kamati za mwaka zijadiliwe kwenye Mkutano wa Bunge la mwezi Januari/Februari kila mwaka ili ushauri unaotolewa uweze kuzingatiwa kwenye Bajeti ya mwaka unaofuata. Ikiwa pendekezo hili litakubaliwa basi taarifa za Kamati za 2007 ziwasilishwe mbele ya Bunge lako Tukufu kabla Kamati hizo hazijabadilishwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba nichukue fursa hii kuwashukuru Mawaziri, Mheshimiwa Nazir M. Karamagi, alipokuwa Waziri wa Viwanda, Biashara na Masoko na aliyekuwa Naibu wake Mheshimiwa Dr. David Mathayo David. Pia namshukuru Mheshimiwa Dr. Ibrahim Msabaha, aliyekuwa Waziri wa Nishati na Madini na aliyekuwa Naibu wake Mheshimiwa Lawrence K. Masha kwa ushirikiano waliotoa kwa Kamati hii.

Mheshimiwa Spika, naomba niwashukuru Mawaziri, Mheshimiwa Basil P. Mramba, Waziri wa Viwanda, Biashara na Masoko na Naibu wake Mheshimiwa Hezekiah Chibulunje . Pia nawashukuru Mheshimiwa Nazir M. Karamagi, Waziri wa sasa wa Nishati na Madini na aliyekuwa Naibu wake Mheshimiwa Bernard K.Membe, ambaye sasa ni Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa kwa ushirikiano walioutoa kipindi chote Kamati ilipokuwa kazini.

Aidha, napenda kumpongeza Mheshimiwa William Ngeleja, kwa kuteuliwa kuwa Naibu Waziri wa Wizara hii wakati wa kukamilisha taarifa hii. Ninamkaribisha kwa dhati katika familia ya Nishati na Madini. Napenda pia kuwashukuru Makatibu Wakuu wa Wizara hizi mbili, Dr. Stergomena Tax- Bamwenda wa Wizara ya Viwanda Biashara na Masoko, Ndugu Arthur Mwakapugi wa Wizara ya Nishati na Madini, Ndugu Wilfred Nyachia aliyekuwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko pamoja na watendaji wote wa Wizara hizo, kwa utendaji wao wenye ufanisi.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla ziara za Kamati Mikoani zilifanikiwa kwa kiasi kikubwa kutokana na mapokezi na ushirikiano ambao Kamati ilipata kutoka kwa Wakuu wa Mikoa ya Arusha, Dar es Salaam, Iringa, Lindi, Manyara, Mtwara na Tanga; Mikoa ambayo Kamati ilifanikiwa kuitembelea na kuweza kujionea shughuli mbalimbali za Wizara za Nishati na Madini na Viwanda, Biashara na Masoko zinazofanywa katika Mikoa hiyo.

Kamati inapenda kutoa shukrani kwa Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya zao kwa ushirikiano mkubwa waliotoa na kushauri ushirikiano huo uzidi kuendelea. Aidha, katika Ratiba ya Kamati kwa mwaka 2007 itazingatia kutembelea maeneo ambayo Kamati haikupata fursa ya kuyatembelea na kuona utekelezaji wa shughuli za Wizara hizo na Taasisi zake.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee Kamati yangu inapenda kukushukuru wewe mwenyewe kwa kuliongoza kwa "Speed and Standard" Bunge letu na pia kwa heshima uliyotupa kwa kututeua kuwa Wajumbe wa Kamati ya Uwekezaji na Biashara. Kwa pamoja tutatekeleza majukumu yetu kwa lengo la kutimiza utekelezaji wa majukumu ya Bunge letu ya kusimamia na kuishauri Serikali na vyombo vyake katika kutekeleza matakwa ya Katiba ya Nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba pia kumshukuru Katibu wa Bunge Ndugu Damian S. Foka na Ofisi yake kwa kuwezesha Kamati yetu kufanya kazi bila matatizo yoyote. Mwisho, naomba niwashukuru Makatibu wa Kamati Ndugu Aggrey N. Nzowa, Ndugu Abdallah Hancha na Ndugu Lina Kitosi kwa kazi nzuri waliyofanya ya kuhudumia Kamati hii kwa ufanisi mkubwa unaoonekana katika taarifa niliyotoa sasa hivi.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na naomba Bunge lako Tukufu lipokee Taarifa hii, liijadili na kuishauri Serikali ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**MHE. DR. HARRISON G. MWAKYEMBE:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa William Shellukindo, Mwenyekiti wa Kamati ya Uwekezaji na Biashara.

Waheshimiwa Wabunge Taarifa ya Kamati ya Uwekezaji na Biashara, imewasilishwa na inayo mapendekezo ambayo yametolewa hoja. Imevutia wachangiaji 16 sidhani kama tutakuwa na nafasi ya kuwasikiliza wote hasa kama watatumia muda wao wa kuchangia ule wa dakika 15 kwa sababu huo utatuwezesha kuwasikiliza labda tisa tu lakini nitaangalia. Hivi sasa nitawataja wale ambao wamejiorodhesha kuomba kuchangia nao ni Mheshimimiwa Khadija Salum Ally Al-Qassmy, Mheshimiwa Beatrice Shellukindo, Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa, Mheshimiwa Mohamed Habib Juma Mnyaa, Mheshimiwa Kabuzi Rwilomba, Mheshimiwa Mkiwa Adam Kimwanga na Mheshimiwa Eng. Laus Omar Mhina.

Wengine ni Mheshimiwa George Simbachawene, Mheshimiwa Mhonga Said Ruhwanya, Mheshimiwa Christopher Olonyokie Ole-Sendeka na Mheshimiwa Dr. Guido

Gorogolio Sigonda, Mheshimiwa Ruth Blasio Msafiri, Mheshimiwa Dr. Binilith Satano Mahenge, Mheshimiwa Siraju Juma Kaboyonga, Mheshimiwa Jackson Makwetta na Mheshimiwa Mariam Reuben Kasembe. Kwa hiyo, nitawaita kwa jinsi ninavyowaona wamo humu wengine hawamo nitaanza sasa na Mheshimiwa Beatrice Shellukindo, atafuatiwa na Mheshimiwa Mohamed Mnyaa na nafasi ikiwepo ataendelea Mheshimiwa Kabuzi Rwilomba. Sasa namwita Mheshimiwa Beatrice Shellukindo.

**MHE. BEATRICE M. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwa sababu huwa ninaongea haraka, nadhani nitajaribu kutumia muda pungufu ili wengi wapate nafasi.

Aidha, nichukue fursa hii, kumpongeza Mwenyekiti wa Kamati, Mheshimiwa William Shellukindo na Kamati yake yote kwa kutuandalia taarifa nzuri yenye changamoto za utekelezaji ambazo kwa kweli zimeangalia sekta muhimu sana ambazo tunazo kwenye jamii yetu.

Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge, mtakubaliana nami kwamba sekta ambazo zipo katika Kamati hii ni zile sekta ambazo kwa kweli ni muhimu sana kwa maendeleo ya nchi yetu kiuchumi na kwa wananchi wetu kwa ujumla.

Nikianza tu pale niliposoma ukurasa wa tatu ile paragraph 1.8, kidogo nilianza kufadhaika kuona Kamati imetembelea wawekezaji wadogo wadogo wazalendo katika maeneo ya uchimbaji wa madini kuona kwamba Kilindi hawakufika japo walikuwa Tanga lakini nimehamasika pale mwisho ambapo Mwenyekiti aliposema kwamba kwa mwaka huu wataenda maeneo ambayo hawakufika, kwa hiyo ninaamini na Kilindi itakuwa kwenye orodha.

Mheshimiwa Spika, kuhusu nishati, ukurasa wa nne pale Kamati imekiri kuwa Sekta ya Nishati na Madini ni moja ya sekta muhimu sana katika kuleta maendeleo ya Taifa na maendeleo ya Taifa ni pamoja na Wilaya ya Kilindi. Mtanisamehe, mtaendelea kusikiasikia Kilindi lakini ndio mambo yaliyonileta humu ndani na kwa sababu Kilindi ni mojawapo, kwa kweli tunahitaji umeme. Kwa heshima kabisa, nasema pale ambapo Serikali inaamua kuwawekea wenzetu taa za barabarani, sisi tunaomba tu taa mpaka Makao Makuu ili tuweze kupata huduma. Ni makosa kuzungumzia mambo ya vyama lakini Ilani ya Chama ambacho kinatawala inasema ni vema pia umeme ukafika katika kila Makao Makuu ya Wilaya lakini kwa kweli inasikitisha sana ukiangalia Makao Makuu ya Wilaya ya Songe umeme haujafika mpaka leo.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2006/2007 ninawashukuru sana, Bunge hili lilipitisha mapendekezo yaliyoletwa na Wizara ya kuwekewa umeme hadi kufikia Makao Makuu ya Wilaya lakini hakuna lililofanyika kwa mwaka ule sababu zilitolewa ni pamoja na njaa na kadhalika ambayo tulikubali. Mwaka 2007/2008 pia zimetengwa fedha na tukaambiwa kwamba zinafika Makao Makuu ya Wilaya, hapa naomba Kamati tushirikiane. Kwa kweli ninaomba sana msaidie kuwaambia watu Wizara kwamba tunaomba kinachosemwa hapa Bungeni kiwe ni kile ambacho kinatekelezeka.

Mheshimiwa Spika, binafsi nimeenda ile Wizara ya Nishati na Madini, nadhani wamechoka kuiona sura yangu pale lakini nashukuru ushirikiano wananipa. Lakini baada ya kufuatilia kwa Mkurugenzi husika nikaelekezwa kwenda *TANESCO* na *TANESCO* nimeenda nimekutana na wale watendaji inasikitisha kwamba fedha ambazo zimepitishwa mwaka huu zinatosha kuweka umeme kilometa nane tu ambao ni kutoka kijiji ambapo umeme ulipo Kwediboma kufika Mgera na hii inakuja kuelezwa wakati tayari kwenye bajeti tumesema kwamba umeme utafika Songe Makao Makuu.

Mheshimiwa Spika, Mbunge wa Kilindi, mama Shellukindo ameenda kwenye majukwaa akiahidi wananchi kwamba ya mwaka jana yamepita lakini safari hii tunapewa umeme mpaka Songe, kumbe eti ni kijiji kimoja. Ninaomba Kamati tusaidiane taarifa zitolewe. Ni kweli tuna tatizo la umeme maeneo mengi siyo Kilindi tu na bajeti yetu ni ndogo tunakubali na sisi wana Kilindi lakini basi tuambieni lile ambalo lipo tusiendelee kuonekana si wasema kweli! Aidha, cha muhimu zaidi tusivunje imani ya wananchi wetu. Unajua Mtanzania ni mtu mwelewa sana ukimweleza hili linawezekana anakubali haliwezekani anakubali basi tuwaeleze ukweli.

Mheshimiwa Spika, lakini vile vile pamoja na kwamba kwa kweli nishati ni suala la kuleta maendeleo lakini pia wananchi wana haki. Leo asubuhi nimesikia hapa kidogo uchungu wakati Naibu Waziri akizungumzia *TV* na nini, maskini wananchi wangu inabidi walipe hela nyingi kwenda kwa wale wachache ambao wana jenereta kuweza kuangalia *TV*, kumbe kuna wengine yaani tu ni kwamba masafa hayaonekani vizuri. Ninaomba basi kwenye hili suala la umeme tupewe kipaumbele angalau na benki nazo ziweze kuja kuwekeza na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, lakini vile vile naomba hizi *BOQ* za miradi mbalimbali ziandikwe kwa lugha nyepesi, lugha ambayo inaeleweka na zile thamani ziwepo. Kwa hiyo, kama mradi unaletwa mahali mara nyingi ile lugha ni ngumu sana inahitaji mtu kwa kweli awe amesoma aweze kuielewa. Hii ni kwa miradi yote ya barabara na kadhalika lakini hata hii ambayo inaletwa na Wizara ya Nishati na Madini iwe inaeleweka thamani ya vitu ambavyo vinakusudiwa na kazi ambayo inakusudiwa kufanywa, hii itasaidia sana hata wananchi kujua linaloendelea na pia itaweza kusaidia kuondoa hisia potofu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Richmond, natoa pongezi nyingi sana kwa Kamati kwa uchambuzi mzuri na mkubwa walioufanya lakini kinachonisikitisha hii Kamati ilipokuwa ikitambulishwa hapa kuna wajumbe waliobobea, wataalam, watu wenye uwezo, watu ambao ni mahiri wanaweza wakaeleza kitu kikaeleweka, hivi kweli tunasubiri mpaka ratiba iandaliwe ya kutoa taarifa za Kamati ndiyo waje watueleze suala la Richmond ambalo ni nyeti na limegusa wananchi wengi na hisia za wengi?

Mheshimiwa Spika, nimeshangazwa na nimesikitishwa pamoja na taarifa yao nzuri, hii ingetoka kwa wakati, hisia nyingi tofauti tofauti ambazo tumekuwa tunazisikia zisingekuwepo angalau ingeonyesha utawala bora ndani ya nchi yetu. Mimi ninaomba taarifa zinapokuwepo kama hizi za masuala ambayo yanagusa jamii, nchi na uchumi na kadhalika na ni suala nyeti litolewe taarifa mara moja siyo Kamati ingoja saa hizi inakuja haya mambo sijui ni ya tangu mwanzo wa mwaka huko leo yanaletwa hapa, hata

ukiyaeleza mara nyingine yanakuwa hayana maana sana. Kwa hiyo, naomba sana Kamati kwa masuala kama haya na siyo Kamati hii tu, Kamati zote inapokuwa na mambo ambayo ni nyeti basi yaletwe kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, kwa kweli nisingependa sana kuongelea *Richmond* maana imeshaongelewa lakini kama wananchi wengine wengi mimi pia natarajia kupata majibu ambayo Kamati hii imeleta ya maswali ambayo yameulizwa. Lakini niseme naungana mkono sana na pendekezo la kuunda Kamati Teule kwa sababu mambo ni mengi unajua hata kama hulielewi hili suala, pale inasema kwamba hawa *Richmond* walishindwa kutekeleza sijui mradi wa bomba la mafuta huko nyuma mwaka 2005, walienda kinyume na makubaliano na Serikali, sasa kweli hii inahitaji hata elimu kidogo kujua kwamba hawa watu wana matatizo halafu leo hii wanakuja kupewa mradi mwingine, haya ndio yanaibua maswali na pale ambapo hayapati majibu kwa wakati yanakuwa kwa kweli yanaleta matatizo. Ninasema hivi haiwezekani kabisa, Kamati Teule iundwe, ukweli ujulikane, wahusika wachukuliwe hatua stahili ili turejeshe imani ya Watanzania ambayo si tu imepotea kwa Serikali yao lakini pia wanasema Bunge hili ni Bunge ambalo linapelekeshwa. Ngoja niachana na mambo ya Richmond ingawa nilikuwa na mengi ya kusema.

Mheshimiwa Spika, kuhusu madini, haya ndiyo yamenisimamisha, nimpongeze Waziri, Naibu Waziri, Kamishna na Ofisi yake kwa ujumla kwa kweli wamenisaidia sana lakini ninachosema hapa ninampongeza Rais Kikwete kwa kuunda ile Tume Maalum ya Kufuatilia Mikataba ya Madini lakini ninauliza labda mimi sijaelewe ili niweze kuelewa na wananchi wangu waelewe kwa majibu nitakayopewa, ni mikataba ya uchimbaji au ya utafiti pia kwa sababu robo tatu ya Wilaya ya Kilindi iko chini ya utafiti lakini vile vile utashangaa kwamba uchimbaji unaendelea? Mara nyingi kuna Wabunge tunazungumza hapa lakini Waziri mara nyingi hupenda kusimama na kusema sheria haziruhusu, lakini nataka kulihakikishia Bunge hili, uchimbaji unaendelea na kama mnataka basi hiyo Kamati ambayo itaundwa kwa mambo mengine basi ije na Kilindi ione kitu tunachokizungumza. Sasa nasema kwamba hebu tujue utaratibu ukoje na hiyo mikataba itaangaliwaje kwa sababu mingine pia ukiiangalia, kwa kweli inashangaza.

Mheshimiwa Spika, lakini pia nizungumzie faida kwenye Halmashauri. Tunapoomba tunaambiwa sheria italetwa lakini mpaka iletwe kweli tutakuwa tumeathirika na madini yetu yatakuwa yameisha kwa sababu unakuta leseni pia zinatolewa Wizarani fedha zinaenda Wizarani, kodi nyingine zinaenda kwa Afisa Madini wa Wilaya yaani unakuta tunachofaidi Halmashauri ni migogoro, uchafuzi wa mazingira na mambo mengine mengi.

Mheshimiwa Spika, lakini pia Kamati wamesema kwamba kipaumbele kitolewe kwa ajira kwa wananchi wenyewe wa Tanzania. Lakini nasema zile ajira za kitaalamu tunaweza tukasema Watanzania lakini ndugu zangu hata kazi za ulinzi basi mnaweka wageni. Nitolee mfano wa mradi mmoja kule kwetu wa Mafulila, wataalam wametoka Ghana na huko walikotoka na walinzi wanatoka huko na kwenye Mikoa mingine ya mbali, kweli wale wananchi wasiwe na hisia kwamba wanaibiwa mali yao hata kama hawaibiwi? Kwa nini tusichukue walinzi kutoka sehemu zile ambapo wananchi wapo

ambao wanafanya kazi za ulinzi, kupika na usafi tunaficha nini kama kazi inafanyika? Sekta hii ni muhimu, sekta hii ni nyeti, inabidi tuangalia kwa uangalifu.

Mheshimiwa Spika, angalizo ambalo amesema Mwenyekiti kwamba taarifa zitolewe Januari, Februari na mimi naunga mkono kwa kweli hii itatusaidia si tu kwenye bajeti lakini taarifa zitatolewa kwa wakati siyo baada ya matukio kupita na ninaiunga mkono hoja hiyo na ninaomba wenzangu waunge mkono.

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa, nina mengi lakini muda hauniruhusu nataka tu kusema sasa wale wananchi ambao wanatusikiliza na vyombo vya habari na wengine waliokuwa wanasema Bunge hili halina meno ni *rubber stamp* sasa wataanza kuona makali ya meno yetu kazi imeanzishwa na Kamati ya Uwekezaji, tunaiunga mkono, tunaomba mambo yaje ili turudishe imani ya wananchi kwamba Bunge lina uwezo na linafanya yale wanayoyaamini.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, ninawapongeza tena na ninasema kwamba nimefurahia taarifa yao na ninaiunga mkono kwa asilimia mia kwa mia. *(Makofi)*

**MHE. MOHAMED H. MNYAA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru na mimi kunipatia nafasi angalau nichangie machache katika Taarifa ya Kamati hii ya Uwekezaji na Biashara.

Mheshimiwa Spika, kwanza ningependa nimshukuru Mwenyekiti wa Kamati ya Uwekezaji na Biashara kwa kuwasilisha taarifa hii vizuri sana kwa njia ya upole, utulivu na taarifa iliyojaa mambo mazito ambayo Serikali yetu ya Jamhuri ikiwa watasikiliza kwa makini na kuyafuata mashauri hayo, basi nina hakika tutasonga mbele.

Mheshimiwa Spika, nategemea taarifa hii kama alivyosema Mwenyekiti katika kurasa za mwisho, imechelewa kidogo lakini nategemea hatujachelewa sana hata hivyo pamoja na kwamba leo angalau watapata usingizi kwa taarifa yetu hii kukosa kuja hapa kwa muda mrefu, nafikiri hata na wewe mwenyewe Mheshimiwa Spika ambaye ulishatoa maelezo kwenye magazeti na ikashindwa kuwasilishwa kama vipindi viwili, vitatu leo at least imefika. Kwa maana hiyo, ninaipongeza Kamati, ninampongeza Mwenyekiti angalau kwa kutupatia taarifa hii na kutimiza Ibara ya 63 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano kama inavyohitaji tuisimamie vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hapo, napenda nijikite katika ukurasa wa nane wa taaria hii ya Kamati. Katika ukurasa wa nane Mheshimiwa Mwenyekiti alizungumzia kuhusu kuharakisha *power system master plan.* Mimi ninaomba nisisitize hapo hii *power system master plan* ni kitu muhimu kwa sababu kitatupunguzia matatizo tuliyonayo ambayo yanaitia hasara Serikali hasa haya matatizo ambayo yanatufikisha kupata huu umeme wa dharura na hivi sasa Shirika la *TANESCO* kupitia mpango wake wa

*financially recovery* plan ni vema ingeenda sambamba na hii *power system master plan.* Ninaelewa tumeahidiwa kwamba ifikapo mwezi wa Desemba mwaka huu itakuwa imeshakamilika. Tunaomba iharakishwe kwa sababu gharama kubwa ya Serikali itaepukika, tutakuwa na malengo, tunajua mpango wetu wa umeme unaenda vipi katika kipindi cha miaka mitano, miaka kumi, miaka kumi na tano, miaka ishirini na kadhalika na tunaenda wapi na tuna malengo gani.

Mheshimiwa Spika, sote tutakumbuka kwamba katika bajeti iliyopita tuliona kule Mwanza kuliwekwa vinu vya umeme vinavyotumia mafuta ya *diesel* na vile vile viligharimu Tanzania pesa nyingi sana za jumla ya dola za Kimarekani milioni 116 na umeme huo unaozalishwa na mitambo hiyo ya Mwanza ya *diesel* ni megawati 40 tu, tuliarifiwa kwamba ni mitambo ya kukodi kutoka Kampuni ya Alstom na ni mwaka mmoja. Huo mwaka mmoja hapana muda tena kwa sababu mitambo ile imeanza kazi mwezi wa Machi kwa hiyo ikifika mwezi Februari 2008 mwaka umeisha na kujiuliza hapa je, tuna mipango gani wakiondoa hiyo forty megawati (*40Mw)* Mwanza tutaipata vipi, vipi tuta-boost grid yetu.

Mheshimiwa Spika, katika bajeti hiyo tuliyopitisha ya mwezi Julai mimi kama Msemaji Mkuu wa Wizara ya Nishati, niliwahi kupendekeza mambo mengi kuhusu kuepukana na kutumia vinu vinavyotumia *diesel*. Tuna mifano tosha wa *IPTL* unaotusumbua na nikapendekeza kwamba zile ziada tukitizama ule umeme tuliouweka kule wa dola milioni 116 na tukalinganisha wa megawati 40 na wa Aggreko wa megawati 40 zile zile lakini uliotumia dola 61 bilioni kuna tofauti ya dola milioni 55, sasa basi tukapendekeza kwamba 55 milioni dola je, hizi pesa haziwezi kweli kununua tanki la kusafirisha gesi kupeleka Mwanza? Hatuwezi kuchimba vile visima vya gesi tu-*store* gasi kwenye visima hivyo kitu ambacho kinawezekana ikiwa hilo bomba bado halijakamilika? Sasa tujiulize Februari hiyo hapo 2008 tutafanya nini mwaka mmoja ukimalizika?

Mheshimiwa Spika, kwa hivyo hii *power system master plan* ina umuhimu mkubwa wa kuharakishwa ili mipango hiyo yote tui-cooperate ili tuepukane na hili tatizo la *shortage* ya umeme. Itakuwa ni aibu kila mwaka kuwa na mipango ya dharura. Hivi sasa wenzetu Kigoma wana shida kubwa sana ya umeme wanatumia genereta na gesi *naturally* tunayo hapa na ndio njia rahisi, nako tukakodi mitambo ya diesel! Tulikuwa na mpango wa kujenga line kubwa ya umeme au kujenga hizi gesi walls lipi ni rahisi? Hili ni suala la engineering, wataalam tunao wafanye mahesabu ili tuondokane na tatizo hili.

Mheshimiwa Spika, baada ya suala hilo la power sister master plan, ninaomba nizungumzie suala la *TPDC*. Ukurasa wa tisa na wa kumi wa taarifa hii ya Kamati imezungumziwa masuala mengi yanayohusu *TPDC* pamoja na hayo ni kuhusu masuala la hifadhi ya mafuta. Ninaamini *TPDC* imeshapeleka mapendekezo Serikalini kuanzia siku au mwaka jana walipotakiwa Tanzania tuwe na hifadhi ya mafuta ili wamiliki biashara na kupunguza hizi kodi zinazoongeka kila siku katika biashara ya mafuta. Ninaamini *TPDC* imeshapeleka mashauri na ninaamini katika mashauri waliyopeleka *TPDC* kuna hii njia ya *BOOT system (Build Own Operate Transfer).* Njia hii haina mzigo kwa Serikali,

Serikali haina haja ya kutoa fedha ni njia ambayo mwekezaji ata-*finance* mradi wote atatuletea mafuta ya kutosha halafu anaweza akajikata pesa zake kwa njia ya kodi ya mafuta, sasa kwa nini mpaka leo hatujapata majibu? Ninaomba Mwenyekiti wa Kamati suala hili alifuatilie kwa karibu. Haya masuala ambayo hayana haja ya kuchukua muda mrefu na tukichukua muda mrefu ni hasara kwetu. Ninaomba Kamati ishauri Serikali wayatekeleza haraka haraka.

Mheshimiwa Spika, mwisho sasa niende ukurasa wa nne wa taarifa hii ya Kamati. Katika ukurasa wa nne wa taarifa hii ya Kamati kuna suala hili la *Richmond*. Suala limeleta matatizo, suala limezungumziwa kwenye vyombo vya habari, Bunge letu kidogo lilikuwa linanung'unikiwa, watu wanalalamika kwa nini hatujachukua hatua zinazofaa lakini at least leo tuko hapa na suala la Richmond linazungumziwa hapa.

Mheshimiwa Spika, katika ripoti hii ya Kamati, imeeleza sababu nyingi sana pamoja na TAKUKURU kuchunguza lakini bado zipo sababu nyingi ambazo suala hili bado ufumbuzi haujakamilika. Kwa vile TAKUKURU kama inavyozungumza ripoti ya Kamati waliangalia upande wa kijinai tu lakini kuna masuala mengi yamejitokeza.

Mheshimiwa Spika, taarifa zilizopo ni kwamba kuna matatizo mengi yaliyojitokeza na ninaomba niwe *analytically* kidogo na univumilie na uniruhusu kidogo kutizama baadhi ya data. Mradi huu uliogharimu dola za Kimarekani milioni 134 na katika bajeti ya mwaka jana nilipozungumzia hivyo Waziri wa Nishati na Madini akatoa ufafanuzi akasema zile dola milioni 134 siyo gharama halisi akataja gharama halisi zilikuwa ni dola milioni 102 kwamba kulikuwa na dola kama milioni 34 ni kwa ajili ya manunuzi ya gesi. Hata hivyo, tukitizama muda wa mradi huu ambao ulitakiwa ukamilike haikuwezekana, hivi sasa ni miezi 16 umekamilika tarehe 03 Oktoba. Kuna c*lause ya liquidated damages* ambayo imezungumziwa kwamba yule Mkandarasi kama hakukamilisha muda unaohitaji basi atalipa dola 10,000 kwa siku. Sasa tukitizama hii *clause* tunajikuta tunaingia matatizoni zaidi. Mradi huu tukilinganisha megawati 100 hizi za Richmond na *megawati* 100 za mradi wa Serikali wa WASIRA na zote zinatumia gesi asilia umezidi kwa gharama ya ziada ya dola milioni 54.

Mheshimiwa Spika, sasa ukitizama hata kama hiyo damages ya liquidated damages tukilipwa basi tuta-*recover* dola milioni 2.4 bado tuna pengo, tumekula hasara ya dola 52 milioni au kama Mheshimiwa Naibu Waziri alivyosema tukitoa zile gharama za mafuta bado tutakuwa na pengo la dola milioni 22 ambazo takriban ni bilioni 29. Hata wakilipa hao *DOWANS* basi tuta-*recover* milioni mbili.

Mheshimiwa Spika, sasa hapo ndipo tuna matatizo katika mikataba yetu na hapa niungane na Mheshimiwa Rais ni kweli ni lazima mikataba iwe *reviewed*, tuna matatizo kwa sababu sisi tumekula hasara. Dola milioni mbili maana yake nini tumeshapoteza tumepoteza, mradi ulitaka kuchukua miezi sita umechukua miezi 16 ambao tungelinganisha na ule mradi wa Serikali wa WASIRA ambao ulikuwa unachukua miezi 14 tungepunguza hayo matatizo yote hayo, tungepunguza gharama zote hizo, sasa kwa nini tuendelee na kula hasara?

Mheshimiwa Spika, kuna matatizo hata huo mkataba wenyewe ulisainiwa kwa mazingira ya matatizo matatizo. Mkataba unasainiwa usiku, Wizara ya Nishati ya Madini haieleweki aliye-*draft* mkataba *tender board* inazuiliwa, *tender board* walishakataa hapo hapo wanaambiwa leteni majina, tender board ilikuwa tayari hizi kampuni nane walizikataa zote kwamba hawakutimiza viwango lakini hapo hapo wanaambiwa wapeleke majina ya kampuni hizo hizo na baadaye anachaguliwa mtu katika kampuni hizo hizo, hii kidogo ni tatizo na hayo ndiyo yanaongezea utata na kuhalalisha kwamba iko haja ya kuungana na Kamati hii ya Uwekezaji wa Biashara ya kuunda Kamati Teule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nije katika viwanda, Serikali imebinafsisha viwanda vingi lakini kwa bahati mbaya kuna viwanda mpaka hivi leo vilivyobinafsishwa havijafanya lolote na wafanyakazi waliokuwemo katika viwanda hivyo wengine hawakupata mafao yao na ni matatizo mapevu. Vipo viwanda mfano *Mkata Saw Mill, Steel Rolling* vya Tanga, Sasa hebu tujiulize mikataba gani hii ya ubinafsishaji ikiwa kiwanda hiki ambacho kinatoa ajira kwa watu wetu leo tunakibinafsisha?

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Kama nilivyotamka awali, wamejitoa wachangiaji wawili lakini bado tunao 12 na muda uliosalia kwa kweli hautoshi kabisa. Kwa hiyo, nimetoa kipaumbele kwa wale ambao ninawaona ukumbini, najua wengine inawezekana kisingizio ni kwamba wapo kwenye Kamati lakini nimeona ni vema hawa waliovumilia kuwemo ndio niwatangulize. Kwa hiyo, orodha yangu saa 11 .00, tutaanza na Mheshimiwa Kabuzi Rwilomba, atafuatia na Mheshimiwa Mhonga Said Ruhwanya, Mheshimiwa Christopher Olonyokie Ole-Sendeka ambaye naye ametoka sasa hivi tena, Mheshimiwa Mariam Reuben Kasembe, Mheshimiwa Dr. Binilith Satano Mahenge, Mheshimiwa Dr. Guido Gorogolio Sigonda na ninadhani tutamalizia na Mheshimiwa Eng. Laus Omar Mhina. Nina orodha ya ziada hapa lakini tutaiona itaendaje saa hizo nyingine. Kwa sasa Waheshimiwa Wabunge nasitisha shughuli za Bunge hadi hapo saa 11.00 jioni.

*(Saa 07.00 Mchana Bunge lilifungwa mpaka saa 11.00 jioni)*

(*Saa 11:00 jioni Bunge lilirudia*)

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaanza na Mheshimiwa Kabuzi F. Rwilomba atafuatiwa na Mheshimiwa Mhonga S. Ruhwanya na wakati huo ajiandae Mheshimiwa Christopher Olonyokie Ole-Sendeka.

**MHE. KABUZI F. RWILOMBA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi nami nichangie hoja iliyo mbele yetu.

Kama ilivyo ada, naomba nianze kwa kutoa pole kwenye familia ya Marehemu Ndugu yetu Mheshimiwa Salome J. Mbatia, aliyetuacha na pia ninapenda kutoa pole kwa wananchi wangu wa Jimbo la Busanda, Kijiji cha Ntono na Rwamgasa ambao walipata maafa ya nyumba zao kuezuliwa na upepo mkali wakati wa mvua. Nawapa pole sana, nawaahidi kwamba nami wiki ijayo nitakuwa nao ili tuweze kusaidiana katika matatizo.

Baada ya utangulizi huo, nianze na kumpongeza Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Uwekezaji na Biashara. Kazi yao ni nzuri wamefanya kazi nzuri na wametembelea sehemu nyingi ingawa hawakuweza kufika eneo langu katika Jimbo langu na katika Mkoa wangu. Lakini inatupa matumaini kwamba watafika safari ijayo kama walivyoahidi.

Niwapongeze vilevile Wanakamati kwa kazi waliyoifanya. Wamefanya uchambuzi wa kina ila ninapenda kuanza na kuwaomba wajaribu kutoa mwelekeo katika hili neno la uwekezaji. Maana sisi tuna wawekezaji wa madini, kuna watu wanakuja wanaweka viwanda, sasa kuna wawekezaji na wavunaji, ninapenda nielewe. Kwa mfano, mtu kama una msitu wako umeukuza vizuri wewe huna mashine ukamwita mtu akaja na mashine na mashoka akavuna akauza halafu akakupa kidogo sasa huyo utamwita ni mwekezaji au mvunaji? Maana yake kama ni mwekezaji inabidi aweke vitu vingi vya kudumu katika maeneo hayo. Mimi nasita sana kuwaita wawekezaji na nikiona katika nchi yetu, wawekezaji mnaowaita wawekezaji na watu ambao tunasema ni wenye fedha vitu walivyoviweka vingi ni kama vya ku – *process* tu yaani vya kuchukua. Utakuta ameweka *godown* kubwa kama hili wanasema mwekezaji lakini ana-*process* anapeleka.

Sasa nafikiri Kamati hii tungeomba itusaidie kutueleza nani mwekezaji hasa na nani mchukuaji. Matajiri wengi katika nchi yetu unakuta ni wale wanaochukua na wengine wanaojifanya wanaingia ubia na wale wengine unakuta wakati mwingine ni walewale na wenyewe ni wachukuaji wanajifanya ni wenzetu lakini na wenyewe ni wachukuaji. Sasa basi, naomba Kamati hii ijaribu kuzisaidia Wizara hizi na itusaidie kwa sababu hii ni Kamati nyeti katika masuala ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, Kamati imeangalia masuala ya madini ingawa ilijikita sana katika eneo la *TANZANITE*. Imetoa wazo zuri kwamba *TANZANITE* ni vizuri ichimbwe na wazawa yaani na Watanzania , wafanye kazi hiyo kwa sababu inawezekana hakuna haja ya kuleta watu wa nje na mimi nakubaliana na hilo.

Mheshimiwa Spika, ningewashauri kwa kuwa wameahidi kutembelea maeneo mengine basi wafike mpaka Geita, kule kuna wachimbaji, Nzega, Musoma na sehemu nyingine katika nchi yetu. Wajaribu kuangalia na kutoa ushauri na kitu kizuri walichokiona wameweza kuona kwamba mahali ambapo kuna migodi wananchi kwa kweli wameachwa kama hakuna chochote, hicho ni kitu kizuri wamekiona. Lakini ni vizuri waende kwa undani zaidi, wazalendo watashirikishwaje katika uchimbaji huo? Watashirikishwa kwa namna gani? Mwekezaji anapokuja kuwekeza anashirikishaje wazalendo? Hilo ni muhimu sana kuliangalia.

Mheshimiwa Spika, wamezungumzia wachimbaji wadogo, nawashukuru sana wamelizungumzia hilo. Lakini wachimbaji wetu wadogo bado hatujawaangalia vizuri sana nashukuru sana sasa hivi Serikali imeanza utaratibu mzuri. Kwangu kuna sehemu ambayo Serikali imefanya kazi kidogo, imewapa eneo la Rwamgasa, wamewaomba wachimbaji wakubwa wamewaachia eneo ambalo la kuchimba, ni hatua nzuri. Lakini ni sehemu ndogo sana waliyopewa na kuna sehemu nyingi ambazo wanahitaji msaada hawa wachimbaji. Sehemu za Nyarugusu bado na *Matabi Barrick* iliachia eneo ili wachimbaji wadogo waingie lakini inasikitisha kwamba bado Serikali haijaamua kuwapa lakini *off course* Wizara ya Nishati na Madini imeshaaamua, imeiomba Wizara ya Maliasili na Utalii iruhusu sasa tunasikitika kuona kwamba ombi ambalo limetoka kwenye Wizara nyingine linachukua mwaka mzima, hilo ndiyo linaleta taabu. Tunaomba Serikali basi ifanye haraka wananchi wale waanze kuchimba. Kwa sababu kama *Barrick* watu wa nje wamekubali kuwapa, waruhusuni na ninyi muwe na huruma kama *Barrick.* Kwanza Mzungu kuona huruma kwa Mwafrika halafu wewe Mbantu mwenzako ukaanza kuona kigugumizi, sio vizuri. Kwa sababu eneo lile limeshaharibiwa sasa hivi ni wachoma mkaa na watu wanaolima viazi na mahindi pale, sasa waruhusuni wachukue eneo hilo kama nia ya Serikali ni njema waruhusuni basi wapewe eneo hilo.

Mheshimiwa Spika, twende zaidi hata hao wawekezaji, waombeni hata wawekezaji wa *GGM,* wamechukua eneo kubwa sana pale Geita Mjini, Nyamongo, nafikiri ni hivyo hivyo, wamechukua eneo kubwa sana sehemu ambayo hawawezi kufanyia kazi, kwa nini wasiwape wachimbaji wadogowadogo? Sehemu zenye matagata waachiwe wachimbaji wadogo wadogo wa Geita na wenyewe wafurahi, hapo mtakuwa mmelisha pua kuliko kulisha mdomo na hao wachimbaji wadogo wadogo ndiyo wetu watakaobaki hapa. Kwa hiyo, nina maombi hayo kuwa Kamati hii ikienda ijaribu kuliona hilo na kuweza kuwaombea wachimbaji wangu waweze kupata sehemu ya kufanyia kazi, naomba sana.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Kamati hii ni ya uwekezaji labda ninaomba twende zaidi kwenye upande wa mazao. Kuna zao ambalo limekuwa linaonekana na mara nyingi nimekuwa nikiuliza kwamba kuna zao la matunda, Lushoto najua kuna matunda mengi sana, Morogoro pia kuna matunda, Geita pia kuna matunda mengi sana kama mananasi tena mazuri sana na tikiti maji nyingi sana za kutosha za kuweza kuendesha kiwanda. Sasa sijui Kamati, hili inalionaje? Tunahitaji uwekezaji wa viwanda, tutaendelea kupokea *juice* za kutoka Afrika Kusini na hata Kenya, kwa nini zisisindikwe hizi *juice* zetu hapa? Maana sasa hivi watu wamepunguza hata kunywa bia utakuta ni *juice* tu na ni hela nyingi yaani dola nyingi hizi. Nadhani kuna haja ya kuangalia hilo. Maembe, nanasi, za Geita na *apple* za Lushoto zikisindikwa tutakuwa tumeingiza fedha za kigeni kwa nchi yetu na watu wetu watazidi kuneemeka na watazidi kupiga hatua.

Mheshimiwa Spika, si vema kurudia suala lakini kidogo naomba nizungumzie *Richmond*. Hii *Richmond* mimi kwanza nashindwa kuelewa tatizo lipo wapi? Kwa sababu Kanuni tunazo na wametusomea Sheria, kazi zao, Kamati hii inaangalia Wizara mbili. Mimi nashindwa kuelewa ni kwa nini Kamati hii haikuweza kumwita Waziri au mhusika na kumuuliza tatizo lipo wapi kwa sababu Kanuni zinaruhusu na kama haziruhusu basi zirekebishwe, kuna nini? Nilitarajia leo tutapata majibu mazuri kabisa kama

limesemwasemwa ndiyo maana ya Kamati kuhakikisha kwamba inafanya kazi na Wizara fulani. Kama kuna kigugumizi hawajatueleza, alibisha? Aliwaambia sitaki kuwasikiliza? Alikuwa ni *cooperative* au nini kilitokea? Kwa sababu jibu hapa lingeweza kupatikana. Sasa wamerudi wanataka nguvu yetu tena, Bunge liweke nguvu tuunde Tume na mimi nakubaliana kwamba haya tuunde Tume lakini bado nauliza ninyi mmeshindwa nini?

Mheshimiwa Spika, mimi niko kwenye Kamati ya Huduma za Jamii, lile la Russia lilipolipuka kule, jamaa wanadai mikopo na kadhalika, tulimwita Waziri, tukamwambia atuambie kuna nini? Magazeti yanasema hivi. Akatuambia ooh! Wamejipeleka. Haya, tuambie lete hizo cheki zimefanyaje, tukazichambua zile cheki tukaangalia kila kitu tukaona aaaaah! Kumbe wamekwenda kinyemela, kwa heri. Sasa hawa namna gani? Au kuna udhaifu kwenye Kanuni zetu, tuziangalie basi kama kuna udhaifu.

Mheshimiwa Spika, ninaomba sana kama Kamati hazina nguvu basi lieleweke kwamba zinaweza zisifanye kazi na Wizara au zikamwita Waziri au zikamwita Katibu Mkuu na au zikamwita Mtendaji yeyote kwenye Wizara basi tuelewe kwamba tunahitaji kurekebisha Kamati na kuangalia tena Katiba ya nchi upya. Nadhani Kanuni zinaturuhusu na walisema wanaangalia utekelezaji wa Wizara hizo, utekelezaji. Sasa kama utekelezaji umeharibika mahali fulani nadhani wanaweza wakapata jibu. Naungana nao kwa ombi lao lakini bado nataka jibu kwamba kwa nini hawakutuletea jibu wakati wa kujieleza?

Mheshimiwa Spika, mwisho, naomba Kamati ipanue wigo kutembelea maeneo yetu ambayo tupo pembezoni, tunahitaji sana sana. Nilikuwa naangalia sehemu walizofika ni sehemu ambazo kwa kweli zinaweza kupitika kwa urahisi, wawezeshwe kufika hata sehemu nyingine. Mimi eneo langu ni la wachimbaji lakini wanakwamishwa kwa sababu hawana umeme na wakipata umeme watatoa dhahabu ya kutosha na nchi hii itapata pesa. Naomba sana wawezeshwe ili waweze kufika kule na tuweze kupata maendeleo.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Faustine Kabuzi Rwilomba na sasa ni zamu ya Mheshimiwa Mhonga Said Ruhwanya ajiandae Mheshimiwa Christopher Olonyokie Ole-Sendeka.

**MHE. MHONGA SAID RUHWANYA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia Taarifa ya Kamati. Nawapongeza kwa kazi nzuri waliyoifanya lakini naungana nao kwamba taarifa hizi ziwe zinakuja kwa wakati na ikiwezekana kweli tuanze kuzijadili kila Bunge la Februari ili tuendane na wakati. Hii ni kwa sababu mambo mengi yanaweza kuwa tayari yamefanyika halafu na wao wameshaandika kwamba yalikuwa hayajafanyika.

Mheshimiwa Spika, nawapongeza vile vile kwa kuja na maswali mengi kuhusiana na Richmond. Ni kweli kwamba ilizua mjadala mkubwa sana hasa katika vyombo vya

habari na watu tulikuwa tukiulizwa maswali mengi sana ilhali tukiwa hatuna majibu na Bunge lilikuwa halijajadili chochote kabisa kuhusiana na suala hili.

Mheshimiwa Spika, kuna maswali sita ambayo Kamati hii wameuliza na mimi naomba niongezee moja. Ni nani hasa wadau wakuu wa hii Richmond ambao wameonekana kwa mfano nikisoma swali la tatu (c) la Kamati linaonyesha kwamba walishindwa kutekeleza mradi wa bomba la mafuta, ilikuwaje tena Serikali ikafumba macho ikawapa mradi mkubwa kama huo? Kwa hiyo, ni swali ambalo naomba kuuliza kwamba ni nani huyu ambaye ana ushawishi mkubwa kwa Serikali mpaka Serikali ikaona kabisa kwamba hawa watu tayari wameshafanya makosa lakini bado wakapewa tena mradi huu mkubwa?

Vilevile napenda kujua kwamba ni kwa nini Waziri mhusika hakuleta taarifa hapa Bungeni wakati bado lina moto? Tukiangalia mfano jana Waziri wa Afya alituletea taarifa ya tatizo lililotokea *MOI*, Muhimbili kwa sababu aliona ni jambo ambalo linaongelewa sana na wananchi wanaweza wakapoteza imani na hospitali ya Muhimbili. Alikuja hapa na akatutolewa hiyo taarifa, naona kama ni jambo zuri sana na Waziri alitakiwa atuletea ile taarifa mapema ili iweze kujadiliwa au kutoa tu taarifa kwamba hili suala likoje. Kwa hiyo, nitaomba niishie hapo kuhusiana na suala la Richmond kwa sababu maswali mengi sana yameshaulizwa na ninatarajia tu kupata majibu mazuri ambayo yatamridhisha kila Mtanzania.

Mheshimiwa Spika, naomba niende moja kwa moja kwenye suala la madini. Madini ni sekta nyeti sana hata Kamati imetuonyesha kwamba bado nchi yetu haijafaidi kuwepo kwa madini katika nchi hii, ni kweli bado hatujafaidi kabisa. Sekta hii inaonekana kweli haijaaleta tija katika ukuaji wa uchumi ingawa madini yenyewe yana thamani mno. Nashukuru kwamba hilo pia limeonekana lakini vilevile katika michango yangu mbalimbali nakumbuka kuna siku niliwahi kuchangia ilikuwa ni katika bajeti ya mwaka huu ya Wizara ya Nishati na Madini, nilitoa mfano wa Kongo tangu mwaka 1975 bado wao wanachimba madini lakini kwa sababu nchi nyingi za Afrika tunategemea wawekezaji kutoka nje waje wachimbe madini yetu ndiyo maana hatupati faida.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali yangu iwasomeshe Watanzania na iwekeze katika kununua mitambo ili tuweze kuchimba wenyewe na ikiwezekana tuanze kununua mashine za kutengeneza viwanda vya kukata na kusafisha na kuchunguza madini hapahapa nchini kwetu ili tuondoe utata kwamba madini yanapelekwa, maroli yanabeba kila siku wanasema wanakwenda kuchunguza lakini hawaendi kuchunguza ni kwamba yale yanakuwa tayari ni madini na wakienda wanatuambia hakuna madini yoyote na hakuna popote ambapo tunaweza kwenda kuwashtaki au kuwauliza. Kwa hiyo, ninaomba sana niishauri Serikali yangu ifanye hilo.

Mheshimiwa Spika, vilevile namshukuru Mheshimiwa Rais kwa kuamua kuunda Tume ambayo itakuwa huru na pana zaidi ambayo itawashirikisha wadau mbalimbali katika kushughulikia hili suala la Mikataba ya Madini ambayo imeonekana ina utata

mbalimbali na sitaona aibu kusema kwamba kelele za Wapinzani pia zimesaidia kwamba ameweza kutanua ile Tume.

Mheshimiwa Spika, ninachoomba ni kwamba Tume hiyo iundwe haraka ili iweze kufanya kazi kwa wakati kwa sababu tuna matatizo mengi ambayo kila mtu nadhani anafahamu kwamba madini nchini kwetu yana matatizo hasa mikataba yake ina matatizo, hivyo inatakiwa hiyo Tume iundwe haraka ili iweze kufanya kazi yake.

Mheshimiwa Spika, vilevile ninaomba niishauri Serikali kwamba kwa mfano wenzetu Ghana wana tabia ya kufanya *review* ya mikataba yao, wameshafanya mara tatu na hata Sheria zao huwa wanazibadilisha mara kwa mara hasa hizi za madini. Kwa hiyo, ninaomba tuwe na tabia ya kufanya *review*. Vilevile muda upunguzwe kwani hawa wawekezaji wa madini wanapewa muda mrefu sana kiasi kwamba wakiboronga au akiendelea kutuambia kwamba hapati faida kwa sababu tumeshaingia naye mkataba hatuwezi ku–*terminate* huo mkataba sijui kama kuna kifungu ambacho kinashauri Mkataba uweze kuwa *terminated*. Kwa hiyo, naomba sana hilo lizingatiwe.

Mheshimiwa Spika, suala lingine kuhusiana na mikaaba ya viwanda, hata hili naona Kamati wamelielezea kwamba mikataba ya mauziano ya viwanda yaangaliwe upya, viwanda vingi vimekuwa havifanya kazi yake. Wenyewe wametoa mfano wa kiwanda cha magunia na kile cha ngozi, lakini mimi nina mfano wa kiwanda cha Chumvi Uvinza kwa kweli hakijafuata mkataba unavyotaka kwa sababu walisema kwamba hawatatumia ile teknolojia ya zamani ya kutumia magogo lakini bado wanaendelea hawatumii umeme kama walivyoahidi na hata umeme wa jua hawautumii na uzalishaji wake pia unaonekana pia ni dun. Kwa hiyo, ninaomba Serikali iangalie pia hili suala.

Mheshimiwa Spika, nikifika kwenye *issue* ya nishati katika suala la umeme, naomba kwanza niwape pole wananchi wa Mkoa wa Kigoma ambao mpaka sasa hivi wanataabika hawana umeme karibia siku 40 sasa.

Mheshimiwa Spika, Kamati hii ukurasa wa nne imeonyesha umuhimu wa sekta hii kwa maendeleo ya Taifa letu na uchumi kwa ujumla. Tumekuwa tukipewa mipango mbalimbali ya muda mrefu ya umeme kwa Mkoa wa Kigoma. Mwaka 2006 tuliambiwa kwamba *ADB* tayari wamekubali kufadhili mradi ambao utaanzia Tabora mpaka Kigoma lakini bahati mbaya Waziri mpya wa mwaka huu amekuja na mradi mwingine wa *North West Grid Extension* ambao utaisha nadhani mwaka 2012 kama sikosei.

Mheshimiwa Spika, sasa ninachoomba mimi hapa ni umeme wa dharura kwa Mkoa wa Kigoma kama Mikoa mingine wanaweza wakapewa umeme wa dharura, naomba na sisi tupewe umeme wa dharura. Ni adha kubwa sana wananchi wanapata kwa sasa hivi mashine inayofanya kazi ni ile inayopeleka umeme katika hospitali ya Mkoa angalau watu waweze kufanyiwa operation lakini watu wote wa Manispaa wako gizani zaidi ya siku 35 sasa. Pamoja na kwamba Mheshimiwa Rais siku ya Mkutano Mkuu alisema kwamba anatambua hilo, alishauri kwamba kuna mashine ambazo ziko Mwanza zilikuwa ni za umeme wa dharura, ninaomba Kamati hii au nikikuomba mwenyewe

Mheshimiwa Spika utusaidie basi kumwambia Waziri kumkumbusha kwamba Rais alisema kuna mashine ambazo ni za dharura zilipelekwa Mwanza zinaweza zikapelekwa Mkoa wa Kigoma kwa sababu wao tayari wana umeme wa gridi ya Taifa. Tunaomba sana kwani wananchi wanateseka.

**SPIKA:** Waziri anakusikia. (*Kicheko*/*Makofi*)

**MHE. MHONGA SAID RUHWANYA:** Mheshimiwa Waziri amesema anaweza kwenda Kigoma ni jambo zuri na kitu kikubwa ninachokiomba mimi hapa ni umeme wa dharura kwa sababu mipango ya muda mrefu kweli tumeiona kuna huu wa *MCC*.

Mheshimiwa Spika, lakini nina ushauri mwingine kuhusiana na huu mpango wa *ADB*. Naomba huo mpango uendelee na washirikiane na *MCC* ili kutuletea huo umeme wa muda mrefu hata ukiwa mwingi tunaweza kuuza nje ya nchi vilevile

Kwa hiyo, mimi naomba sana zile mashine ambazo ziko Mwanza ziletwe Mkoani Kigoma na huo mpango wa kuendelea kutengeneza vipuri kama mlivyojibu swali namba 28 la Mheshimiwa Peter Serukamba unaonekana utachukua muda mrefu kwa sababu mmesema kwamba mmesaini mikataba na hawa *Anglo-Belgium Cooperation* mpaka 2009 ina maana mpaka hivyo vipuri vije vifungwe mwaka huo wa 2009 ni muda mrefu sana. Ninaomba tu hizo mashine za dharura zije kwa kweli kwa sababu kuna watu wengi sana ambao wanategemea umeme katika kuendesha maisha yao.

Mheshimiwa Spika, unga wenyewe umepanda bei kwa sababu hakuna mashine za kusaga, wanaosaga ni wale wenye mashine za mafuta ya taa au za mafuta ya dizeli. Kwa hiyo, ninaomba sana hicho ndiyo kilio kikubwa kilichonisimamisha mimi hapa pamoja na kwamba Mheshimiwa Waziri umesema unalijua sana na unalitatua lakini ninakuomba kwamba ikiwezekana zile mashine ambazo ziko Mwanza zipelekwe Kigoma.

Mheshimiwa Spika, naomba kuishia hapo na ninashukuru sana kwa nafasi hii.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mhonga Said Ruhwanya na sasa namwita Mheshimiwa Christopher Olonyokie Ole-Sendeka, wakati huo huo atafuatiwa na Mheshimiwa Mariam Reuben Kasembe na Mheshimiwa Dr. Binilith Satano Mahenge ajiandae atakuwa msemaji wa tatu.

**MHE. CHRISTOPHER OLONYOKIE OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nichukue nafasi ya awali kabisa kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia mchana huu.

Mheshimiwa Spika, Lakini nichukue nafasi hii tena kama walivyofanya Waheshimiwa Wabunge wenzangu, kwa niaba ya wananchi wa Wilaya ya Simanjiro kukupa wewe salamu za rambirambi na Bunge lako Tukufu pamoja Rais wetu na wananchi wa Mkoa wa Kilimanjaro na Watanzania kwa ujumla kufuatia kifo cha dada yetu, Naibu Waziri wa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, Marehemu

Salome Joseph Mbatia na nimwombe Mwenyezi Mungu aiweke roho ya Marehemu mahali pema peponi, amin!

Mheshimiwa Spika, ninapenda pia kuwapa pole wale wote waliopata ajali wakiwemo Mawaziri wetu na Wabunge wenzetu na kwa kweli pia kuwapa pole na salamu za rambirambi wale ambao katika ajali hizo waliweza kupoteza ndugu zao.

Mheshimiwa Spika, kazi iliyopo mbele yetu leo ni kujadili Taarifa ya Kamati ya Bunge ya Uwekezaji na Biashara ambayo nakushukuru sana kwa kuniteua mimi wakati ulipokuwa unaunda Kamati kuwa mmoja wa Wajumbe wa Kamati hiyo.

Mheshimiwa Spika, lakini kabla sijaenda moja kwa moja kwenye kuchangia, wananchi wa Wilaya yangu watashangaa sana nisipochukua nafasi hii kuwapongeza Wabunge wenzangu wakiongozwa na Katibu Mkuu wa Chama cha Mapinduzi kwa kura nyingi za kishindo walizozipata katika uchaguzi uliofanyika Kizota. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini nampongeza Mwenyekiti wa Chama chetu na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Jayaka Mrisho Kikwete na Makamu wake wote wawili kwa kura nyingi walizozipata katika mkutano wa Kizota ambao unaonyesha jinsi ambavyo wanachama na Watanzania wana imani kubwa na uongozi wa Mwenyekiti wetu ambaye pia ni Rais wa nchi yetu na ndiyo maana amepata kura za kishindo.

Mheshimiwa Spika, baada ya pongezi hizo, wakati nilipokuwa nikichangia kwenye Bunge lililopita, yapo mambo ambayo yanahusiana na yale yaliyozungumzwa na Kamati ya Uwekezaji na Biashara ambayo nilileta kama kilio cha wananchi wa Jimbo langu la Simanjiro na nina heshima kutambua usikivu wa Serikali ya Awamu ya Nne kwa kuyashughulikia baadhi ya mambo ya msingi ambayo niliyawasilisha hapa.

Mheshimiwa Spika, kupitia kwa Waziri wa Nishati na Madini, napenda kuishukuru Serikali kwa kutenga au kutoa eneo la Kitalu *'A' Extension* katika machimbo ya *TANZANITE*, Mererani na kuyagawa kwa wachimbaji wadogo zaidi ya 800.

Mheshimiwa Spika, wachimbaji wadogo walikuwa wanahitaji maeneo ya kuchimba na Serikali yao imesikia kilio chao lakini najua haitoshi bado wanahitaji maeneo lakini nisiposhukuru kwa hilo nitaonekana sawa na mwizi wa fadhila. Hii ni pamoja na umeme wa Ngage ambao Mheshimiwa Nazir Mustafa Karamagi aliahidi kwamba atashughulikia na kuhakikisha kwamba umeme ule unarudi mahali palipokuwa pamepangiwa mwanzoni.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nina maeneo mawili tu ambayo ninapenda kuchangia katika taarifa ya Kamati ya Uwekezaji na Biashara na ninapenda kuchangia kwa ufupi. Katika suala zima la mikataba ya Madini, Rais wetu alituelekeza wazi kwamba ni vizuri wawekezaji hawa wakanufaika na sisi Watanzania tukanufaika.

Kwa maana hiyo, suala la kutazama mikataba ya madini ili iweze kuendelea kuwanufaisha Watanzania, ni jambo muhimu sana. Suala la kuweka makubaliano kwenye *Memorandum of Understanding* ili kuhakikisha kwamba Halmashauri zetu za Wilaya zinakuwa na hisa na Makampuni yanayowekeza katika sekta ya madini katika Wilaya zao, ni jambo muhimu na lingetakiwa lisiwe jambo la hiari bali ni jambo ambalo lingewekwa katika makubaliano *(MOU)* zetu za madini ili Halmashauri zetu ziweze kunufaika na raslimali hiyo. Kwa kufanya hivyo, suala la ajira pia liwe ni jukumu la msingi kwa watu wanaozunguka maeneo hayo ya migodi ili kuweza kuinua kipato cha Watanzania katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, ninapenda pia kuungana na Kamati ya Uwekezaji na Biashara katika pendekezo la kuundwa kwa Kamati Teule ya Bunge ya kushughulikia suala la *Richmond*. Wako wenzetu ambao wamechangia awali ambao wamekuwa wakisema ni kwa nini pengine tumefika mahali tukapendekeza haja ya kuundwa kwa Kamati Teule ya kushughulikia suala hili. Kwanza ni vizuri ieleweke wazi kwamba Serikali ya Awamu ya Nne iliangalia tatizo lililokuwepo la dharura ya kukosekana kwa umeme na ikaona haja ya kuingia ubia au kuwatafuta wawekezaji wanaoweza kuwekeza katika upatikanajiwa umeme wa dharura. Lakini si Richmond peke yake wala *DOWANS* ambao walipewa, wengine walipewa kama *AGGREKO* na wengineo na waliweza kuzalisha umeme kwa wakati. Moja kati ya suala lililopelekea Kamati ya Uwekezaji na Biashara kuona haja ya kuundwa kwa Kamati Teule ya Bunge ni kukosekana kwa uwazi katika suala zima la Mkataba wa *Richmond DOWANS*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Rais wa Jamhuri ya Muungano alipokuwa akifungua Bunge letu alisema maneno haya na ninaomba kununukuu:-

“Ninyi Waheshimiwa Wabunge ndiyo macho na masikio ya wananchi, mmeaminiwa na kuheshimiwa. Naomba kila siku mnapoingia na kutoka katika Bunge hili, mnapozungumza humu ndani au mnaposikiliza wengine wakizungumza, mnapokuwa macho au mnapofumba macho kwa kutafakari kwa kina, kila mmoja akumbuke imani na heshima hiyo kubwa mliyopewa na wananchi ”.

Mheshimiwa Spika, tumepewa jukumu la kuwawakilisha Watanzania wenzetu kuwa macho na masikio yao na imani hii ni kubwa sana. Ttunapofika mahali pa kutumia haki yetu tuliyopewa kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, katika Ibara ya 63(2) ya kuweza kuisimamia na kuishauri Serikali ikiwa ni pamoja na kutaka kuona Mikataba hii, hii Serikali inapata kigugumizi. Walipata kigugumizi kwenye Kamati yetu na tukaona kwamba hapa ndiyo mahali pakee iundwe Kamati Teule ili haya mambo yaweze kufahamika kwa uwazi zaidi. Sababu nyingine zimeainishwa zaidi ya sababu sita na maswali sita ambayo yalitakiwa kujibiwa yapo pale kwenye ripoti ya Kamati ya Uwekezaji na naungana nazo kabisa. Lakini ukungu zaidi unazidi kuingia au utata pale ambapo baadhi ya ripoti nyingine za *TANESCO* zenyewe zinapobainisha mashaka zaidi wakati wa zabuni ya kupatikana kwa kutolewa kwa tendahii kwa Richmond na baadaye kwa dada yake *DOWANS*.

Mheshimiwa Spika, ukisoma ripoti ya *TANESCO* ya *Procurement Contract and Perfomance Audit* , utaona wazi kabisa kwamba wakati Bodi ya Zabuni ilipokuwa

inakutana kulikuwa na kuingiliwa kwa uhuru wa Bodi yenyewe kufanya maamuzi. Ukiendelea zaidi ,wakati dharura ya umeme imekwisha na yule *Richmond* ameshindwa kutoa umeme kama ilivyokuwa inatakiwa bado iliwezekana kuhamisha mkataba kutoka Richmond kwenda *DOWANS* kinyume na mkataba wa awali inavyosemekana katika ripoti hii.

Mheshimiwa Spika, kwa ruhusa yako, naomba tu ninukuu baadhi ya maeneo katika *report* ya *PPRA* ili kubainisha utata uliokuwepo na ambao unalishawishi Bunge hili liunde Kamati Teule ili iweze kuujua ukweli na kuweza kuwaambia Watanzania ukweli juu ya Mkataba huu. Ripoti hiyo inasema hivi:-

"*Emergency Power Supply - Richmond Development Company LCC, with regard to tender PC 010/2006 for emergency Power Supply from Rental Gas Base Generating Plant of 100MW in Dar es Salaam, the tender Board at its meeting held on 28 and 29th March, 2006, disqualified all bids and decided to retain to eight bidders who submitted bids and in addition include five new friends in the power rental business following non responsibleness of the previous eight bidders. But on 4th April, 2006, the Chairman of the Tender Board received instructions from the Board of Directors, in response to directives from the Government to recall for eight bidders and get clarification for the submission bids with the purpose of finding a possible bidder that could deliver same plan successful. This was clear interference with the tendering procedures and was not consistent with the Public Procurement Procedures". (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukiendelea mbele kwa kuwa muda umekwenda, utabaini wazi kabisa kwamba inasema *contract between Richmond Development Cooperation and TANESCO did not provide for reassignment of the contract to DOWANS but subtracting arrangement however political influence force TANESCO to waiver from the principles of the contract*.

Mheshimiwa Spika, unahitaji nini zaidi ukishapata mashaka kama haya na hii ni ripoti iliyotolewa na *TANESCO* yenyewe ambayo ni *Auditing Report*.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, tulipowahoji Bodi ya *TANESCO* walibainisha wazi kwamba kulikuwa na mashinikizo. Lakini mbaya kuliko yote ni kwamba *Richmond* haikuwa na uwezo lakini ilipewa *tender*. Tunataka kujua ukweli juu ya jambo hili. Mbaya zaidi ni kwa Wizara kutotoa ushirikiano kwa Kamati ya Uwekezaji na leo kuiingiza Serikali na wananchi hasara ya kuundwa kwa Kamati ya kujua ukweli juu ya jambo hili ambalo lingeweza kuishia kwenye Kamati ya Uwekezaji na Biashara. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ningependa kuchukua nafasi hii kusema kwamba hatufurahii wala hatupendelei kuundwa kwa Kamati Teule, lakini tunalazimika ili kuweza kuunda wajibu wetu wa msingi wa kuiona mikataba ile kwa niaba ya Watanzania na kuwaeleza Watanzania ukweli.

Mheshimiwa Spika, nataka niunge hoja mkono kabla sijapigiwa kengele ya pili na niunge mkono pendekezo la kuundwa kwa Kamati Teule ya Bunge. (*Makofi*)

**MHE. MARIAM R. KASEMBE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kuchangia hoja hii iliyo mbele yetu, hoja ya Kamati ya Uwekezaji na Biashara. Kwanza kabisa niungane na wasemaji wenzangu waliotangulia kwa kuipongeza Kamati hii kwa taarifa nzuri ambayo wametuletea hapa, kwa kweli ni taarifa nzuri, inayoeleweka ambayo imegusa maeneo ambayo kwa kweli tulikuwa tunatafuta majibu na naamini kabisa mambo mengi leo tunaweza tukayapatia ufumbuzi hapa.

Mheshimiwa Spika, niipongeze Kamati hii kwa ziara ambazo wameweza kuzifanya katika Mikoa ya Arusha, Dar es Salaam, Tanga, Mtwara, Lindi, Manyara na Iringa. Naamini kabisa wasingeweza kutembelea katika Mikoa hii taarifa hii tuliyoletewa hapa leo pengine ingekuwa na upungufu au isingeweza kujitosheleza, lakini kwa ziara yao hii imeweza kuleta matunda mazuri kwani imeleta taarifa nzuri ambazo sasa hivi tunaendelea kuzijadili hapa.

Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii na mimi niungane na Kamati hii kwa kuwashukuru kabisa kwa kutembelea Mikoa ya Mtwara na Lindi kwa sababu wamefika na wameangalia kero hasa zinazotugusa sisi kwenye Mikoa ya Mtwara na Lindi hususan kwenye suala la viwanda vya korosho. Kwa kweli nimefurahi sana kuona kwamba Kamati hii ilipofika kule imeweza kutembelea kwenye viwanda hivi na kuona hali halisi ya suala zima la korosho katika mikoa yetu hii.

Naamini kabisa mapendekezo waliyoyatoa hapa ya kuwawezesha wenzetu ambao Serikali iliweza kutoa upendeleo na kuwawezesha kununua viwanda hivi kama watawezeshwa na Serikali kupata mikopo kwa kweli wanaweza kutusaidia sana juu ya zao letu la korosho kwa sababu mpaka hivi sasa tayari Serikali imekwishatuandalia mpango mzuri wa kuweza kutusaidia katika ununuzi wa korosho lakini mpango huu mzuri unaweza kuwa mzuri zaidi endapo viwanda hivi vinaweza kupewa mikopo ili waweze kubangua korosho na kuzipeleka nje ya nchi korosho zilizobanguliwa ili kuongeza pato la Taifa na kutuletea tija sisi wakulima wa korosho.

Mheshimiwa Spika, vilevile kwa kuwawezesha wenye viwanda hivi naamini kabisa kama wataweza kubangua korosho, ajira zitaongezeka kwa akinamama na vijana kwa mikoa yote inayolima korosho. Hivyo basi, naiomba Serikali waweze kufikiria ombi hili walilolitoa kwenye Kamati hii ili waweze kuwawezesha hawa ambao sasa hivi wanamiliki viwanda hivi lakini uwezo wao wa kujiendesha ni mdogo.

Mheshimiwa Spika, vilevile nimefurahi sana kuona Kamati hii walipofika Lindi waliweza kutembelea katika mashamba ya chumvi. Chumvi ni kitu kinachodharaulika lakini ni kitu ambacho kila binadamu anakitumia kila siku. Sasa kuna jambo la ajabu limejitokeza mwaka huu kwenye mikoa yetu ya Kusini, chumvi imepanda maradufu. Chumvi ilikuwa inauzwa kilo sh. 200/=, lakini tulipomaliza kikao cha bajeti tuliporudi

majimboni tulikuta chumvi imefikia mpaka sh. 1,200/=, kitu ambacho hakijawahi kutokea toka tupate uhuru kwa mikoa yetu ya Kusini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hii inasikitisha sana. Tulipokuwa tunafuatilia kujua ni kwa nini chumvi imepanda, tuliambiwa kwamba vilevile bidhaa ya madini joto imepanda, hivyo, wenye mashamba ya chumvi wanalazimika kuiuza kwa bei ghali mno. Kwa hiyo, naiomba Serikali iangalie hawa wanaofanya biashara ya madini joto ni kwa nini wamepandisha madini joto kwa kiwango kikubwa na kuwasababishia wananchi wetu kushindwa kumudu kununua chumvi. Nasema hivyo kwa sababu kule kwetu kuna kutengeneza chumvi ya kienyeji. Tumerudi safari ile tumekuta akina mama wamerudia tena kwenye mambo ya miaka ya 47 ya kutengeneza chumvi ya kienyeji ambayo haina hata madini joto. Hii ni hatari kwa sababu baadaye inaweza kutuletea ugonjwa wa *goitre* kwa ajili ya kukosa madini joto. Naiomba sana Serikali iliangalie suala hili, nimesema suala la chumvi ni dogo lakini hii ni bidhaa ambayo inatumika kila siku.

Mheshimiwa Spika, nimesema naipongeza hii Kamati kwa sababu kwenye mapendekezo yake wao wamesema kwamba wanaishauri Serikali kuwawezesha wenye mashamba ya chumvi ili waweze kupata mashine za kusindika chumvi. Naamini kabisa nao kama wataweza kusaidiwa kupewa mashine za kusindika chumvi ajira vilevile zitaongezeka lakini tutapata chumvi iliyo bora ambayo haitaweza kutuleta matatizo kiafya. Naweka msisitizo kuomba suala hili nalo lifikiriwe waweza kupatiwa hizo mashine ili waweze kusindika chumvi. Inachekesha sana Mikoa yetu tunavuna chumvi kwa wingi lakini madukani tunakwenda kununua chumvi ya kutoka nje. Tunanunua chumvi ya kutoka nje kwa sababu hawa wakulima wetu wa mashamba ya chumvi hatujawasaidia wala kuwaboresha. Kwa hiyo, bidhaa zao zinaonekana hafifu, tunakimbilia kununua chumvi zinazotoka nchi za nje. Tunaomba sana Serikali iwaangalie wakulima hawa wenye mashamba ya chumvi ili nao waweze kuboreshwa.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo nimeliona katika taarifa hii, naomba nichukue nafasi hii kuipongeza Serikali pamoja na hao wenzetu wa *ATUMAS* kwa jitihada kubwa wanazozifanya kuhakikisha kwamba Mikoa ya Kusini tunaweza kupata umeme wa kutosha lakini bado naiomba Serikali iweze kutia msisitizo kwa hawa *ATUMAS* kwa sababu sasa hivi tunahesabika kwamba Mikoa ya Mtwara na Lindi tunapata umeme huu wa Mnazibay. Lakini ukweli ni kwamba umeme huu bado haujaenea katika Wilaya zetu zote. Naomba sana Serikali itie msisitizo ili waweze kuharakisha kufanya shughuli zao na sisi tunufaike kupata umeme huu katika Wilaya zote za Mikoa ya Mtwara na Lindi na Mikoa mingine kadhalika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo naomba pia nichangie ambalo lipo katika taarifa hii ni suala la Mtwara *Corridor*. Hili ni suala ambalo limeandaliwa vizuri na tunaishukuru Serikali na tunaamini kwamba litakapokamilika litachochea maendeleo katika Mikoa yetu ya Kusini. Kwa hiyo, naiomba sana Serikali kwa sababu tunaporudi majimboni tunapata maswali kuhusu suala la Mtwara *Corridor,* hadi hivi sasa limefikia hatua gani na sisi tunajitahidi kujibu kwa kadri tunavyoweza, lakini naomba Serikali iweze nayo kuweka msisitizo ili yale ambayo yanaweza kuonekana dhahiri kwa

wananchi basi yaendelee kufanyika ili wao wenyewe wajionee kwa macho ili wapunguze kuuliza maswali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nataka nami nichukue nafasi hii kuungana na wasemaji wenzangu wote waliozungumza kuhusu suala la *Richmond*. Naungana nao na nakubaliana nao kwamba ipo haja ya kuunda Kamati hii ili tuweze kupata majibu sahihi juu ya suala hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo narudia tena kuipongeza Kamati hii na naomba Kamati zingine nazo zitakapokuwa zinapanga ziara, basi zifikirie pia kwenda Mikoa ya Kusini. Naamini zikienda kuna mambo mengi watakayojionea wenyewe na tutaweza kusaidiana kuyasemea katika Bunge hili kwa sababu hawa wenzetu wasingeweza kwenda huko haya tunayoyazungumza hapa leo tusingeweza kuyasikia au wasingekuwa na uhakika pale tunapozungumza sisi.

Mheshimiwa Spika, naomba nichukue nafasi hii kuiunga mkono hoja hii iliyo mbele yetu na ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. DR. BINILITH S. MAHENGE:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii kukushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia hoja hii ya Kamati ya Uwekezaji na Biashara. Kabla sijaanza, kwanza, nichukue nafasi hii kuipongeza sana Kamati hii kwa kuleta hii ripoti yao hapa ambayo kwa kweli imeandaliwa kwa makini pamoja na kwamba imechelewa. Pili, nataka niipongeze sana Serikali katika uamuzi wake wa kuamua baada ya kuona matatizo ya umeme yanavyozidi kuwa makubwa yaliyotupelekea mpaka tukajiingiza kwa hawa wenzetu wa *Richmond* na Serikali ikafikia uamuzi wa kuendeleza ule mpango wa *Stigler's Gorge Hydropower Project* wa Rufiji.

Mheshimiwa Spika, nataka kusema kwamba mchango mkubwa wa matatizo yetu ni nini katika suala zima la umeme. Mimi nadhani ni matatizo ya kutofanya wakati mwingine maamuzi sahihi kwa wakati husika na kuyafanyia kazi. Huu mradi wa *Stigler's Gorge Hydropower Project* ni mradi ambao umekwishafanyiwa *project*, ni mradi ambao umekwishafanyiwa utafiti mwaka 1978 mpaka 1980 na kampuni moja ya *NOPLAN* ambayo ilikuwa imepewa kazi hii au ilikuwa *commissioned* na Rufiji *Basin Development Authority (RUBADA).* Sasa hawa walipofanya ule utafiti katika mwaka huo wa 1978 mpaka 1980 walidhamiria baada ya kufanya utafiti wao wakaona kwamba upo uwezekano wa kujenga *power stations* tatu ambapo moja ilikuwa inaweza kutoa *megawatt* mia nne; ya pili ingetoa *megawatt* mia nane na ya tatu ingetoa *megawatt* mia tisa, ambazo zote kwa ujumla wake zingetoa *megawatt* elfu mbili mia moja. Hiyo ni kazi iliyofanywa na Awamu ya Kwanza mwaka 1978 mpaka 1980 na gharama za mradi huu mwaka 1985 ilikuwa ni dola za Marekani milioni elfu moja na mia mbili. Kimsingi mradi huu kama utachukua njia ya mkato kutoka Chalinze ni kilomita 165 tu unafika kwenye huu mradi.

Mheshimiwa Spika, nadhani tulishindwa kufanya yale maamuzi ama ni kwa sababu ya mashinikizo ya wenzetu wakitumia kigezo cha mazingira lakini ukweli ni kwamba walitushinikiza wakati hata wao wenyewe mpaka tunavyoongea sasa hivi

wameshindwa kusaini Mikataba ya Kyoto. Sasa nadhani haya ndiyo yaliyotufikisha mahali mpaka tukajikuta tuna matatizo ya umeme na tukaanza kutafuta vitu gani viweze kutusaidia. Ripoti ya Kamati imeonyesha kwamba *Richmond* ile shughuli nzima imetumia Shilingi bilioni 172.9/=. Hizo ni hela nyingi sana, ni asilimia kumi na tano ya zile fedha ambazo tungewekeza wakati ule ambapo tungeweza kupata mradi wa kudumu, lakini hizi hazipo na wale wameshindwa kazi. Hilo ni la kwanza, kwamba tunatakiwa tufike mahali tufanye maamuzi yanayotusaidia sisi na wananchi wetu kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, la pili, huko nyuma kulikuwa na mpango wa kuanzisha Mfuko mmoja unaitwa *ESCO Account*. Huu ulikuwa ni kati ya mwaka 1995 na 2000 kama sikosei ambapo ilikuwa kwamba kila mtumiaji wa umeme achangie Mfuko huu ambao tunadhani kama ungeendelea kufanyiwa kazi basi ungeweza kutumika wakati wa dharura kama hii ilipotokea. Vilevile ungetumika kupeleka umeme Vijijini, ungetumika kutekeleza Ilani ya Chama ya Uchaguzi ya kuhakikisha kwamba kila Wilaya inafikiwa na umeme. Lakini kwa bahati mbaya Mfuko huu haueleweki uliishia wapi na kama unaendelea sijui umefikia wapi. Sasa haya yote ndiyo yanayonisukuma kwanza kuunga mkono hoja ya Kamati, ni kweli wamechelewa lakini kuchelewa hakuna maana kwamba tusiifanyie kazi. Suala la muhimu ni kujua tatizo, unapojua tatizo lifanyie kazi wakati wowote bila kuzingatia limefika wakati gani.

Mheshimiwa Spika, Kamati hii ipo kwa Kanuni za Bunge, ni wenzetu ambao wamefanya kazi ambao wameliona. Kwa hiyo, tunadhani ni vizuri basi ili kuwapa imani wananchi wetu kuweka mambo wazi, upo umuhimu wa Kamati hii kuundwa. Ni vitu vichache tu inaweza kujiridhisha, kwa mfano, inaweza kuangalia tu uhalali wa wakati ule tulipokuwa tunakaribisha hizi kampuni hali halisi ya umeme ilikuwaje na uhalali wake ulikuwaje, *rationally* ili ku-*justify*.

Vilevile inaweza kuonyesha mahitaji ya umeme kwa wakati ule yalikuwaje na pia inaweza kuonyesha au kujiridhisha kwamba ni makampuni mangapi kama alivyosema Mheshimiwa aliyepita kwamba yali-*tender* na utaratibu mzima wa *process* ya *tendering*. Nadhani haya ni mambo ambayo Watanzania wakiyajua kupitia watu wao waliowachagua yatakijengea Chama na Serikali heshima kubwa sana. Kwa hiyo, naunga mkono kabisa kwamba ipo haja ya kuundwa kwa hii Kamati Teule kwa nia njema ya kuchunguza na inaweza kutoa mapendekezo nini kifanyike baadaye hasa ukizingatia nilivyotoa historia ya huu mradi wa *Stigler's Gorge Hydropower Project*.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya pili ambayo nataka kuchangia ni sehemu ya madini. Hii pia ni sehemu ambayo inasumbua vichwa vya Watanzania, inapigiwa kelele kuhusu Mikataba. Mimi nadhani katika hili kuna mambo ya kujiuliza, inawezekana sisi wenyewe Watanzania labda ni wachanga katika hii sekta ya madini. Kama si hivyo kwamba sisi sio wachanga katika sekta hii kwa maana ya utaalamu na mambo mengine ya Mikataba basi tujiulize kwamba inaweza kuwa ni sababu gani, kama ni *ignorance* au *corruption* au yote mawili yanatusibu ndio maana tunafikia hapa. Kwa hiyo, nilikuwa napendekeza mambo kadhaa kwenye sekta hii ya madini kwamba kitu cha msingi kwa sababu sisi Watanzania sasa hivi kwanza hatuna wataalamu wetu ambao wamebobea

katika mambo hayo na kuweza kutoa taarifa sahihi za utafiti wa madini yanayohusika kila mahali Tanzania.

Mheshimiwa Spika, pili, hatuna teknolojia na pia hatuna hata washirika ambao tungefanya nao kazi wakatusaidia kama vile leo ninavyosikia wenzetu wa India wana mshirika wao Mrusi ambaye anawasaidia kujenga *Nuclear Power Plant* huko India, washirika kama hao sisi hatuna.

Mheshimiwa Spika, tatu, hatuna teknolojia na wataalamu ambao wangeweza mambo hayo yote. Sasa haya mambo yanapokosekana huwezi kuleta wawekezaji ili wawekeze katika madini fulani ambayo wewe utaalamu huo huna. Kwa hiyo, nilikuwa napendekeza kwamba kwanza kabisa tusifanye pupa kuleta wawekezaji katika sekta hii ya madini. Pili, tutumie muda mwingi kujiandaa zaidi kuliko kugawa rasilimali zetu, tujiandae kwa kuandaa wataalamu, kutafuta washirika ambao ni sahihi, ni wazuri na ambao watatusaidia, kupata vifaa vya uwekezaji, kuandaa taratibu nzuri za uwekezaji na vitu vingine. Tatu, ni vizuri basi kama tatizo lipo kwenye *corruption* sisi wenyewe tujisafishe kwanza.

Mheshimiwa Spika, pia nilitaka kuiomba Kamati kuhusu suala hili la madini kwamba ingechukua nafasi hii kutembelea sehemu zote ambazo kuna watu waliopewa leseni ya utafiti, kama wale wanaofanya utafiti wa madini ya *platinum* katika Wilaya ya Makete kwenye Vijiji vya Nkenja, Ujuni kule Kitulo. Sisi tumefika kule na nawapongeza sana Madiwani ambao walifika pale, lakini ni vigumu sana kwa mwananchi kumwelewesha kwamba wale watu wanafanya utafiti pale wanapoona vyuma vizuri vinameremeta vinachukuliwa na kwenda nje. Sasa nilidhani maeneo kama haya Kamati ingetembelea ikajifunza, kutokana na kujifunza huko ingeweza kuandaa mikakati kupitia Wizara husika ya namna gani ya kuwaelewesha watu hawa kwamba kweli ule ni utafiti.

Mheshimiwa Spika, tulipoongea na yule mwekezaji anayefanya utafiti wa *platinum*, alisema yeye hawajibiki kusaidia kitu chochote kwenye shughuli za jamii katika wale wanaomzunguka. Kwa hiyo, tunadhani ni vizuri katika Mikataba ya Madini ikawekwa sheria ya waziwazi kabisa kwamba moja ya kipengele ambacho inabidi yule mwekezaji wa utafiti atekeleze iwe ni pamoja na kusaidia huduma za jamii pale anapofanya utafiti na kwa sababu hii itamsaidia sana kuwa na uhusiano mzuri na wanaohusika, ulinzi wa mali zake na vitu vingine.

Mheshimiwa Spika, napenda niiombe Kamati hii vilevile kutembelea *water falls* za Bulongwa ambazo zilifanyiwa utafiti huko nyuma na kuona kama zinatoa *megawatt* mia mbili ishirini katika Mto Ruvanyina au Wanaita Rumakalya. Mheshimiwa Waziri Mkuu alipotembelea mwaka jana mwezi Septemba aliwaahidi wananchi kwamba Waziri wa Nishati na Madini angefika kuona nini kinaweza kufanyika katika huo Mto, lakini nadhani wale wanaohusika kufuatilia mpaka sasa hivi hakuna walichokifanya. Kwa hiyo, naomba Kamati ifike kwenye sehemu hizi, watembelee na kuona kwamba ahadi za Waziri Mkuu kwenye vitu kama hivi zinatekelezwa mara moja.

Mheshimiwa Spika, huu ndiyo mchango wangu. Kwa hiyo, naunga mkono hoja kwamba Kamati Teule iundwe kwa nia njema ya kujichunguza sisi wenyewe. Haiwezekani ukafanya usafi kwenye nyumba yako kama wewe mwenyewe mambo yako siyo safi sana. Nadhani tujifanyie usafi sisi wenyewe kwanza. Ahsante sana. (*Makofi*)

**MHE. DR. GUIDO G. SIGONDA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili nami nijaribu kuzungumzia kwa uchache sana kuhusu hii taarifa ambayo ipo mbele yetu. Kwa sababu mengi yamekwishazungumzwa kuhusu hii taarifa mimi kwa kweli nisingependa kuzungumza mambo ambayo tayari yanaeleweka isipokuwa tu labda niipongeze kwa dhati kabisa hii Kamati kwa jinsi ilivyoandaa hii taarifa. Kwa kweli naipongeza sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, mimi bahati mbaya sana mambo mengine yote huwa sielekei kuzungumzia, napenda zaidi kuzungumzia mambo yanayohusu Wilaya yangu. Napenda kufanya hivyo kutokana na hali halisi ya Wilaya yangu jinsi ilivyo. Ni Wilaya ambayo ipo nyuma, kila mmoja anajua. Kwa hiyo, likitokea jambo kama hili la kuzungumzia maendeleo mimi huwa naanza na Wilaya yangu. Katika suala la uwekezaji kwa kweli inanishangaza sana kuona kwamba suala hili katika Wilaya ya Chunya nadhani toka taasisi ya *TIC* hakuna hata mradi mmoja ambao umekwishaanzishwa kule na hasa katika Jimbo langu.

Mheshimiwa Spika, tuna vivutio vingi sana, lakini bahati mbaya ndiyo hivyo tena hakuna anayeviona. Tuna dhahabu, hivi kweli wakati mlipotembelea Mbeya, Kamati hamkuona kwamba Chunya ina dhahabu mkaweza kuizungumzia angalau kwa kunisaidia? Tuna mifugo mingi kabisa ambayo faida yake tunaifahamu, kweli Kamati hamkuweza kuangalia kuona kwamba angalau tuizungumzie habari ya mifugo iliyoko Chunya? Tuna vivutio vingi sana vya rasilimali, lakini hakuna anayefikiria kwamba vivutio hivyo vinaweza kufanyiwa utaratibu na ikawa ni moja ya vigezo vya kuleta maendeleo. Kwa hiyo, pamoja na kuipongeza Kamati hii, bado nilikuwa nasikitika kwamba mngenisaidia mimi mwenzenu angalau kuelezea haya mambo yaweze kueleweka vizuri zaidi. Kamati ina uwezo mkubwa sana lakini kama angalau mngeweza kulizungumzia kidogo suala la Chunya basi ningeweza kuwapongeza zaidi ya hapo nilipowapongeza.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo nilifikiri labda nilizungumzie kwa uchache kabisa ni suala la madini. Madini ambayo mimi nayazungumzia ni zile leseni zinazotolewa, leseni za utafutaji. Katika Wilaya ya Chunya tuna leseni zaidi ya elfu mbili na kitu lakini hatuna leseni ya uchimbaji. Mbaya zaidi zile leseni zinazotolewa zinakwenda kufanya utafiti katika Vijiji ambavyo vina hati yake. Kwa kweli hili linasikitisha sana.

Kuna Kijiji kimoja cha Saza, kwa kweli kijiji hicho kina sifa ya kuwa na dhahabu nyingi, wale wanakijiji wana hati ya kumiliki kile kijiji, lakini leseni imetolewa kwa hawa watafutaji, wanaambiwa waende wakatafute kijijini ambako kuna nyumba na mashamba, kwa kweli hili linanishangaza sana. Lakini bahati nzuri nilikwishazungumza na Naibu Waziri wa Nishati na Madini alikwishaniahidi kwamba angekuja, nina imani

kwamba ahadi yake itatekelezwa ili aje aone hali halisi ya sehemu hii, ni kero kubwa sana.

Mheshimiwa Spika, halafu mbaya zaidi ni kwamba hata hawa watafutaji ambao tunasema ni watafutaji leseni zao huwa zinakuwa *renewed* baada ya miaka mitano, wengine mpaka miaka ishirini, wanapofikia hali ya kusema kwamba sasa nime-*renew* vya kutosha anageuza jina la Sigonda anakuja anaweka jina la Lotto, lakini anakuwa ni mtu yule yule. Kwa kweli inatuletea shida sana, afadhali kama ingekuwa ni uchimbaji au ni migodi lakini utafutaji miaka ishirini unatafuta nini, hujapata kweli miaka yote hiyo? Kwa hiyo, hii ni kero ambayo bahati mbaya Kamati haikuweza kuiona lakini naomba ikumbuke kwamba inatusibu sana sisi tuliopo kule.

Mheshimiwa Spika, kuna suala lingine ambalo dogo kabisa kuhusu hali ya hivi sasa ya mfumuko wa bei. Naona na hili nalo niliongelee kidogo, kwamba kwa kweli sasa hivi katika nchi yetu na hasa katika Jimbo langu mfumuko wa bei unatuathiri sana. Mwaka jana kipato cha kawaida cha mwanachi *income per capita* ilikuwa ni sh. 467/= mwanzoni mwa mwaka jana, sasa hivi angalau imeongezeka kufikia Sh. 500/= au Sh. 600/=. Nyama kilo moja ni Sh. 2,000/= na ndiyo kitoweo chenye protini ya kutosha.

Sasa huyu mtu unataka aendelee, mfuko wa sementi unauzwa Sh. 14,000/=, fedha ambayo mkulima, mwananchi wa Jimbo la Songwe anapata kwa mwaka mzima. Kwa sababu ukianza kufanya mahesabu ya Sh. 467/= kwa siku kwa mwezi mmoja ni Sh. 14,000/=, kwa mwaka mzima ni Sh. 168,000/=, ndiyo mahesabu ya kawaida. Hivi unategemea huyu mwananchi kweli atavuka, ataleta mabadiliko ya maendeleo katika eneo lake wakati shughuli ambazo ndizo zinatarajiwa kuwa zinaweza kuonekana za maendeleo anashindwa kuzifanya, mfuko wa sementi mmoja ni Sh. 14,000/=, mtu mwenye wastani wa kipato cha Sh. 467/= kwa kweli inatuathiri sana.

Mheshimiwa Spika, nafikiri kwamba sijui katika sehemu zingine, lakini mimi kwa upande wangu tumeathirika vibaya sana, na bahati mbaya miundombinu ndiyo inazidi kutuathiri zaidi. Nahisi kwamba hata Kamati ilishindwa kwenda huko kwa sababu ya hali mbaya ya miundombinu iliyopo katika Jimbo langu.

Mheshimiwa Spika, mimi nina wito tu kwa ndugu zangu Wanakamati kwamba waangalie kama mwenzangu mmoja alivyosema kwamba kwa kweli kuna maeneo ambayo hayafikiki kwa urahisi, lakini naomba tutafute uwezekano wa kuyatembelea hayo maeneo. Wanaweza wakatusaidia sana sisi ambao tunatoka kwenye maeneo ambayo ni magumu, nawaombeni sana.

Mheshimiwa Spika, kwa upande mwingine naishukuru Serikali kwa sababu imekwishaanza kusikia kilio changu, nimekuwa nikilalamika kila wakati, na bahati nzuri Serikali imekwishaanza kunisikiliza, naishukuru sana. Nikianza na Mheshimiwa Waziri Mkuu, baada ya kusikia kilio changu amefika kwenye Jimbo langu, alitutembelea ingawa hakulimaliza Jimbo lote na baadhi ya Mawaziri wengine vilevile wamefika.

Lakini nasema kwamba wamefika hawakuona hali halisi ya Wilaya ya Chunya. Nawaomba waendelee kuniunga mkono mwenzao kwa sababu kitu ambacho mimi ninakililia hapa angalau kuwepo mabadiliko ya aina fulani katika ile Wilaya. Wilaya ile imeanza mwaka 1922 mpaka hivi sasa ipo katika hali ile.

Mheshimiwa Spika, juzi Mheshimiwa Waziri Mkuu alisikitika sana kuhusu upande wa elimu mpaka akaagiza Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi iende ikapige kambi kule. Mimi nawaombeni sana Waheshimiwa Mawaziri waiangalie ile Wilaya kama ni moja ya Wilaya za Tanzania.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunao muda kidogo, kwa hiyo, nadhani Mheshimiwa Raus Mhina angekuwa wa mwisho, lakini kwa kuwa tutakuwa na Waheshimiwa Mawaziri wawili watakaofuatia na bado tutakuwa na muda, nitamruhusu Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa awe mchangiaji wa mwisho kwa jioni hii. Kwa hiyo, namwita sasa Mheshimiwa Laus Omar Mhina.

**MHE. ENG. LAUS O. MHINA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipata nafasi hii.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote ningependa kwanza nitoe pole kwa maafa, ajali au misukosuko iliyotupata sisi sote hapa Bungeni kwa kuondokewa na ndugu zetu au kupata ajali, *anyway* hayo tumwachie Mwenyezi Mungu kwani sote yanatugusa.

Mheshimiwa Spika, baada ya pole hizo ningependa nianze pia kwa kuipongeza Taarifa hii ambayo imeletwa na wenzetu wa Kamati ya Uwekezaji na Biashara inayoongozwa na Mheshimiwa William Shellukindo.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, ningependa nianzie na dhana nzima ya uwekezaji. Dhana ya uwekezaji tunaelewa kabisa kwamba malengo yake makuu yanaingia kwenye MKUKUTA kwa maana ya kuharakisha maendeleo. Kuyaharakisha maendeleo hayo kwa malengo gani, kuongeza pato la Taifa na pia kuwapatia ajira watu wetu watanzania. Kwa hiyo, nilitaka nianzie hapo, lengo la dhana hii ya uwekezaji.

Mheshimiwa Spika, naishukuru sana Serikali kwamba imeliona hilo kwamba dhana ya uwekezaji ni dhana ambayo inaweza ikaiendeleza Tanzania, na hii ni baada ya kusoma kutoka kwa wenzetu hususan wa nchi za Kusini Mashariki ya Asia ambazo zimefanikiwa sana katika lengo hilo.

Mheshimiwa Spika, napenda pia niipongeze Serikali kwani kwa kuliona hilo leo hii imeanzisha hata maeneo maalumuu ya uwekezaji. Kwa mfano, tunalo eneo la Mheshimiwa Benjamini William Mkapa (*Special Economic Zone)* na haikuishi hapo tu, bali pia kumepitishwa Sheria maalumuu, *Special Economic Zone Act* ya kuweka maeneo maalumuu ya uwezekaji.

Mheshimiwa Spika, katika Taarifa ya Uwekezaji na Biashara imeonyesha karibuni takriban sehemu nne maalumu. Kwa maana ya Umeme, Maendeleo ya Petroli, imeonyesha Sekta ya Madini, Viwanda na Biashara pamoja na Masoko.

Mheshimiwa Spika, mimi nasema kwa bahati mbaya kwenye taarifa hii nimejaribu kuangalia Sekta ambazo ni muhimu sana na zinanigusa mimi mwenyewe kama Sekta ya Kilimo na Sekta ya Ufugaji sikuziona. Hizo ningeomba wenzetu walioandaa Taarifa hii waishauri Serikali iziingize hizo za Kilimo na ufugaji, kwani zinatugusa sana hususan sisi watu ambao tupo katika maeneo ya vijijini.

Mheshimiwa Spika, nianze na Sekta ya umeme. Nakubaliana kabisa na maandishi yaliyomo katika Taarifa hii. Lakini ningependa niweke msisitizo mkubwa katika Nishati ya Upepo. Nishati ya Upepo ni nishati ambayo kwa kweli ingeweza ikatusaidia sana Tanzania kwa sababu upepo tunao na upepo ni wa bure hasa ukizingatiwa kwamba nishati hii haiharibu mazingira. Kwa hiyo, tukizingatia suala la mazingira nadhani hiyo ndiyo nishati mbadala kwa Tanzania, na pia nishati hii haihitaji marekebisho au matengenezo ya mara kwa mara ya mashine zile zikishawekwa, kwa sababu zinategemea upepo tu labda na mafuta kidogo ya kuweka grisi kwenye mitambo ile, lakini zaidi ya hapo haina gharama nyingi zaidi. Kwa hiyo, ningependa kwa kweli tuliangalie hilo.

Mheshimiwa Spika, nishati nyingine ambayo ningependa niiongelee bahati mbaya haikuongelewa katika Taarifa hii ni nishati ya umeme ambayo unaweza ukazalishwa kutokana na mabaki ya mkonge na siyo mabaki ya mkonge tu, lakini ningependa sana niongelee mkonge kwa sababu hii imekwishafanyiwa utafiti wa hali ya juu. Nadhani Waheshimiwa Wabunge, Waheshimiwa Mawaziri, wana taarifa ya Kiwanda kinachozalisha umeme cha Hale ambacho umeme wake unatokana na mazao au mabaki ya mazao ya mkonge.

Mheshimiwa Spika, kiwanda kile cha pale Hale kina uwezo wa kuzalisha megawati za umeme 2 ambazo ni kiasi kikubwa sana, na inasemekana kama mkonge utatumika vizuri kwa Mkoa mmoja tu wa Tanga kina uwezo wa kuzalisha megawati za umeme 500 ifikapo 2025. Megawati 500 kwa kweli ni umeme ambao tunaweza hata tuka-*export* tukauza nchi ya Kenya. Kwa hiyo, ningeomba hili liangaliwe kwa undani.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Shirika la Maendeleo ya Petroli hili sina matatizo nalo, wenzetu wamelielezea vizuri sana, isipokuwa tu nisisitize tu kuwaunga mkono kwa dhana hii walioileta kwamba mauzo ya gesi baadhi ya fedha zake au *percent* fulani ya mauzo ya gesi kwa kweli fedha hizo zisaidie ziende kwenye Shirika *(TPDC).*

Mheshimiwa Spika, kuhusu Sekta ya Madini pia maelezo nimeyakubali yameelezwa vizuri sana katika ukurasa 12 *section* 4.7. Labda hapa ningependa niongelee upande wa vito. Kwa sababu Jimbo langu la Korogwe Vijijini vilima vyote vile vinavyoonekana vimezungukwa na vito upande wa Kigwasi, upande wa Kalalani, upande wa Magoma mpaka Mkalamo kote huko kwa kweli tunapata vito vya aina mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, tuna vito kama nilivyosema, lakini matunda ya vito hivyo mpaka sasa kwa kweli sisi wakazi wa Korogwe hatuyaoni. Nasema hiyo makusudi, tunao wachimbaji wakubwa upande wa Palalani, lakini wachimbaji wale hawalipi kodi yoyote kwa Halmashauri kutokana na namna leseni zinavyotolewa. Hili limeongelewa sana bahati nzuri na Mheshimiwa Beatrice Shellukindo, naliunga mkono sana. Ningeomba liangaliwe kwa undani kusudi mapato yale kwa kweli yaweze kwenda kwenye Halmashauri yetu kwa ajili ya miradi yetu ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, niongelee Sekta ya Kilimo ambayo haikuongelewa kwenye taarifa hii. Hapa ningependa nionge tu kwa kifupi. Uwekezaji kwenye kilimo nadhani upewe kipaumbele pia. Upande wa Korogwe Vijijini nikitoa mfano wa Tarafa yangu moja ya Bungu.

Tarafa ya Bungu inafahamika sana kwa kilimo cha Chai, na kilimo hicho kwa kweli wakulima wake wengi ni wadogo wadogo ambao hawana uwezo wa kujenga viwanda vya kusindika majani hayo ya chai. Kwa hiyo, naiomba Serikali ijaribu kutoa ushawishi kwa wawekezaji hao kuwapatiwa viwanda wakulima hao wadogo wadogo wa chai ambao ni wengi, kwa kweli na hilo ndilo zao lao kubwa la biashara.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa wanachofanya wakulima wale ni kuuza majani hayo ya chai kwa wenye viwanda wakubwa wanaozunguka mashamba yale na kujipatia senti ambazo kwa kweli ukiangalia sana ni kama za kununulia mafuta ya taa tu.

Mheshimiwa Spika, mfano mwingine ni zao la Mkonge. Zao la mkonge limeitikiwa vizuri sana katika Wilaya ya Korogwe, lakini kinachowakwamisha au kitakachowakwamisha zao hili kweli likianza kustawi vizuri, hakuna korona za kutosha. Kwa hiyo, ningeiomba Serikali kwenye uwezekano iwashawishi waweke korona kwenye sehemu nyingi za Korogwe. Ninaelewa jitihada zinazofanywa na Katani *Limited* za kufufua korona zilizopo, lakini hata kama zitafufuliwa kwa kweli hazitatosha.

Mheshimiwa Spika, kuna Mheshimiwa Mbunge mmoja ameongelea kuhusu mboga mboga na matunda katika Wilaya ya Korogwe na jirani zake. Ni kweli kabisa wapo wazalishaji wakubwa sana wa mboga mboga na matunda, lakini matunda yale wanafaidi wenzetu wa Kenya. Tumeambiwa tutajengewa soko sehemu ya Segera. Mimi ningeomba kweli twende ndani zaidi siyo soko tu, bali tujengewe kiwanda pia cha kusindika matunda hayo. Hapo itakuwa tumeokoa soko la matunda kwa sehemu ile ya Korogwe na majirani zake. Lakini tukisema kwamba itakuwa ni soko la kuuza matunda tu itakuwa bado hatujawafaidisha wananchi wakulima wadogo wadogo wa Wilaya ile ya pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ningependa tu nimalizie kwa kitu ambacho sikukiona kwenye Taarifa ya Kamati. Kwa upande wangu mimi nasema ni cha masikitiko. Kuna wawekezaji wamekwishapata mashamba au viwanda vingi hapa nchini, na mashamba yale au viwanda hivyo vilikuwa vina madeni na kuna wafanyakazi wa awali katika viwanda vile waliokuwa wanafanya kazi, wanadai mafao yao mpaka leo.

Katika mikataba ile ilikuwa wawekezaji wale wakishachukua kama ni kiwanda au ni mashamba wawalipe mafao watu waliokuwa wanafanya kazi katika viwanda hivyo au mashamba hayo. Mfano hai ni katika Jimbo langu Kiwanda cha Mkumbala *Chipboard*, kuna wafanyakazi pale wanateseka kuomba mafao yao na sasa ni karibu miaka 6 au 7 hawajalipwa mafao yao na wengine wamekwishafariki. Kwa hiyo, ningeiomba Serikali kwa kweli ingeangalia ni jinsi gani itashughulikia mafao ya wafanyakazi ambao walikuwa wanafanya kazi katika mashamba au viwanda kabla ya kuchukuliwa na wawekezaji katika sehemu hizo.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba tu niseme nakubaliana na Taarifa niliyowasilishwa. Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Laus Mhina ahsante sana. Namwita sasa Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa. Mheshimiwa Ruth Msafiri ameniomba nafasi achangie kwa dakika 10, nitamruhusu awe msemaji wa mwisho. Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa!

**MHE. DR. WILLBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii niweze kuchangia hoja hii. Awali kabisa niseme nakubaliana na hoja ya Kamati ya Uwekezaji na Biashara na naiunga mkono. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa niseme nimefarijika sana na Taarifa ya Kamati hasa nilipotazama maeneo yaliyoweza kutembelewa na Kamati. Nimegundua kwamba Kamati hizi zikiwezeshwa zikapata fedha za kutosha zinasaidia sana Bunge letu kutimiza jukumu lake la Kikatiba kwa mujibu wa Ibara 63(2) ya kusimamia Serikali. Taarifa hii yote inaonyesha kwa kina kabisa maeneo yaliyotembelewa na hasa ni muhimu unaposimamia shughuli kuona kwa macho yako yale unayoambiwa kwamba yamefanywa. Hasa unapokuwa chombo cha kupitisha Bajeti basi ni vyema pia ukajua namna gani ile bajeti inatumika, na hii ndiyo kazi ambayo Kamati hii imetufanyia. Naishukuru sana na kuipongeza Kamati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ningependa kujikita kwenye suala la Kamati Teule ya *Richmond.* Napenda kuzungumzia hili kwa ajili ya mambo mawili tu. La kwanza, Kamati hii imetuonyesha maeneo ambayo yana dosari katika taratibu zilizotumika kuingia kwenye Mkataba ule wa *Richmond*. Lakini la pili, kuna kelele nyingi zilipigwa katika nchi nzima, dalili kwamba kuna kasoro, kuna tatizo na tatizo lolote hakuna namna ya kufanya isipokuwa kwa kufanya uchunguzi wa kitaalamu. Lakini isitoshe vilevile panapokuwa na hisia namna nzuri ya kusafisha hisia ni kuingia kwenye chungu kile kuona kwenye chungu kuna kitu gani. Nadhani Kamati imefanya kazi yake, yenyewe imekwishafanya utafiti wake imeona maeneo. Sasa inaliomba Bunge na lenyewe lisaidie kuunda Kamati Teule. Kwa hiyo, nadhani walishafanya kazi yao, mimi sitaki hata kuwauliza walishindwa nini. Kwa sababu mtu anapokuomba msaada ni wazi si lazima aseme kwamba alishindwa mahali fulani, unajua kwamba kuna kasoro fulani na mimi nguvu yangu imeishia hapo, naomba sasa nisaidiwe na chombo kikubwa zaidi.

Mheshimiwa Spika, lakini ninafahamu vilevile TAKUKURU chombo chetu kimekwishafanya uchunguzi na kilimaliza na kufungua uchunguzi wake, taarifa yake ilitolewa hadharani kwenye Vyombo vya Habari tuliisoma ile taarifa. Lakini bado yakabaki maswali mazito, nadhani tulihoji ndani ya Bunge hili kwamba mbona taarifa ile haikukidhi haja.

Sasa la tatu, ni taarifa ambayo tumekuja kuipata kutoka kwenye chombo ambacho tulikiunda kisheria, chombo cha Serikali, tulikiunda kwa sheria hapa hapa ndani ya Bunge hili, ni taarifa iliyotolewa na *Public Procurement Regulatory Authority (PPRA)*. Kwa bahati nzuri *PPRA* ni mkaguzi wa mambo haya yote. Sasa unapopata taarifa kama hiyo ya *PPRA* huwezi kuipuuza hata kidogo ina-*raise* hasa mambo mazito.

Mheshimiwa Spika, napenda ninukuu tu mambo machache sana mazito ambayo *PPRA* imeyasema. Taarifa hii ni taarifa *Public* na ilishatoka kwenye Vyombo vya Habari. Taarifa hiyo inasema katika sehemu moja kwa mfano, "*Even after Tender Board recommended that TANESCO should not be a part of contract of a Procurement process it had not seen through it was overruled and it ended up signing a contract with a Contractor Richmond Development Company LLC it had intially established conclusively that it was none responsible to bid requiments and he was unable to deliver the service required.*" Hii ni taarifa nzito sana kwamba walitakiwa kusaini Mkataba na *Contractor*, Mkataba ambao wao hawakujishughulisha katika taratibu za kawaida. Sasa unapopata taarifa hii kutoka kwa chombo ambacho ni chetu tumekiunda kwa Sheria ya Bunge, ni taarifa nzito, ni lazima ifanyiwe kazi kwa uzito unaostahili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika sehemu nyingine ya taarifa ya *PPRA* inasema na hiyo imenishitua zaidi kuliko hata ile ya kwanza: "*Contract between TANESCO* na *Richmond Development Company was signed in strange circumstances*." Kwa Kiswahili kizuri nadhani mazingira ya kutisha au ya kushangaza *at night,* usiku *under the Ministry of the Mineral*s and *Energy with some contractual issues protecting the client having been ignored as there was no room for TANESCO to review the draft contract. The Company Secrectary doesn't know who drafted the contract.*" Hata yule Mwanasheria wa *TANESCO* hakufahamu ni nani ametengeneza Mkataba huo. *No performance Bond, the power rental* ikatoa sasa mambo ya kitaalamu, nafikiri yatakuwepo huko mbele sina sababu ya kuyasoma. Akaendelea "*The TANESCO Board was ordered by the Ministtry of the Minerals and Energy to signed the contract despite TANESCO's initial resistance especially after the process that brought the winner was handled outside TANESCO procurement process.*"

Mheshimiwa Spika, nilisimama ili niyaongelea haya, kwa sababu sisi wenyewe tulipitisha sheria ndani ya Bunge hili. Tukasema kuanzia sasa haya matatizo ya taratibu za ununuzi yatakwisha kutokana na sheria hii. Nakumbuka tulisimama wakati ule na Mheshimiwa Waziri akatuthibitishia kwamba kuanzia mwaka 2002 hapatakuwepo tena na taratibu hizi za kinyemela nyemela kama naweza kutumia neno hilo. Kwa sababu tulikuta kwamba mambo mengi ya *tender* yalikuwa yanafanyika kinyume cha taratibu. Baada ya kupitisha sheria hiyo tukaambiwa kwamba hayo sasa ndiyo mwisho.

Mheshimiwa Spika, sasa ulipofika mwaka 2006 tukayapata haya, ni lazima Bunge hili tujiuliza Sheria tuliyopitisha, tuliipitisha kwa ajili ya nini kama kuna mahali inaweza ikabadilishwa tu. Aidha, ni Wizara au ni nani aliyetoa mamlaka kwa huyo mtu aliyefanya mabadiliko hayo ya kwenda kinyume cha sheria tuliyopitisha, kinyume cha taratibu au *regulations* zilizopitishwa zinazotekelezwa na ile *Public Procurement Act*. *Regulations* za *Public Procurement* zimetengenezwa mwaka 2005, hazijakaa hata zaidi ya mwaka na kabla ya mwaka kwisha zimekwishakiukwa na kuvunjwa. Ni kwa sababu zipi haya mambo yanafanyika?

Mheshimiwa Spika, sasa nikiona haya ndiyo maana nakubaliana kwamba Kamati inapotoa pendekezo kuna kitu kizito kimeonekana na hicho kitu kinahitaji chombo kizito kinachopaswa kukishughulikia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hakuna chombo kizito katika Bunge letu kwa kufuatana na sheria yetu ya *Parliamentary Immunity Powers and Privileges Act*, na Kanuni zetu, Kanuni ya 104, kama Kamati Teule. Kwa sababu Kamati Teule inapata haki, inapata wajibu wa kutekeleza shughuli zake kwa lugha ya Kiingereza wanasema "*Quasi judicial"*. Wenzangu wasiozungumza Kilatini watasema, "*Quas*". Sasa kwa mimi mlatini nitasema *Quasi judicial,* mnisamehe hiyo ndiyo lugha yangu. Naona *Attorney General* ananicheka lakini asiniharibie lugha yangu.

Mheshimiwa Spika, chombo hiki "*Quasi judicial"*" ni nusu ya Mahakama, kina mamlaka ya kuita, kina mamlaka ya kuapisha, kina mamlaka ya kuchukua hoja hizo na hoja hizo zikichukuliwa baadaye zikawasilishwa kwa Spika, ndiyo hoja ambazo zinaweza kwenda hata Mahakamani na zikakubalika na Mahakama. Sasa inapofikia hatua hii mimi nafikiri hakuna njia nyingine isipokuwa kukubaliana na Kamati yetu kwamba chombo hiki kilichopendekezwa ndiyo chombo pekee kitakachoondoa hisia, kitakachoondoa maneno na manung'uniko yaliyopo huko nje, kitachoisafisha Serikali yetu. Kwa sababu tunachotaka sisi ni Serikali safi inayofuata taratibu, inayolinda sheria, inayolinda kanuni ambazo tumejiwekea. Ndiyo heshima ya nchi ambayo inafuata *Rule of Law*, inafuata taratibu zake kikamilifu kadri zilivyopitishwa na Bunge na haziwezi tena kupindishwa na chombo kingine chochote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, wala sihitaji kuongea zaidi kwa sababu, sababu hizo hasa za chombo cha Serikali ni nzito na hakuna namna nyingine ya kupata majibu ya hoja hizo isipokuwa kwa kuunda Kamati Teule ya Bunge.

Mheshimiwa Spika, kwa ruhusa yako naomba niwashawishi na wenzangu tukubaliane katika kuunda Kamati hiyo Teule. Nakushukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA.** Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa ahsante sana. Msemaji wangu wa mwisho leo ni Mheshimiwa Ruth Msafiri.

**MHE. RUTH B. MSAFIRI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii. Naomba nianze kwa kumshukuru na kumpongeza sana Mheshimiwa Mwenyekiti wa

Kamati ya Uwekezaji na Biashara kwa kuiwasilisha hoja yake na jinsi ambavyo wameifanyia uchunguzi wa kina.

Mheshimiwa Spika, naomba niende moja kwa moja kwenye hoja ambazo napenda kuzichangia. Napenda nizungumzie kuhusu Sekta ya Madini. Mimi naipongeza sana Serikali kwa jinsi ambavyo imetoa kipaumbele katika kuendeleza Sekta ya Madini, na kwa kweli Sekta ya Madini kama itapewa ufuatiliaji wa karibu na taratibu zetu ambazo Serikali yetu imejiwekea inaweza ikawa ni upande mmoja wa kuinua maendeleo ya wananchi, lakini vilevile kuinua pato la Taifa letu kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, naiunga mkono hoja ya Kamati moja kwa moja ambapo imezungumzia umuhimu wa wananchi katika maeneo ya uchimbaji wa madini na wenyewe kuweza kupewa haki ya kuwa na ubia na wawekezaji, na vilevile kuweza kuchukuliwa kama wao ni sehemu ya wamiliki wa ardhi ile wakaweza kuwa na hisa ambayo itakuwa inadhaminiwa na sehemu ya ardhi wanayoimiliki. Kipindi hiki kumekuwa na upatikanaji wa madini katika sehemu nyingi sana za nchi yetu ambalo ni suala la kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa sababu madini tumepewa na Mwenyezi Mungu. Lakini katika maeneo mengi utakuta mara tu yanapojulikana kwamba mahali pale madini yapo kinachofuata ni kuwaondoa wananchi wakazi wa eneo lile na eneo lile kubinafishwa kwa wageni.

Mheshimiwa Spika, madini hayo yanapatikana kwa lengo la kuwasaidia watanzania wote, lakini katika Taifa letu mojawapo ya hoja nzito ambazo zinafanyiwa kazi ni kuhakikisha kwamba ni maisha bora kwa kila Mtanzania. Mtanzania anayebahatika kwamba ama shamba lake au makazi yake yameonekana kuwa na madini, naishauri Serikali imlinde sana kuhakikisha kwamba asibughudhiwe. Badala yake yeye awe ni wa kwanza kuwa mmiliki wa eneo lile na yeye asaidiwe kuona amkubali mwekezaji yupi ambaye atashirikiana naye kuhakikisha kwamba anatumia eneo lake kama sehemu ya mtaji wake, ama kama sehemu ya hisa kuhakikisha kwamba anaweza akajipatia kipato katika maisha. Akawa ni mmoja wa wamilikaji wakubwa wa eneo lake akawa ni yeye. Miundombinu inayopatikana pale wakati mwingine wanakuwa walikwishaanzisha shule, shule zinahamishwa, sehemu nyingine kuna barabara, barabara inahamishwa na kadhalika ilimradi tu kutoa nafasi kwa wawekezaji wageni.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali kwamba madini yanapopatikana moja kwa moja watanzania wasitupwe nje na badala yake wasaidiwe ili waweze kupata maendeleo katika maisha yao. Kama ikitokea eneo lile lilikuwa ni pori ambalo lilikuwa halimilikiwi na mtu yeyote moja kwa moja, basi iende katika taratibu za Serikali. Lakini kama ardhi ile ilikuwa chini ya kijiji ni vizuri vilevile Halmashauri za Wilaya, Miji, Manispaa na Jiji zikasaidia kuona kwamba wale wananchi pale wanaboreshewa maisha yao.

Mheshimiwa Spika, naomba lingine nizungumzie umeme. Kamati imezungumzia vizuri pia kuhusu tatizo la umeme. Kumekuwa na tatizo la umeme ambalo ni kweli limekuwa sugu na linaathiri maendeleo ya kijamii na kiuchumi kwa Taifa letu. Mara nyingi imeonekana kwamba umeme ni kwa ajili ya watumiaji wa mijini.

Mheshimiwa Spika, umefika wakati umeme sasa siyo kwa mahitaji ya watu wa mijini tu. Sasa hivi umeme unahitajika kila mahali Tanzania. Umeme ingelikuwa ni bahati ukaweza kupatikana vijijini nina uhakika ungelisaidia kukuza kilimo, ungelisaidia kukuza ufugaji bora na wa kisasa wenye tija ya kutosha. Kwa sababu wananchi wangeliweza kulima na kusindika mazao yao pale pale yalipo na kuweza kuyasafirisha yakiwa na thamani kubwa sana, na wangeshawishika hata kuziboressha *SACCOS* zetu ambazo tumekwishakuwa nazo. Nina hakika tumejitahidi sana kuwahamasisha watanzania waunde *SACCOS*, lakini *SACCOS* ni vikundi vya kuchangiana kwa sehemu kubwa, na kuchangiana lingekuwa ndilo tatizo kwa sababu kipato chao bado kiko chini sana.

Mheshimiwa Spika, juzi Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini alipokuwa akijibu swali la Mheshimiwa Wilson Masilingi alitaja Wilaya ya Muleba ikiwa katika Awamu ya Tatu katika kusambaziwa Umeme Vijijini katika Mkoa wa Kagera.

Mheshimiwa Spika, lakini katika Wilaya ambazo zimejitahidi katika kilimo cha mananasi kwa mfano ni pamoja na Wilaya ya Muleba ambako maeneo yaliyo na umeme ni machache mno. Maeneo yaliyotajwa juzi kwamba yatapata umeme katika Awamu ya Tatu vilevile ni machache mno.

Mheshimiwa Spika, nashawishika kwa kuangalia hali halisi ya umeme. Sasa ingelipewa uzito mkubwa sana na umeme ukapelekwa vijijini ili kuwawezesha wananchi kuweza kulima na kuanzisha viwanda vidogo vidogo kwa sababu historia ya maendeleo katika miji na hata katika mataifa makubwa ni yale yaliyoanziswha katika vijiji, yalianzisha viwanda vidogo vidogo vya kifamilia vikawa vikubwa na vikaweza kufikia hata mapinduzi makubwa ya viwanda. Kwa hali hiyo kusema kwamba vijijini ni mahali pa mwisho pa kupeleka umeme kwa kweli kwa kipindi hiki sio sawa kabisa ni mahali ambapo panatakiwa paangaliwe kwa ukaribu sana.

Vilevile maeneo ambayo tayari yana umeme mara nyingi tumekuwa tukijaribu kuishawishi Serikali ione uwezekano wa kushusha *transformer*. Kwa mfano, Wilaya ya Muleba ina maeneo mengi sana ambayo tayari umeme unapita. Jimbo langu la Muleba Kaskazini ni mojawapo ambalo lina maeneo mengi ambapo umeme unapita. Mimi nafikiria tarafa zangu tatu, nimebakiza tarafa moja tu ambayo haina umeme kabisa. Lakini unakuta umeme wanaona tu nyaya zikipita, nguzo zinapita kwenye mashamba yao wanakatiwa migomba, mibuni yao lakini hawapati umeme.

Mheshimiwa Spika, suala hili kwa namna fulani linaleta udhaifu. Kuna watu wengi ambao wameamua kufanya *wiring* katika majumba yao ili waweze kupatiwa umeme na mpaka sasa hawajapatiwa umeme. Naishauri Serikali iangalie basi njia nyingine iondoe ushuru hata katika vyombo vingine kwa mfano *solar* inaweza ikawa ni njia mbadala. Kama ingeweza kuwa na ushuru kidogo wananchi wangeliweza wakatumia *solar* katika kujiendeshea maisha yao. Mimi naamini kwamba ingesaidia sana. Lakini sasa hivi *TANESCO* imekuwa ikipandisha kiholela umeme, hizi gharama za umeme kwa kweli zinatisha sana. Sasa hivi wamekuwa wakitangaza kupandisha mara kwa mara.

Haya mabadiliko ya mara kwa mara ya viwango vya umeme wa *TANESCO* ambao hauzingatii kipato cha Watanzania. Sasa hivi wanapandisha wakati wowote wanapopenda wenyewe ni suala ambalo naomba Serikali iliangalie sana.

Vilevile napenda niende katika hoja nzito ambayo imetolewa na Kamati ambayo inahusu kuundwa kwa Kamati Teule ambayo itakuwa na uwezo wa kisheria kupata mikataba kuhusu suala zima la *Richmond*. Wote tuliathirika sana na matatizo ya *Richmond* na tumeathirika hata sasa hivi. Sitopenda kuongezea maneno mengi napenda niseme neno moja tu kwamba ninaunga mkono kuundwa kwa Kamati hii Teule ikafanye kazi yake ili tuweze kupata majibu yaliyo sahihi.

Naamini itakuwa ni njia iliyo nzuri itakayosaidia wanaosaini mikataba kuwa makini pale ambapo wanatakiwa kusaini mkataba kwa niaba ya Watanzania wenzao. Lakini wanaotakiwa kuingia mikataba nchini pia wajue kwamba wawakilishi wa wananchi ambao wanakuja kufanya kazi katika nchi yao vilevile wako makini. Madhara yoyote yanayotokea kwa *Richmond* kutokufanya kazi kwa wakati uliotakiwa yanatugusa sisi wote. Ninaunga mkono suala hili.

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa ninaomba nizungumzie kuhusu gharama za mafuta. Mafuta ya magari na mitambo yamekuwa yanapanda ovyo ovyo. Kama Serikali inaweza itumie wataalamu wake ione uwezekano wa kupata njia mbadala ya kupata mafuta kuendeshea vyombo vya usafiri na mitambo mingine ili kuweza kupunguza kupanda kwa maisha na gharama za kila mara kwa ajili ya Watanzania. Mimi naamini inaweza ikasaidia pengine tukaweza kuwa na maisha yaliyo afueni badala ya hivi ilivyo sasa kila wakijisikia kidogo wanapandisha bei na sasa hivi leo asubuhi nimesikia wanatangaza pipa moja limefikia dola 100 za Kimarekani hali ambayo inatishia. Hata sisi hapa mafuta yanaweza yakaongezeka. Sasa kama hakuna njia mbadala inawezekana tukaendelea kupata tatizo hili siku hadi siku. Nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Ahsante sana.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Msafiri. Nimepata maombi ya wachangiaji wawili kutoka upande wa Serikali na nitawaita kwa mpangilio ufuatao: kwanza, ni Mheshimiwa Chibulunje, Naibu Waziri wa Viwanda, Biashara na Masoko na atahitimisha Waziri wetu wa Nishati na Madini, Mheshimiwa Karamagi.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii na mimi nichangie hoja hii ya Taarifa ya Kamati ya Uwekezaji na Biashara ambayo imewasilishwa mbele yetu hapa asubuhi.

Mheshimiwa Spika, kwanza kwa sababu nasimama hapa kwa mara ya kwanza kwa kutoa hotuba, napenda kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Chilonwa na mimi mwenyewe niungane na wenzangu waliotangulia kutoa rambirambi za kifo cha Mbunge mwenzetu aliyekuwa Naibu Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, Mheshimiwa Salome Mbatia aliyetutoka hivi karibuni. Pia nitoe pole kwa wale wote

waliopata ajali mbalimbali hapa nchini wakiwemo wenzetu hapa Bungeni, Mheshimiwa Juma Kapuya na Mheshimiwa Mudhihir Mohamed Mudhihir.

Mheshimiwa Spika, nataka nianze kuchangia hoja hii kwa kujielekeza katika maeneo machache yaliyoelekezwa katika Wizara yetu ya Viwanda, Biashara na Masoko ambayo ni moja ya Wizara inayosimamiwa na Kamati hii. Lakini kabla ya hapo nataka niishukuru sana Kamati kwa ushirikiano mzuri ambao imekuwa ikitupa katika kutushauri na kutuelekeza mara kwa mara katika maeneo mengi. Kwa hiyo, nataka tu nitangulie kuahidi kwamba tutaendelea kushirikiana na Kamati katika kufanya kazi pamoja kwa nia ya kuboresha shughuli zetu za maendeleo ya wananchi.

Mheshimiwa Spika, maeneo machache ambayo nataka nijielekeze ambayo yamejitokeza ama kwenye taarifa yenyewe au kutokana na michango ya wazungumzaji ni kama ifuatavyo: Kwanza limeelezwa hapa suala la viwanda vinavyozalisha hapa nchini vishawishiwe kutumia malighafi zilizoko hapa nchini. Hili sisi tunaliunga mkono na kama ambavyo Kamati inafahamu baadhi ya viwanda ambavyo tumevitembelea tumekuwa tukihimiza hivyo kwamba katika kufanya hivyo kwanza tunaongeza thamani ya mazao yetu ambayo yanazalishwa hapa nchini na hivyo hivyo tunaongeza ajira badala ya kupeleka malighafi nje kwenda kusindikwa au kufanyiwa matengenezo yoyote tunakuwa tunawapunguzia ajira wananchi wetu. Kwa hiyo, hili sisi tunaliunga mkono na kama ambavyo Kamati inafahamu tulipokuwa tumetembelea kile Kiwanda cha *NIDA* tuliona mfano mzuri sana ambao wale wenye kiwanda wanahangaika kutafuta kwanza pamba kutoka kule Kahama na kuileta Dar es Salaam kuitengeneza kuwa nyuzi na hatimaye kutengeneza nguo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, huo ulikuwa mfano mzuri na sisi tunaendelea kuzingatia hilo, tunaendelea kuongea na viwanda vingine na kuvihimiza viweze kuiga mfano huo. Lakini pia katika eneo hilo hilo kwenye sekta ya ngozi kwa mfano tumeshatoa taarifa kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Kuendeleza Zao la Ngozi Tanzania kwamba inaweza ikawa mfano mzuri sana wa kuhakikisha kwamba tunatumia malighafi zetu zilizopo hapa nchini kuweza kubadilisha kupata bidhaa zinazotokana na malighafi zetu hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, eneo la pili ambalo nilitaka nijielekeze ni lile ambalo lilizungumzia habari ya wale waliouziwa viwanda vya korosho kuwezeshwa ili waweze wakapata mikopo na hatimaye wafanye kazi ya biashara. Kazi tunayoifanya sasa hivi na ambayo kusema kweli tumefika nayo mbali kidogo ni kwamba wale wote waliouziwa viwanda ambao waliuziwa viwanda vile kwa bei nafuu, kuhakikisha kwamba wanamilikishwa vile viwanda ili waweze wakafanya kazi ili viwe mikononi mwa wananchi.

Kwa hiyo, kazi tunayoifanya sasa hivi ni kuthaminisha vile viwanda ili waweze wakapata hatimiliki, wakishapata hatimiliki yenye thamani, yenye ukubwa, itakuwa ndiyo dhamana yao ya kuwapatia mikopo ya kuendesha viwanda hivyo. Kazi hii tayari tumekwishaanza kuifanya kwa kushirikiana na Taasisi mbalimbali vikiwepo vyombo vya fedha pamoja na wadau wenyewe. Sisi kama Wizara tumeshawaita hao wahusika hapa

Bungeni mara mbili na mimi mwenyewe nimekwishafika Mtwara tukazungumza nao. Kwa hiyo, kazi hiyo tunaendelea nayo na tunazingatia ushauri wa Kamati wa kuhakikisha kwamba tunashirikiana na wale wenye viwanda ili waweze wakafanya kazi yao kwa kadri ilivyokuwa imekusudiwa.

Mheshimiwa Spika, eneo la tatu ambalo ningependa niielezee Kamati pamoja na baadhi ya Waheshimiwa Wabunge waliochangia, ni kwamba hapa wamezungumzia suala la ujenzi wa masoko uende haraka. Lakini kwa kweli hapa kikubwa kilichokuwa kinazungumziwa ni kuhakikisha kwamba masoko haya yaweze yakasaidia mazao yetu yasiweze kwenda nje na hasa mboga mboga na matunda. Juzi nilipokuwa najibu swali Bungeni nilitoa taarifa juu ya upembuzi yakinifu uliokuwa unafanyika kwa ajili ya ujenzi wa masoko makubwa mawili, la Segera katika Mkoa wa Tanga na lile la Makambako katika Mkoa wa Iringa, nataka nilitaarifu Bunge lako Tukufu kwamba Ijumaa ya wiki iliyopita taarifa ya upembuzi yakinifu ilikwishapokelewa na Wizara, kwa hiyo, sasa hivi kitakachofuata ni kuendelea kuipitia hiyo taarifa tuichambue na hatima yake tuweze tukashirikiana na wadau wengine pamoja na Halmashauri za Wilaya zinazohusika kwa maana ya Wilaya ya Handeni pamoja na Wilaya ya Njombe ili utaratibu wa ujenzi wa masoko hayo uweze ukaanza.

Mheshimiwa Spika, lakini kama nilivyokuwa nimekwishasema katika kujibu swali hapa, nilisema ujenzi huo utategemea sana na msukumo wa Halmashauri za Wilaya hizi zinazohusika, na sisi kama Serikali tutaendelea kushirikiana nao kuweza kuona kwamba masoko haya yanajengwa kwa wakati. Lakini niseme tu kwamba hata katika usindikaji wa mboga mboga pamoja na matunda katika maeneo nilitoa taarifa kwamba kadri masoko haya yatakapokuwa yanazidi kupanuka mambo mengine vilevile yatakuwa yanafikiriwa namna ya kuyashughulikia.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ambalo limegusiwa na taarifa pamoja na wasemaji wengine lilikuwa ni suala la uzalishaji wa Kiwanda cha chumvi kule Lindi. Nataka kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba muda mfupi uliopita, nadhani wiki tatu au nne hivi zilizopita nilipata heshima ya kuitembelea Mkoa wa Mtwara kwa kazi maalumu ambayo tulikuwa tumeagizwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Nilipata fursa ya kuona vilevile Viwanda vya Chumvi Mtwara ambavyo tayari Shirika letu la *SIDO* limewapa mashine kwa ajili ya kusaga chumvi. Sasa kwa ombi au ushauri huu wa Kamati ambao umetolewa kwamba huduma hii iendelezwe mpaka kule Lindi, tuko tayari kwa sababu watu wetu wa *SIDO* wanadhani kwamba itakuwa ni njia bora zaidi kueneza huduma hii hatimaye tuweze kupata chumvi ambayo inalingana na mahitaji kuondokana na malalamiko haya ambayo tunaendelea kuyapata kila siku. Kwa hiyo, katika hili la chumvi, Shirika letu la *SIDO* limekwishaanza kufanya maandalizi hayo, lilianza katika maeneo mengine ya Mtwara lakini huko Lindi pia litafikishwa. Kwenye taarifa imezungumziwa kwa kirefu kidogo kuhusu utaratibu wa ununuzi wa mazao hasa korosho Mikoa ya Kusini. Sasa nataka tu niseme kwamba nadhani taarifa hii ilipokuwa inaandaliwa kwa sababu ni taarifa ya mwaka 2006 tulikuwa hatujafikia hatua ya uanzishaji wa utaratibu huu mpya ambao tumeuanza hivi karibuni wa *warehouse resist system* ambao umekwishaanza katika Mkoa wa Mtwara kwa mwaka huu. Lakini

azima yake ni kuhakikisha kwamba utaratibu huu unaenea hata katika mikoa mingine ya Lindi, Pwani pamoja na maeneo mengine yanayolima korosho. Kwa hiyo, tunadhani kwa sababu kumekuwa na mafanikio ya kuridhisha katika mkoa huu wa Mtwara tulioanzia, kwa hakika tutakapokwenda katika mikoa mingine hili suala la ununuzi wa korosho pamoja na kusuasua kwa bei ambako kunatokana na ulanguzi pengine tutakuwa tumefika mahali pa kulitafutia ufumbuzi tatizo hili.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ambalo nataka nilielezee ni kwamba taarifa imeeleza juu ya kuwasaidia wajasiriamali wadogo kuweza kuzalisha bidhaa ambazo zinakidhi ubora na vilevile kuwatafutia masoko. Kazi hii tumeendelea nayo kwa sababu Shirika letu la *SIDO* wakishirikiana na Shirika la Viwango Tanzania *(TBS)* mara kwa mara tunaendesha maonesho pamoja na mafunzo ambayo yanawapa wajasiriamali ujuzi wa kutengeneza bidhaa zinazokidhi viwango lakini wakati huo huo kuwatafutia masoko. Lakini sio kwa kuwatafutia masoko vilevile kubadilishana uzoefu wanapokuwa katika maeneo yale kwa sababu bidhaa zile wanazozitengeneza zinakuwa ni za aina mbalimbali.

Kwa hiyo, niliona yale yaliyogusiwa katika Wizara yetu niyatolee taarifa kwa kiwango hicho na nimalizie kwa kuwashukuru sana Wajumbe wote wa Kamati kwa ushirikiano tuliokuwa nao. Tunaendelea kurudia kuahidi kwamba tutaendelea kushirikiana nao katika kufanya kazi za Wizara na tunaomba wasisite wakati wote watakapokuwa na lolote la kutushauri au kutuelekeza, utakuwa ni wajibu wetu kufanya hivyo.

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo, nakushukuru sana na nashukuru sana Taarifa ya Kamati. (*Makofi)*

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, na mimi nataka kuchukua nafasi hii kukushukuru wewe kwa kunipa fursa hii ili na mimi niweze kuchangia hoja za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji na Biashara.

Mheshimiwa Spika, natumia nafasi hii vilevile kumshukuru kwa dhati Mheshimiwa William Shellukindo, Mwenyekiti wa Kamati ya Uwekezaji na Biashara pamoja na Kamati yake kwa ujumla kwa kazi yao nzuri. Wizara yangu imefaidika sana na ushauri na maoni ambayo yamekuwa yakitolewa na Kamati hii mara kwa mara na nawaomba waendelee kufanya hivyo hivyo.

Mheshimiwa Spika, kama jinsi Taarifa ya Kamati ya Uwekezaji na Biashara inavyofafanua pamoja na matatizo yaliyojitokeza kwenye sekta za nishati na madini yapo maeneo ambayo Wizara imefanya vizuri na yako maeneo mengine jitihada za zaidi zinahitajika. Tutaendelea kuthamini na kutumia ushauri wa Kamati ili kuongeza ufanisi na tija ya utendaji kazi wa Wizara katika kusimamia sekta ya nishati na madini.

Mheshimiwa Spika, katika upande wa sekta ya madini kuna hoja mbalimbali zimejitokeza. Napenda niungane na Kamati ya Uwekezaji na Biashara kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kuunda ama kutangaza kuunda Tume Maalumu ya kufuatilia Sera ya Madini, Sheria ya Madini na Mikataba ya Madini. Nina imani kuwa Tume hii

itasaidia kuweka wazi zaidi masuala ya sekta ya madini kuwa mapana zaidi na kutoa ushauri stahili kwa lengo la kuhakikisha kwamba sekta ya madini inachangia ipasavyo katika pato la Taifa.

Mheshimiwa Spika, katika hoja mbalimbali zilizotolewa, zimetolewa hoja kwamba wananchi wanapohamishwa kwenye maeneo wakati migodi inapofunguliwa hawapati fidia stahili. Kwanza, nataka kurudia ambalo nimekuwa nakilirudia mara kwa mara kwamba wakati wa utafutaji mtu akipata *prospecting license* hiyo haina maana kwamba wananchi katika eneo husika wanahamishwa, wanakaa pale pale na mtafutaji anaendelea kutafuta. Akiwa anahitaji eneo *specific* labda kwenye shamba la mtu ili achoronge pale ndipo itabidi azungumze mwenyewe na yule mwenye eneo hilo ili aweze kulitumia na kumfidia kwa kazi hiyo.

Kazi ya kuhamisha wananchi, ama kuwafidia wahame eneo huwa inakuja wakati tayari mwekezaji amekwishapata leseni ya uchimbaji. Katika mchakato mzima wa kuwafidia wananchi kwanza wananchi ambao wako kwenye eneo ambalo linahusika huorodheshwa na kwa kutumia Serikali za Vijiji, Serikali ya Wilaya na Mkoa ili kupata idadi ya wananchi hao ambao wako katika sehemu ile. Tathmini hufanywa na mdhamini wa Serikali lakini vilevile wakati anafanya tathmini hii vilevile viongozi wale niliowataja huwa wanashirikiana na uongozi wa Serikali za Vijiji, Wilaya, Mkoa, Wizara yangu na uongozi wa Kampuni na wenyewe huhusika. Jambo ambalo limekuwa likijitokeza mara kwa mara ni kwa wananchi kulalamikia viwango vya fidia kwamba ni vidogo.

Mheshimiwa Spika, inawezekana kuwa viwango vya sasa ni vidogo lakini ndivyo viwango ambavyo vipo kwa mujibu wa sheria. Hata hivyo Kampuni kupitia Wizara yangu tumekuwa tukiwashawishi na wenyewe wamekuwa wakifanya hivyo. Kampuni zinatoa nyongeza juu ya fidia ya sheria kwa kutumia utaratibu wa *exagratia* kwa lengo la kudumisha mahusiano na wananchi waliohamishwa katika maeneo yao ikiwa ni pamoja na kuwajengea nyumba. Ni kweli katika baadhi ya maeneo kumekuwapo na udanganyifu uliosababishwa na watu wasiostahili fidia na wale waliolengwa kutolipwa. Serikali imekuwa kila ikibaini inachukua hatua, kwa mfano, kasoro hizo zilijitokeza sehemu za Geita na hatua zilichukuliwa. Wizara yangu itaendelea kushirikiana kwa karibu na Serikali za Vijiji na uongozi wa Wilaya na Mikoa husika ili kuhakikisha kuwa kasoro hizi hazijitokezi.

Mheshimiwa Spika, pamejitokeza suala la kwamba wananchi kwenye maeneo hayo wanaomiliki ardhi ama wananchi au Halmashauri zipewe hisa. Kwa sasa hivi ardhi na rasilimali ya madini ni mali ya Taifa, mmiliki wa ardhi hana fursa ya kuingia mkataba kwa lengo la kupata hisia kwenye Kampuni ya uchimbaji wa madini kwa kuwa tu ni mmiliki wa ardhi. Kwa sasa hivi ndiyo sheria yetu ilivyo na ndiyo tunaitumia mpaka pale itakavyobadilishwa vinginevyo.

Mheshimiwa Spika, umepokewa vilevile ushauri wa kuongeza thamani madini yetu. Ushauri huo tumeupokea, Serikali inatambua umuhimu wa kuanzisha viwanda vya kukata madini hapa nchini kwa lengo la kuyaongezea thamani. Hata hivyo, Serikali

ilikwishaanza kuchukua hatua kuhakikisha kuwa madini yanaongezwa thamani hapa nchini. Hatua zilizochukuliwa ni pamoja na kutoa fursa (*incentive)* katika sheria zetu. Katika sheria ya madini tumeweka kwamba mrabaha utakuwa asilimia 0 kwa madini ya vito yanayosanifiwa hapa nchini. Hii ilifanyika kwa nia ya kutoa motisha ili wawekezaji wa ndani ama wa nje waweke viwanda vya namna hiyo hapa nchini. Wizara yangu inaimarisha vilevile kituo cha Arusha kwa kuanzisha sehemu ya utakaji na uchongaji wa madini ya vito.

Mheshimiwa Spika, pametokea hoja ya uchimbaji wa vito *gemstones* kwamba ufanywe na wazalendo ama kama wazalendo hawawezi waingie ubia na wale wa nje ilimradi hawafanyi hivyo watu wa nje peke yao. Ushauri tumeupokea, hata hivyo, kwa sasa chini ya kifungu Na. 8(3) cha Sheria ya Madini ya Mwaka 1998 wageni hawaruhusiwi kupewa leseni ya uchimbaji wa vito bila ya kuwa na Watanzania wenye hisa zisizopungua asilimia 25. Lengo la kifungu hiki ni kuhakikisha kuwa Watanzania wanashiriki katika uchimbaji wa madini ya vito. Hapa naomba tuzingatie kwamba sheria hii ni ya mwaka 1998, kwa hiyo, wale ambao walikuwa wamepata hivyo kabla ya sheria hiyo kuwepo hatuwezi kuiondoa.

Mheshimiwa Spika, niende kwenye sekta ya nishati. Pamezungumziwa kwamba Shirika la Petroli liwezeshwe zaidi. Tunakubaliana na Kamati kuhusu umuhimu wa Shirika la Maendeleo ya Petroli *(TPDC)* kuwezeshwa kifedha. Wizara imetumia ushauri wa Kamati na inaandaa hoja ya kupeleka Serikalini ili *TPDC* kuruhusiwa kutumia sehemu ya mapato yanayotokana na mauzo ya gesi. Sitaki baadaye nije ninukuliwe kwamba Serikali ilisema kwamba mapato yatakatwa, yako wapi? Tumeandaa rasimu yatakwenda Serikalini, tutaujadili kwa nia kwamba tukikubaliwa sasa kama Wizara na tunaomba Kamati itusaidie tukifanikiwa sisi na Kamati tunakuwa wamoja kwenye hili, basi na *TPDC* ipate *retention* kwenye mauzo ya gesi.

Kufuatilia kukamilishwa kwa *Business*, hapa pamezungumziwa juu ya kuanzishwa kwa *Strategic Oil Reserve* kama tulivyosema wakati kwenye bajeti yetu tulivyokuwa tumetangaza. Sasa hivi *TPDC* wamekwishatengeneza *Business Plan* imekwishamalizika. Wizara imeandaa rasimu ya Waraka wa Baraza la Mawaziri kuhusu *TPDC* kuwezeshwa kuingia tena kwenye biashara ya mafuta pamoja na kuanzisha *Strategic Oil Reserve*. Wakati nazungumza sasa hivi Wizara yangu imekwishaandaa warsha ya kujadili mapendekezo yatakayopelekwa Serikalini kuhusu suala hili. Warsha itafanyika tarehe 22 Novemba, 2007.

Waheshimiwa Wabunge wamekaribishwa kupitia uwakilishi kutoka kwenye Kamati za Uwekezaji na Biashara na Uchumi na Fedha za Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na Baraza la Wawakilishi la Zanzibar. Kamati imezungumzia juu ya deni la *ADAX* kwa *TPDC* kwa *US Dollar* takriban 1.9 *million*. Kimsingi hili deni limechukuliwa na Serikali kama tulivyoshauriwa na Kamati.

Mheshimiwa Spika, mapendekezo mengine ya Kamati yalihusu matumizi ya jengo la Mafuta *House*. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba *TPDC* imekwishapewa ghorofa 7 katika jengo hilo na ghorofa hizo zinatosheleza mahitaji ya

*TPDC*. Aidha, kuhusu *National Housing Corporation* wameshakubaliana na *NSSF* kurudishiwa fedha zao zote walizowekeza kwenye jengo hilo.

Mheshimiwa Spika, pametokea hoja ya mpango kabambe wa umeme ambao unahusisha *power masterplan. System master plan* ni mpango muhimu unaotumika katika dira ya kuendeleza sekta ya umeme. Mpango kama huo unaandaliwa na tayari *load forecast* ilikwisha tayarishwa. *Load forecast* ni matarajio ya matumizi imekwishaandaliwa na imekwishawakilishwa na kujadiliwa na wadau. *List cost generation* hivi vituo ambavyo namna gani tunaweza kuvipanga ili tuanze na vile ambavyo vinazalisha kwa gharama kidogo na *transmission expansion* kuongeza usambazaji hiyo ripoti inatarajiwa kukamilika mwishoni mwa Desemba mwaka huu.

Hizo ripoti mbili ambazo nimezungumzia *Load forecast* na *List cost generation plan* na *transmission expansion,* majumuisho ya ripoti zote zilizotajwa hapo juu yatakamilika mwezi Februari, 2008 ambapo miradi yote itaainishwa ikizingatia gharama na ratiba ya utekelezaji. Miradi iliyotajwa kwenye taarifa ya Kamati itakuwa sehemu ya mpango huo.

Mheshimiwa Spika, Kamati imezungumzia na imetoa mapendekezo kwa Serikali kuhusu kununua *IPTL*. Masuala ya *IPTL* yanazingatiwa kama ilivyoainishwa na Kamati, zoezi limechukua muda mrefu na ni kweli hii inatokana na sababu kuwa uamuzi hautokani na upande mmoja tu wa Serikali, ni lazima pande zote husika zipate muafaka ikiwa na maana ni Serikali wana hisa kwenye hiyo Kampuni na wale ambao walitoa mkopo kwenye Kampuni. Serikali imeagiza Kamati inayojadiliana na *IPTL* iongeze ufanisi ili muafaka upatikane mapema zaidi.

Mheshimiwa Spika, sasa kuhusu suala nyeti kuhusu mkataba wa *Richmond Development Corporation*. Kwanza, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba Wizara yangu ina ushirikiano wa karibu sana na Kamati ya Uwekezaji na Biashara. Huu ushirikiano umedumu toka muda mrefu. Toka nilipoingia Bunge hili tu mimi nilikuwa mwanachama wa hiyo Kamati na bahati nzuri mpaka sasa hivi naendelea kuwa mwanachama wa hiyo Kamati kwa maana kwamba inasimamia sekta yangu. Kawaida si vizuri wala si busara kwa Waziri anayehusika na sekta kupingana ama kubishana na mjumbe wa Kamati ambayo inasimamia sekta yake. Lakini napenda nitofautiane kidogo na kauli aliyotoa Mheshimiwa Ole Sendeka kwamba Wizara yangu haikutoa ushirikiano kwa suala hili la *Richmond*.

Mheshimiwa Spika, Mwenyekiti atapata nafasi ya kujumuisha na nafikiri ataniunga mkono kwamba mimi kama Waziri mwenye dhamana ya Wizara ya Nishati na Madini, sijawahi kupokea taarifa ya Kamati kutaka Mkataba wa *Richmond* ama kuhojiwa kutoa taarifa ya kina kuhusu *Richmond.* Hata hivyo, Serikali imepokea na kutafakari taarifa ya Kamati iliyowasilishwa leo hususan suala lote la jinsi Kampuni ya *Richmond* ilivyopatikana.

Mheshimiwa Spika, kimsingi, Serikali haina pingamizi lolote juu ya mapendekezo ya Kamati. Kama inavyofahamika, Serikali ilishughulikia suala la umeme wa dharura katika mazingira magumu, lakini ilifanya kazi hiyo kwa nia njema, kwa uadilifu, kwa uwazi na kwa kufuata taratibu kulingana na mazingira yaliyokuwepo. Nataka kulihakikishia Bunge lako Tukufu kuwa Serikali haina kitu cha kuficha.

Bunge lako tukufu likiridhia hoja ya uundwaji wa Kamati Teule kuchunguza jinsi Kampuni ya *Richmond* ilivyopatikana, kama nilivyokwishasema, Serikali haina pingamizi na pendekezo hilo na itatoa ushirikiano wake wa dhati kwa Kamati hiyo na kuhakikisha kuwa Kamati inapata nyaraka zote, inapata taarifa zote itakazozihitaji. Lengo ni kukamilisha suala hili kwa kuhakikisha kuwa ukweli wote unafahamika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa sababu tungali na muda kidogo na kwa ruhusa ya Mwenyekiti wa Kamati, nitapitia tu masuala mbalimbali yaliyojitokeza kwa wachangiaji. Hii ninaifanya kwa sababu Mwenyekiti ameniruhusu. Nitaanza na Mchango wa Mheshimiwa Habib Mnyaa ambapo amezungumzia mitambo ambayo iko Mwanza. Mwezi wa tatu mkataba unamalizika, inaondolewa, tutafanya nini? Kweli Mheshimiwa Mnyaa ni mtaalamu katika mambo ya umeme na anajua kwamba tuliweka mitambo hii ili iweze ku-*boost Grid* ama ku-*stabilize Grid* ya Taifa kwa sababu uzalishaji wote unatokea huku na *Grid* yetu karibu sasa hivi imelemewa kimzigo.

Lakini Mheshimiwa Mnyaa nataka kumhakikishia kwamba Serikali inalitambua hilo na katika *Financial Recovery Plan* ya *TANESCO* ndiyo sababu imeweka kipaumbele katika kuimarisha *Grid* ya Taifa ambapo kuna mpango wa kuweka njia nyingine sambamba ya *220KV* toka Iringa – Mtera – Dodoma – Singida – Shinyanga. Tunafahamu kwamba hilo likifanyika *Grid* yetu itakuwa ime-*stabilize* na ingawa tuna sababu ya kuwa na vyanzo vya huko lakini hatutakuwa na haja ya kuendelea kuwa na gharama kubwa…..!

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Spika, Mwongozo wa Spika!

**SPIKA:** Mwongozo wa Spika!

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Spika, wakati Waziri wa Nishati na Madini alipokuwa anachangia, alisema kwamba nilipokuwa nachangia nilisema kwamba Wizara yake haikutupa ushirikiano wa kutosha. Tulimwomba atupe mkataba wa Richmond/Dowans mbele ya Kamati ya Uwekezaji na Biashara. Mpaka tunapozungumza, hajaleta mkataba mbele ya Kamati hiyo! Je, huo ndiyo ushirikiano anaomaamisha Waziri kuwa ni ushirikiano alioutoa kwa Kamati wakati amekataa kutoa mkataba mpaka leo tunapozungumza? Naomba Mwongozo wako! *(Makofi)*

**SPIKA:** Hilo halihitaji mwongozo wa Spika hata kidogo. Waziri mwenyewe ana uwezo kabisa wa kulijibu! *(Makofi/Kicheko)*

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, nafikiri hili suala nimesema kwamba nitaliachia kwa Mwenyekiti, kwa sababu tunajua taratibu za kuomba nyaraka, mpaka sasa hivi sina chochote. Lakini labda aliambiwa ama alilete, kama anavyo atalileta. Nilivyosema si kawaida ya Waziri mhusika kuingia katika malumbano na mjumbe wa Kamati inayosimamia sekta yake. Kwa hiyo, nitaomba tu niseme kwamba mimi sikuipata, labda anaweza kuwa ameileta, lakini mimi sijaipata, ndiyo nimesema.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mnyaa amezungumzia hasara iliyopatikana na akalinganisha kukodisha na kununua. Ni kweli katika taratibu za kifedha huwa unaweza ukalinganisha na hiyo unalinganisha ili ufanye uamuzi, ununue, ukodishe ama u-*lease*.

Hizo ni taratibu za kifedha. Lakini unapolinganisha gharama, unalinganisha machungwa kwa machungwa ama wengine wanasema *apples* kwa *apples*. Ni kwamba tunapolinganisha hili tunaweza kulinganisha katika Dunia nzima, mitambo inayonunuliwa na mitambo tunayonunua tumenunua kwa gharama iliyo sawa ama tumepunjwa. Tunapokodisha, tunaangalia tulivyokodisha, gharama ya kukodisha tuliyokodisha na wanavyokodisha wengine ni sawa ama tumepunjwa. Lakini tukilinganisha gharama za kukodi na gharama za kununua, wakati mwingine inakuwa si sahihi.

Mheshimiwa Spika, Serikali inajua kwamba kulikuwa na ulazima wa kununua mitambo yake na kweli ingekuwa rahisi kuinunua ile mitambo. Lakini wakati umepatwa na shida na tunajua kwamba kutengeneza mitambo yako kunachukua muda mrefu, ndiyo unaingia gharama ya haraka ya kukodi ili baadaye ukiwa na ya kwako, utaendelea nayo ya kudumu.

Kwa hiyo, sina tatizo na hoja yake kwamba kweli kama tungejua mapema miaka iliyopita huko kwamba hili litatokea, tungeanza kujenga mitambo yetu na tusingekuwa na haja ya kukodisha kwa sababu kuwa na mitambo yetu ni rahisi. Lakini mpaka *Richmond* wanaondoka, nataka kukulihakikishia Bunge lako tukufu kwamba haikuwahi kulipwa hata senti moja na Serikali.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Kabuzi, nataka kutoa shukrani na pongezi alizoziweka kwenye Wizara yetu jinsi tunavyoshughulikia suala la wachimbaji wadogo wadogo. Tuliliweka kwenye bajeti yetu na ni kweli tunalifuatilia. Tunafuatilia kwamba maeneo yoyote ambayo tunayapata ambayo yanafaa kwa wachimbaji wadogo, tunawapatia wachimbaji wadogo, lakini kwa utaratibu wa kisheria, siyo kuingia pale kiholela na kuharibu mazingira. Tumewashawishi wawekezaji wakubwa pale ambapo utafiti umeonekana kwamba hakuna rasilimali za kutosha kuchimba kwa faida kwa kutumia mwekezaji mkubwa, basi waachie maeneo hayo kusudi tuweze kuyapangia wawekezaji wadogo wadogo. Mpaka sasa hivi wanaitikia wito wetu na ndiyo sababu tumefanikiwa kwenye maeneo ya Mheshimiwa Kabuzi na maeneo mengine tunaendelea taratibu kwa sababu utaratibu huo tumekwishajiwekea kama Wizara.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mhonga Ruhwanya amezungumzia mambo mengi, kumpongeza Rais, amekwishampongeza, lakini mimi nimeiboresha zaidi. Lengo la Mheshimiwa Rais si mikataba tu, anataka sekta nzima iangaliwe na tuangalie na nchi nyingine zinafanyaje. Kwa hiyo, ni pana zaidi ya ile mikataba aliyozungumzia. Tunazungumzia sera, tunazungumzia sheria zenyewe, tunazungumzia na mikataba kwa ujumla wake.

Nafikiri atakapounda Kamati hiyo, wakitufikia sisi Wabunge, tutatoa ushirikiano na Kamati hiyo. Amezungumzia tatizo la Kigoma, ni kweli nalifahamu na ni kweli amekuwa analifuatilia sana suala hili mpaka nimepewa vi-*memo* nilipokuwa nimekaa kwamba "huyu binti lini umemwambia utakwenda Kigoma?". Kwa sababu siye yeye tu, kweli Wabunge wote wa Mkoa wa Kigoma wamekuwa wanalifuatilia hili na mimi nitakwenda kule.

Mheshimiwa Spika, suala la Mitambo ya Mwanza, tumelifikiria na Rais mwenyewe amelizungumzia. Lakini tunaiangalia kwa njia hii kwamba zile jenereta za Mwanza ni za *high speed*. Na mitambo ya *high speed* inahitajika kwenye maeneo ambako unataka ku-*boost Grid* kwa muda ama kwa *standby*. Umeme umekatika, unaiwasha baada ya saa tatu, mbili, ukirudi, unatoa. Ukitaka kwenye maeneo ambayo mitambo hiyo itakuwa inaendelea muda wote, lazima uwe na mitambo ambayo ni ya *low speed*.

Mheshimiwa Mnyaa anaweza kukubaliana na mimi juu ya hilo. Kwa hiyo, ndiyo sababu tumeona kwamba badala ya kuleta mitambo ambayo inaweza ikaleta matatizo, afadhali tuagize mtambo ambao utaweza kukaa pale kwa muda mrefu na wa kudumu ambao unaweza kufanya kwa saa 24. Hata hivyo, siyo kwamba mpaka 2009 Kigoma watabaki vilevile, vipuri tumekwishaviagiza, mapaka sasa jenereta ambazo zinafanya kazi ni tatu Kigoma. Lakini zinatoa umeme kidogo, *1.5MW* ambapo sasa hivi Kigoma mnahitaji *5MW*.

Lakini vipuri vya kutengeneza jenereta 4, vimekwishafika Kigoma sasa hivi na wataalamu wa kutengeneza hiyo mitambo wako Kigoma wanafanya hivyo. Na ninapokwenda Kigoma, nakwenda kuangalia kasi wanayofanya na kuwahimiza kufanya hivyo. Wakishamaliza hilo, mitambo hiyo ikiishamalizika, tutaweza ku-*boost* ile jenereta ya Kigoma mpaka ifikie *3.5MW*.

Tutakuwa bado tuna upungufu wa *1.5MW* hivi ambapo ule mtambo tunaoufikiria wa *2MW* ukifika, utaweza kutosheleza na wakati ule, mpango ule wa Malagarasi ambao sasa hivi tumepata pesa kutoka kwa *MCC*, utakuwa unakamilika. Ule mpango wa Malagarasi utakwenda mpaka 2012. Ukishakamilika ule wa 2012, ule mtambo ambao tutakuwa tumeununua wa *2MW* tutautafutia mahala pa kuuhamishia na sehemu nzuri ambayo tunaweza kuhamishia kwa haraka haraka, tunafikiria itakuwa ni Kibondo.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Ole-Sendeka, nimekwishazungumza. Nilikuwa na hilo tu kwamba hiyo taarifa mimi nilikuwa sina rasmi ambayo anaizungumzia, lakini inawezekana labda ilikuja, sikuiona, lakini ndivyo ilivyo.

Mheshimiwa Kasembe, amezungumzia mengi, lakini kubwa amezungumzia kwamba Wilaya zote za Mtwara na Lindi hazijawahi kufikiwa na umeme wa *Artumas*. Hilo tunalijua na tunalifahamu. Tunaharakisha kufanya mkataba wa *Franchise Agreement* wa *Artumas* kusudi ukimalizika waanze kufanya shughuli hii ya usambazi wa umeme katika maeneo yote ambayo alikuwa ameyazungumzia.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Dr. Binilith Mahenge amezungumzia kuwa kulikuwa na mpango wa *Master Plan* ambao haukutekelezwa kwa muda mrefu na labda ndiyo sababu tumefikia kiasi hiki.

Ni kweli huo mpango ulikuwa umesitishwa wakati ule ambapo *TANESCO* ilikuwa imewekwa katika programu ya kubinafsishwa, ilikuwa *specified* na kwa kipindi cha miaka 10 ilikuwa kwamba hakuna kinachofanyika, tulikuwa tunangojea *TANESCO* iuzwe.

Lakini baada ya Serikali kubadilisha msimamo wake ule wa kuuza *TANESCO*, sasa hii *Power Master System* iliyokuwa imepangwa wakati ule, sasa hivi imekuwa *revised*. Mshauri yupo kama nilivyowaelezea na sasa hivi tuko katika mchakato wa mwisho na kufikia mwezi wa pili mwaka ujao, *Master Plan* yetu itakuwa imekwishakamilika.

Mheshimiwa Spika, upande wa madini, nakubaliana naye. Katika Madini tuna watalaamu kama nilivyosema pale awali. Wataalamu tunao, wanafanya kazi yao vizuri, lakini kuna *specialized areas* ambazo kweli zinahitaji wataalamu. Tunachukua ushauri wake, tutaendelea kushauriana na wenzetu *Development Partners* na kwa sasa hivi najua tuna *offers* kutoka Canada na Norway juu ya wataalamu wetu kujihusisha katika hizi *specialized areas* kusudi tuweze na sisi kuzungumza lugha moja na wenzetu wanapokuja.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Dr. Sigonda amezungumzia juu ya *PL* za leseni ambazo maeneo ya Chunya yamekuwa ni muda mrefu lakini mpaka sasa hivi hakuna *Mining Licenses*. Na ni kweli kwamba maeneo ambayo yana *Prospecting Licenses* za muda kwa wale ambao wameingia kwenye maeneo yale ya kuitisha muda huo yakahuishwa mara tatu tukaona kwamba hawana nia ya kutuingiza iwe *mining license*.

Tunawatafuta walio bora zaidi na nafikiri sheria ambayo ilikuwa inaongoza hili, tutaileta. Kwa sababu tunadurusu sheria ya madini na baadaye itabadilisha sheria ya madini na Mheshimiwa Rais amekwisharidhia mchakato huo.

Tutaangalia namna gani vilevile hizi *Prospecting Licenses* haziwezi kutumika watu wakawa nazo wanazibadilisha badilisha mpaka wanazirudia rudia, lakini hawaingii katika uchimbaji wa madini ambavyo tunapoteza kile tunachokuwa tunakitafuta.

Nampongeza *Engineer* Laus Mhina kwa kutukumbusha juu ya *renewable energies* na tuna mikakati kama hivyo hivyo kama tulivyozungumza. Mheshimiwa Dr.

Slaa amezungumza na tunaafiki Kamati Teule ili ifanye hayo yote ambayo alikuwa anafikiri ameyazungumzia na kuhakikisha kwamba hakuna kinachobaki.

Mheshimiwa Ruth Msafiri amezungumzia kwamba maeneo ya wananchi yakipatikana madini watambuliwe kuwa wawekezaji wa kwanza. Nakubaliana naye lakini atambue kwamba madini hayapatikani hivi hivi, lazima uwekeze rasilimali kubwa ili ufanye utafiti, ndiyo tunafanya *prospecting licenses*.

Kwa hiyo, kwa sasa hivi hilo hatuna lakini linajadiliwa. Vilevile amezungumzia juu ya umeme vijijini na kusema kwamba lazima tuwe na umeme vijijini kusudi tuweze kufikia malengo ya *Millennium*, MKUKUTA. Nakubaliana naye mia kwa mia na ndiyo sababu tumeanzisha Sheria ya Umeme Vijijini ili kufanya hayo ambayo amaezungumza.

Mheshimiwa Spika, hayo ndiyo ya nyongeza, ilikuwa ni kusaidia kujibu hoja kusudi Mwenyekiti wangu wa Kamati ya Kudumu ya Uwekezaji na Biashara awe na maeneo machache ya kuweza kujibu. Kwa hayo machache, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii kuchangia hoja ya Kamati hii. Asante sana! *(Makofi)*

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. VUAI ABDALLA KHAMIS:** Mheshimiwa Spika, kwanza nakupongeza kwa kuliongoza Bunge la Jamhuri ya Muungano na kutupa fursa za kuchangia bila ubaguzi na upungufu wowote. *Richmond/Dowans* tulikuwa na matumaini mazuri na pia kutegemea matunda yao lakini kwa kweli walitupa mazungumzo mitaani na hata vyombo vya habari. Kwa hiyo, naiomba Serikali kuondosha tuhuma kama ilikuwapo. Serikali isimamie mikataba na Kamati ya Bunge inapofanya kazi yake ipewe nafasi yake.

Tunafaidika sana na madini Tanzania. Kwa hiyo, wachimbaji wakubwa wapewe haki zao na wachimbaji wadogo pia. Lakini kwa nini wachimbaji wadogo ambao wazalendo wasipewe misaada wakue? Kuundwa kwa Kamati Teule mimi sina kipingamizi kwani itarahisisha kazi na kutuwezesha kuona ubaya na uzuri wa matatizo yaliyojitokeza.

Mheshimiwa Spika, Tanzania ni nchi yetu wenyewe. Kwa hiyo wajenzi wa Tanzania ni sisi wenyewe. Hivyo, naiomba Serikali isimamie mazuri na yale mabaya yakemewe na hatua zichukuliwe. Kwa niaba ya wananchi wa Magogoni naunga mkono hoja.

**MHE. TEDDY LOUISE KASELLA-BANTU:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nami nafasi kuchangia hoja iliyotajwa hapo juu. Awali ya yote, kwa kuwa sijasema tangu tukio la msiwa wa marehemu Salome Mbatia aliyekuwa Mbunge na Naibu Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Bukene, naomba kutoa salamu za rambirambi kwako Mheshimiwa Spika, familia ya Dr. Mbatia na kwa ndugu na jamaa wote walioguswa na msiba huu. Nawaombea moyo wa subira na roho ya Marehemu Salome Mbatia ipumzike kwa amani. Amina!

Naomba kukumbushia Wizara ya Nishati na Manidi, kwamba ni ustaarabu na hapana budi umeme wa kijiji cha Bukene tuhitimishe. Kwa kweli ni jambo la kushangaza kuwa bajeti ilipitishwa 2006/2007 kwa ajili ya umeme wa Bukene na Ndala, na kwa sababu zisizoweza kuzuilika (sitaki kuchimba zaidi), fedha hizo zilitumika vinginevyo na hivyo kwenda kinyume na bajeti iliyopitishwa. Lakini yote ni sawa tu kwa manufaa ya Taifa. Bajeti ya 2007/2008 ambayo tumeiptisha Juni/Julai, 2007, kwa misingi hiyo zile shilingi milioni 50 kama kianzio au kuonyesha mradi huu unaoendelea sasa kwa kusikitisha hadi hivi leo hakuna hata dalili ya kuanza kazi. Ni busara kabisa shughuli hii iwe imeanza sasa ili kuhitimisha suala hili. Ni vema kuhitimisha kabla ya kuanza mradi mwingine. Naomba kuwasilisha.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini, nakushukuru sana kwa uchambuzi huo uliotoa. Kwa hapa ndani mnaonekana kama wewe na Mwenyekiti mna ushirikiano, lakini basi sasa namwita mtoa hoja Mwenyekiti wa Kamati ya Uwekezaji na Biashara, Mheshimiwa William Shellukindo.

**MWENYEKITI WA KAMATI YA UWEKEZAJI NA BIASHARA – MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi tena hii kwa nia ya kuhitimisha hoja ambayo iko mbele yetu. Lakini kwanza kabisa, napenda kuwashukuru kwanza, wewe mwenyewe, Waziri Mkuu pamoja na Waheshimiwa Wabunge na Mawaziri kwa kusikiliza taarifa yetu na kuichangia vya kutosha. Nawashukuru sana kwa niaba ya Kamati ya Uwekezaji na Biashara.

Mheshimiwa Spika, sasa kama ilivyo kawaida, nitapenda niwatambue ambao walitoa michango. Kwanza, wale waliochangia kwa kuzungumza, wako 13. Napenda niwatambue:- Mheshimiwa Beatrice Shellukindo, Mheshimiwa Mohamed Mnyaa, Mheshimiwa Kabuzi Rwilomba, Mheshimiwa Mhonga Ruhwanya, Mheshimiwa Christopher Ole-Sendeka, Mheshimiwa Mariam Kasembe, Mheshimiwa Dr. Binilith Mahenge, Mheshimiwa Dr. Guido Sigonda, Mheshimiwa Eng. Laus Mhina, Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa, Mheshimiwa Ruth Msafiri, Mheshimiwa Hezekiel Chibulunje, Naibu Waziri wa Viwanda, Biashara na Masoko, Mheshimiwa Nazir Karamagi, Waziri wa Nishati na Madini.

Mheshimiwa Spijka, wale ambao wamechangia kwa maandishi wako 18. Napenda niwatambue:- Mheshimiwa Mwinchoum Msomi, Mheshimiwa Maria Hewa, Mheshimiwa, Mwanawetu Zarafi, Mheshimiwa Dr. Ali Taarab Ali, Mheshimiwa Lucas Selelii, Mheshimiwa Khadija Al-Qassmy, Mheshimiwa Ania Chaurembo, Mheshimiwa Prof. Raphael Mwalyosi, Mheshimiwa Mkiwa Kimwanga, Mheshimiwa Mohamed Mnyaa, Mheshimiwa George Simbachawene, Mheshimiwa Fatma Fereji, Mheshimiwa Ameir Ali Ameir, Mheshimiwa Susan Lyimo, Mheshimiwa Victor Mambalaswa, Mheshimiwa Benito Malangalila, Mheshimiwa Vuai Khamis na Mheshimiwa Teddy Kasella- Bantu. Labda tungesema taarifa kama hizi ni tofauti kidogo na taarifa au maelezo binafsi au hoja binafsi. Kwa hiyo, katika namna ya kuishughulikia, kwanza mimi kama Mwenyekiti na Kamati yangu tunawasilisha kwa niaba ya Bunge yale ambayo tumeona yafikishwe Serikalini. Kwa hiyo, tunategemea zaidi kupata majibu kutoka Serikalini. Na nawashukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini na

Naibu Waziri wa Viwanda, Biashara na Masoko, kwa kujibu na kutoa maelezo kwenye hoja za Waheshimiwa Wabunge ikiwa ni pamoja na hoja za Kamati yangu ambazo nimezitoa.Kwa upande wangu nadhani mnachotaka kujua ni kama nimeridhika na jinsi walivyojibu. Mimi nimeridhika kabisa na majibu waliyotoa kwa wakati huu. Isipokuwa kuna wenzetu 18 ambao wameleta kwa maandishi, ni marefu sana, kwa hiyo, tumekubaliana na Mheshimiwa Waziri Karamagi atazichukua hoja zao, halafu atashirikiana na Waziri wa Viwanda, Biashara na Masoko kuziangalia hoja hizo tena na kuzitolea maelezo. Ni nyingi sana, 18, kuzisoma zote mpaka kuzielewa itakuwa ni tatizo kidogo.

Mheshimiwa Spika, kwanza, nashukru kwamba waliochangia wote wamegusa sekta zote ambazo tumezielezea: nishati, madini, viwanda, biashara na masoko. Vilevile, majibu yametolewa kwenye sekta zote hizo. Sasa labda itokee tu kuna mtu ambaye alitaka ajibiwe hasa kwenye Jimbo lake kwamba hapa tutafanya hivi na hivi. Nadhani iliyobaki sasa ni kufuatilia wewe Mheshimiwa Mbunge kwamba ulitoa mawazo yako, je, yamefikia wapi? Katika hoja zote nilivyozisikiliza na hizi zilizoletwa kwa maandishi, wote hawa jumla wanakuwa 31. 30 wameunga mkono hoja, isipokuwa mmoja tu kati ya walioandika, yeye hakuunga mkono hoja. Amesema hivi, “hakuna haja ya kuunda Kamati Teule, *Richmond* haikuzalisha umeme ila imekuwa ni Kampuni ya kununua nyumba za Msajili”. Sasa hii ni mpya, sisi hatukuijua hii. Kwa hiyo, tunampongeza na kumshukuru kwa kutupa maelezo hayo mengine ambayo sisi wengine tulikuwa hatuyajui. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, kuna suala moja ambalo pengine hilo inabidi tulitafutie muda tulizungumze la uwekezaji ambalo amezungumza Mheshimiwa Rwilomba na limezungumzwa na Waheshimiwa Wabunge wengine. Nakumbuka Mbunge wa Chunya amelizungumzia, Mbunge wa Makete amelizungumzia na wengine juu ya uwekezaji kwamba hivi ni uwekezaji au ni uchukuaji? Sasa sisi kama Wabunge nadhani tutafute majibu hayo. Hao wawekezaji tulionao kwenye maeneo yetu, majimbo yetu, ni wawekezaji au ni wachukuaji? Nadhani hayo majibu tuyatafute. Mimi nakubali kabisa kwamba kuna wengi hawakwenda kuwekeza. Kwanza, kuna wawekezaji wa namna mbili: Kuna wawekezaji ambao wanakuja yeye na *briefcase* tu na mawazo yake. Anakuja hapa, kila kitu anakipatia hapa pamoja na mikopo. Kwa mfano, kama mkitazama ile taarifa ya *TIB*, unaweza kuona kwamba kuna watu walikuja na wamepata mikopo hapa hapa ya kuwekeza. Hilo ni kundi la kwanza. Hatujakataza hiyo! Anaandika mradi wake unakubalika, unasaidia taarifa, anakwenda kukopa *TIB* na anarudisha, hicho ni kitu kimoja. Lakini kuna wengine wanakuja na fedha zao kabisa. Kwa mfano, mwekezaji yule aliyeko kwenye *Mellenium Business Park* Ubungo ambaye tulimtembelea, yeye ni mtu wa Cyprus, amekuja na dola zake. Hao ndio wachache sana, wengi wanaokuja kuwekeza wanategemea *capital markets*. Akishapata hapa mradi akautengeneza vizuri, anakwenda kukopa kwenye *capital markets* lakini fedha hizo zinapitia kwenye benki kama utaratibu ulivyo. Sasa ni sisi wenyewe sasa tuangalie, hivi ni mwekezaji yupi mwenye manufaa. Yule anayekuja na fedha, nadhani mnampa kipaumbele, yule anayekuwepo hapa kama ni eneo moja hilo anataka kuamua, ni afadhali umpe yule anayekuja na dola atatuongezea zaidi kuliko huyu ambaye yuko sasa hivi, atafutiwe eneo lingine.

Mheshimiwa Spika, nadhani Mheshimiwa Rwilomba, hii hoja tungeizungumza, tuangalie matatizo ya wawekezaji ambao wako katika maeneo yetu. Mimi naamini kwamba kuna wengine wana nia nzuri sana, lakini kuna wachache pengine ni watu wa kuja kuchukua tu na anachukua nafasi hiyo, pengine eneo analofanyia kazi hatuna utalaamu nalo sana, mathalani, Mheshimiwa Beatrice Shellukindo alizungumzia habari ya kuchimba na kuondoka kwa muda mrefu. Kuna mwingine wamesema ametafiti kwa miaka 20, bado hajachimba, je, kama utafiti wenyewe ni miaka 20 na uchimbaji utachukua miaka mingapi? Nadhani hii ni juu ya Serikali kwa kweli kama tunamjua hasa, tuwaandikie Mawaziri kwamba huyu tunadhani ni mwekezaji mbababaishaji. Nadhani itatusaidia zaidi kumwandikia Mheshimiwa Waziri kwamba huyu mliyempa *License* ya Utafiti, siyo mtafiti ni mbababaishaji ili wachukue hatua. Hiyo itatusaidia sana maana yake Mawaziri hawako kila mahali, lakini sisi karibu majimbo yote, Wilaya zote zina Wabunge wako hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna ombi ambalo lilitolewa, sisi tunashukuru sana kwamba Waheshimiwa Wabunge wametupongeza kwa kutembelea maeneo. Nadhani tungefanya hivyo ili tuweze kujibu au kutoa hoja ambazo zina uhakika zaidi. Na tulitoa ahadi kwamba tutatembelea maeneo mengine ambayo yana sekta hizi zinazotuhusu ili tuweze kusaidia kutoa mawazo na kuishauri Serikali ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, hoja moja ambayo haikuwa ya Waziri kujibu ni hoja ya kuunda Kamati Teule. Nadhani maudhui yako kwenye taarifa, sina zaidi ya kuongeza, yale ndiyo ambayo nilipewa na Kamati kuja kuyaeleza. Kama hayakutosheleza basi tuelezwe kwamba hayakutosheleza. Lakini kwa upande wa Kamati, sisi tuliona hili suala kwa sababau limeandikwa mno, ni vizuri kwa vyovyote vile tulitolee majibu na tulifunge, tusitumie muda mrefu zaidi.

Mheshimiwa Spika, sasa nikifika hapa, napenda kutoa hoja, halafu tutaingia kwenye hatua ya pili.

**SPIKA:** Hoja hii ya kwanza ni kuhusu mapendekezo ya jumla ya taarifa ya Kamati. Kwa mujibu wa Kanuni zetu, Kanuni ya 104(i), hoja ile ambayo inahusu jambo mahususi, lazima iamuliwe peke yake, ndiyo maana nadhani kwa kuwa Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Uwekezaji na Biashara ni mzoefu, amesimama hapa ili niweze kuwahoji kwa yale mapendekezo mengine yaliyomo katika taarifa ukiacha jambo mahususi la kuunda Kamati teule ambalo tutaingia baada ya kumaliza hili.

*(Hoja Iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Taarifa ya Kamati ya Uwekezaji na Biashara kwa mwaka 2006 ilipitishwa na Bunge)*

## Hoja ya Kuunda Kamati Teule Itakayochunguza Mkataba wa *Richmond*

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Spika, kwanza, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa niaba ya wajumbe wenzangu wa Kamati ya Bunge ya Uwekezaji na Biashara kwa kunipa fursa ya kuleta hoja hii hapa kwenye Bunge lako Tukufu kwa mujibu wa Kanuni ya 104(1) ya Kanuni za Bunge, Toleo la 2004. Kuletwa kwa hoja hii bila kujali maamuzi kuhusu hoja yenyewe, ni ishara tosha ya ukomavu wa demokrasia katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, msingi wa kuletwa kwa hoja hii unatokana na taarifa yetu kuhusu utekelezaji wa shughuli za Kamati kwa mwaka 2006 kama nilivyokwishaiwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu leo asubuhi na kuitolea uamuzi leo jioni. Ikumbukwe kwamba mwaka 2005 Tanzania ilikumbwa na tatizo la uhaba wa nishati ya umeme katika mikoa yote. Katika kukabiliana na tatizo hili, Serikali iliingia mikataba na Kampuni ya *Richmond* ambayo ilitakiwa kufunga mitambo ya kuzalisha umeme wa dharura.

Mheshimiwa Spika, baada ya kufuatilia taarifa ya Serikali ya Shirika la Umeme *TANESCO* ambalo halikuridhishwa na utendaji kazi wa kampuni ya *Richmond Cooperation* ya Marekani na mrithi wake *Dowans Holdings SA* ya Falme za nchi za Kiarabu, kwa kushindwa kukamilisha mradi wa umeme wa dharura katika muda muafaka yaani ndani ya kipindi ambacho nchi ilikuwa inakabiliwa na tatizo la upungufu wa umeme. Kwa mujibu wa taarifa za kampuni ya *Dowans*, ufungaji wa mitambo ya kuzalisha umeme na kuingiza umeme wenye *Megawalt* 100 kwenye *grid* ya Taifa ulitegemewa kukamilika mwezi Juni mwaka 1007, badala ya tarehe 2 Feburuari, 2007 kama ilivyosainiwa kwenye mkataba miezi kadhaa baada ya hali ya dharura kumalizika.

Mheshimiwa Spika, utendaji kazi usioridhisha wa *Richmond* na ushahidi bayana ulijitokeza pole pole wa kampuni hiyo kutokuwa na uwezo wa kutosha kifedha na kukosa kabisa uzoefu katika miradi ya umeme, umezua masuala mengi miongoni mwa wananchi kuhusu umakini uliotumika katika kuiteua kampuni hiyo kutekeleza mradi nyeti kitaifa wa aina hiyo na wenye gharama kubwa ya shilingi bilioni 172.9/=.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, nakuomba wewe na Bunge lako Tukufu lipokee, lijadili na liamue hoja ifuatayo:-

KWA KUWA suala la tatizo la umeme nchini ni la Kitaifa, na inapotafutwa njia mbadala ya kukabiliana na tatizo hilo la kuzalisha umeme wa dharura, njia hiyo mbadala lazima iwe ya uhakika, hasa kwa kufahamu kuwa umeme ni nishati muhimu hasa katika masuala ya uwekezaji na utoaji huduma muhimu;

NA KWA KUWA kampuni ya *Richmond* ilipewa kazi hiyo ya kuzalisha umeme wa dharura, ilishindwa kufanya hivyo kama ilivyokubaliwa katika mkataba wake na Serikali ambao Kamati haikuweza kuuona; Na Kwa Kuwa suala zima la *Richmond* limezua maswali mengi kwa wananchi ambayo hayana budi kupatiwa majibu ya uhakika na ya kuridhisha, KWA HIYO BASI Bunge liazimie kwamba iundwee Kamati Teule

itakayochunguza mkataba na mchakato mzima uliopelekea kampuni ya *Richmond* kuteuliwa kufanya kazi ya kuzalisha umeme wa dharura. Kamati itakayofanya kazi hii itatumia vigezo vipana zaidi kuliko vile vya makosa ya jinai au ya kijinai vilivyotumiwa na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa *TAKUKURU*.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

**MHE. MOHAMED A. CHOMBOH**: Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwenyekiti kwa hoja hiyo. Waheshimiwa Wabunge hoja iliyopo mbele yetu sasa ni hoja mahususi inayolitaka Bunge letu liridhie kuundwa kwa Kamati Teule ya Bunge kufuatilia suala la *Richmond Development Cooperation* na hiyo naombwa kuiamua chini ya kanuni ya 104 (1). Kwa hiyo, hoja ni je! iundwe Kamati Teule au hapana?

*(Bunge liliafiki kuundwa kwa Kamati Teule ya kuchunguza*
*mkataba wa Richmond Development Cooperation)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge nilikuwa natafakari uwezekano wa hilo kutokea kwamba Bunge laweza kuridhia na kwa sababu mambo kama haya yanahitaji *speed* inayohitajika basi kwa mamlaka niliyopewa na Kanuni ya 104(3) wajumbe wa Kamati Teule watateuliwa na Spika na watachagua Mwenyekiti wa Kamati hiyo miongoni mwao. (*Makofi*)

Ukiendelea Kanuni ya 105 inasema kila Kamati Teule itakuwa na wajumbe wasiozidi watano, na Spika wa Bunge ataamua idadi ya wajumbe inayofaa kuwa kiwango cha mikutano, hapo walikuwa na maana ya akidi ni kosa siyo idadi. Kwa mamlaka hayo nimewateua wabunge wafuatao kuunda Kamati teule mliyoiafiki sasa hivi, ni Mheshimiwa Dr. Harrison George Mwakyembe, Mheshimiwa Eng. Stella Martin Manyanya, huyu ni Mhandisi wa umeme, Mheshimiwa Mohamed Habibu Juma Mnyaa kutoka Kambi ya Upinzani na ndiye Waziri Kivuli wa mambo ya Nishati na Madini na ni mtaalamu, halafu niongeze wengine wawili ambao huwa nawaona ni makini na wafuatiliaji wazuri, Mheshimiwa Lucas Lumambo Selelii na Mheshimiwa Harbert James Mtangi, hao ndiyo watano. Kwenye kikao chao cha kwanza, kama Kanuni ya 105 (1) inavyohitaji watamchagua Mwenyekiti wao, wakishamchagua nitamkabidhi habibu za rejea, kwa sababu Mwenyekiti alikuwa anasema jambo hili unaweza kupanua na mambo mengine hapana! Huwa tunashughulikia jambo mahususi isije ikawa kuingiza *Dowans*, *IPTL*, hairuhusiwi kwa Kanuni, tunashughulikia Richmond. Kanuni zinanisaidia, mchana niliweza kutazama taarifa nzima na nikaona wanachohitaji ni kama ifuatavyo, na hizi ndiyo hadidu za rejea:-

(1). Kubainisha *Richmond Development Corporation* ni kina nani na ni Kampuni ya shughuli zipi na hivyo kupima uwezo wake kupatiwa zabuni ya kuleta nchini na kujenga mtambo wa umeme wa gesi wa Megawati 100.

(2). Kuutathmini mchakato mzima wa jinsi zabuni waliyoshinda *Richmond* ilivyoshughulikiwa kuanzia Kamati ya Zabuni hadi mwisho ili kujiridhisha kuwa sheria, taratibu, miiko na maadili ya Zabuni yanayotawala zabuni za aina hiyo vilifuatwa au vipi.

(3). Kuutathmini Mkataba baina ya *Richmond Development Corporation* na *TANESCO* ili kujiridhisha kuhusu uhalali wa masharti ya Mkataba huo ukizingatia gharama na masharti mengine yakilinganishwa na masharti yaliyomo katika mikataba ya aina hiyo iliyoafikiwa na *TANESCO* na Serikali.

(4). Kubainisha huduma na misaada mbalimbali waliyopewa *Richmond* kama vile kufunguliwa *Letter of Credit* na kupima uhalali wake.

(5). Kuziangalia na kuzitolea maoni taarifa za TAKUKURU, *PPRA* na taarifa zozote nyingine zilizoangalia utaratibu wa zabuni ya *Richmond*. (*Makofi*)

(6). Kuangalia mambo mengine yoyote yenye uhusiano na mchakato mzima wa *Richmond* ili kutoa mapendekezo ya kuboresha taratibu za zabuni kwa siku zijazo, kwa maslahi ya Taifa letu.

Hizi ndiyo Hadidu za Rejea watakazozifanyia kazi Kamati niliyokwishaiteua. Baada ya hayo nitoe tu tangazo kwamba kesho saa saba na nusu Wabunge wote wa Chama cha Mapinduzi nimearifiwa na Katibu watakuwa na Kikao katika Ukumbi wa Pius Msekwa.Katibu amekaribisha ajenda, inaelekea ni kikao cha mambo ya jumla, kwa hiyo, wale wote ambao wana ajenda ambazo wanataka zifikishwe ni vizuri waandike kwa kifupi hata kwa vichwa vya maneno ili ziwe katika mtiririko ambao zitazingatiwa. Kwa kuwa muda uliosalia hautuwezeshi kuendelea na shughuli za Bunge, naahirisha Bunge hadi kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 1.40 Usiku Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Jumatano, Tarehe 14 Novemba, 2007, Saa 3.00 Asubuhi)*